# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 23 Aprili, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao chetu cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Tano.

Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA– KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Buhigwe, Mheshimiwa Abert Obama Ntabaliba.

Na. 112

**Changamoto ya Walimu wa Hesabu na Sayansi**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Walimu wa hesabu na sayansi ni changamoto kubwa ndani ya Wilaya ya Buhigwe:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu katika wilaya hiyo na waliopo sasa ni wangapi?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa vya maabara katika shule za Buhigwe?

**SPIKA:** Swali hilo litajibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa, Mheshimiwa Mwikwabe Mwita Witara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe ina jumla ya shule 19 zenye wanafunzi 6,622. Jumla ya Walimu waliopo wa hisabati na sayansi ni 83 sawa na asilimia 54 ya Walimu 155 wanaohitajika. Mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri Walimu wa masomo hayo kwa awamu na kwa sasa kibali cha kuajiri Walimu 4,549 kimekwishatolewa

ambapo kati ya hao, 1,374 ni wa Masomo ya Sayansi na Hisabati. Utaratibu wa kuajiri Walimu hao unaendelea na watapangwa kwenye halmashauri zenye upungufu mkubwa ikiwemo Halmashauri ya Buhigwe.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018, Halmashauri ya Buhigwe ilipokea vifaa vya maabara kwa shule mbili za sekondari zilizokamilisha ujenzi wa maabara. Vilevile katika Mwaka 2018/2019 Serikali inatarajia kununua na kusambaza vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari 1,250 zikiwemo shule za sekondari katika Halmashauri ya Buhigwe zilizokamilisha vyumba vya maabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Obama, nilikuona.

**MHE. ALBERT N. OBAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nishukuru majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni ukweli kwamba tuna upungufu mkubwa nchi nzima wa Walimu wa sayansi na hesabu na kwenye jibu lake la msingi ameonesha kwamba Buhigwe ina upungufu wa asilimia 46. Sasa na hiki kimekuwa ni kikwazo ambacho kinatufanya kwamba ufaulu wetu uwe mdogo na kule ni pembezoni, kwamba watoto hawawezi kupata namna ya kuweza ku-*access* namna ya kujisomea kwa kufundishana. Je, ni lini itaweka umuhimu wa kuongeza Walimu wa sayansi katika Wilaya ya Buhigwe?

Mheshimiwa Spika, la pili nipongeze wananchi wa Wilaya ya Buhigwe kwa juhudi na kujitolea kujenga maabara na kujenga madarasa. Je, ni lini Serikali italeta sasa vifaa vya maabara kwa sababu tunaendelea kukamilisha sasa maabara katika shule nyingine, ni lini italeta vifaa hivyo kwa wanafunzi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Walimu wa hesabu hata Kongwa hakuna. Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa

Spika, nakushukuru. Naomba nijibu mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Obama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna upungufu wa Walimu wa masomo ya sayansi na hisabati na kama nilivyoongea kwenye jibu langu la msingi ni kwamba sasa hivi tunafanya mchakato wa kumalizia kuajiri Walimu zaidi ya 4,500 na tumeyaweka mahsusi kabisa kwamba maeneo haya, Wilaya yako ya Kongwa, kule Buhigwe na maeneo mengine, tutazingatia maeneo ambayo yana upungufu mkubwa zaidi.

Tunaomba tupate taarifa kwa sababu kuna mahali unakuta kweli shule nzima haina hata Mwalimu wa hesabu, au baiolojia, kemia au fizikia, tutaweka vipaumbele maeneo hayo ambayo yana changamoto kubwa. Hii ni awamu ya kwanza ya ajira, awamu ya pili ikipatikana pia tutakuwa tunapeleka Walimu kadri uwezo utakavyokuwa unapatikana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anauliza habari ya kumalizia maboma ya maabara. Nimesema kwenye majibu yangu ya msingi ni kwamba tayari hapa tulipo tunasambaza vifaa, tenda imeshatangazwa, kazi inafanyika. Inawezekana wakati tunaomba taarifa kwenye halmashauri mbalimbali labda watu wetu kule hawakuleta taarifa hiyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Obama kama ana wasiwasi kwa hili la kupeleka vifaa vya maabara kwenye eneo lake, basi naomba tuwasiliane ili tuweze kuzingatia maombi yake. Ahsante.

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Shule zingine unakuta shule ya sekondari ina Mwalimu mmoja tu wa hesabu *form one* mpaka *form four* na vidato kadhaa ndani yake. Kwa hiyo yaani safari nyingine tuje tupate ajira ya Walimu wa hesabu tupu hata kama ni 3,000 au 4,000. *(Makofi)*

Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe.

Na. 113

**Hitaji la Barabara ya Mkato Kutoka Songwe kwenda Mbozi**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO** aliuliza:-

Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Songwe yapo Mbozi na hakuna barabara ya kuunganisha Wilaya mpya ya Songwe kufika mkoani hadi upitie Mbeya:-

Je, Serikali haioni haja ya kutengeneza barabara ya mkato toka Songwe kupitia Kata ya Magamba kwenda Mbozi Makao Makuu ya Mkoa ili kuwarahisishia usafiri wananchi wa Wilaya ya Songwe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaona haja ya kutengeneza barabara ya mkato kutoka Wilaya ya Songwe kwenda Wilaya ya Mbozi kupitia Kata ya Magamba. Barabara iliyopendekezwa inaitwa Galula – Itindi – Magamba yenye urefu wa kilometa 32.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imeshaanza kutengenezwa kupitia *TARURA* ambayo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 imetengwa shilingi milioni 65 kwa ajili ya kujenga daraja lenye urefu wa mita tisa katika Kijiji cha Itindi na mpaka sasa Mkandarasi anaendelea na kazi. Vilevile katika mwaka wa fedha 2019/2020, barabara hii imeombewa kiasi cha shilingi milioni 63 kwa ajili ya kufanya matengenezo sehemu korofi kwa urefu wa kilometa saba.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* Wilaya ya Songwe inaendelea kufanya usanifu wa kina ili kujua mahitaji na gharama halisi za kufanyia matengenezo makubwa. Mara kazi hiyo itakapokamilika Serikali itatafuta fedha kuhakikisha inajenga barabara hiyo na kufanya ipitike majira yote ya mwaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwalimu Mulugo, tafadhali swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii ninayoiombea ni ya kutoka Makao Makuu ya Wilaya kwenda mkoani, Wilaya ya Songwe ni mpya kabisa, kwa hiyo hatuna barabara inayounganisha wilaya na mkoa, kwa hiyo ningependa Serikali ifanye uharaka zaidi kwa sababu wale wananchi wanapitia Mbalizi ambako ni mbali sana. Kama itakuwa inatenga milioni 63 kila mwaka maana yake itachukua miaka sita kuja kupata hii barabara, nataka Serikali angalau iniongezee fedha kutoka milioni 63 mpaka milioni 300 ili tuweze kumaliza hii barabara kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Rais alipokuja Wilaya ya Songwe tulimwomba kilometa nne kwa ajili ya kufanya Mji wa Mkwajuni, Makao Makuu ya Wilaya yawe salama na yawe safi. Sasa ni lini Serikali itatupa fedha kwa ajili ya kilometa nne za lami pale Mji wa Mkwajuni?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mulugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa majibu kwenye majibu yangu ya msingi, yeye mwenyewe anakiri kwamba ameona nia ya Serikali ya kuhakikisha kwamba kwanza tunatambua kwamba tunataka tutumie kilometa 32

ili wananchi wasiendelee kuzunguka na tumeanza kujenga hayo madaraja. Katika majibu yangu ya msingi nimemhakikishia kwamba ni vizuri tukawa na tathmini kujua gharama halisi ili hata hicho kiasi cha fedha kinavyotafutwa tuwe tunajua tunatafuta kwa ajili ya kazi gani ambayo inatakiwa ifanyike. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuiamini Serikali tunatambua iko haja ya kuhakikisha kwamba wanafika Makao Makuu ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anasema iko ahadi ya kilometa kwa ajili ya lami ili na wao katika makao makuu ya wilaya wafanane na makao makuu ya wilaya zingine. Naomba nimhakikishie Mhesimiwa Mbunge; ahadi zote za Viongozi wa Kitaifa tunazitekeleza na kwa Mkoa wa Songwe tumeanzia Makao Makuu kwa maana ya Momba, tunaanza kuweka kilometa moja, lakini pia na Mbozi. Naomba hatua kwa hatua, hakika ahadi zote za Viongozi wa Kitaifa sisi tutakwenda kuzitekeleza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Sware atamulizia.

Na. 114

**Kodi Itokanayo na *VAT* Kwenye Taulo za Kike**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI (K.n.y. MHE. UPENDO F. PENEZA)** aliuliza:-

Je, katika mwaka 2016/2017 na 2017/2018 Serikali ilikusanya kiasi gani cha kodi ya 18% *(VAT)* kwa taulo za kike *(sanitary pads)* zote zilizotengenezwa nchini na zile zilizoingizwa nchini kabla ya kodi hiyo kuondolewa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilikusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya kiasi cha shilingi bilioni 3.01 na shilingi bilioni 2.54 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwenye bidhaa ya taulo za kike zilizoingizwa nchini pamoja na zile zilizozalishwa hapa nchini kabla ya kodi hii kuondolewa Juni, 2018.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Upendo Peneza bado ana maswali mawili ya nyongeza kutokana na majibu ya Serikali. Swali la kwanza, nauliza kwamba, japokuwa Serikali imeondoa baadhi ya kodi katika uzalishaji wa taulo za kike lakini bado bei ya taulo hizo iko juu sana. Sasa Serikali ina mkakati gani wa kusimamia bei hii kushuka ili kufikia wale walengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anauliza, sasa kama Serikali imeshindwa kusimamia kushuka kwa bei za hizi taulo japokuwa wameondoa baadhi ya kodi, je, haioni kwamba iendeleze tu kodi zile za awali lakini kodi hii ikusanywe na iwe *ringfenced* ili kuweza kununulia hizi taulo za kike na kuzigawa bure shuleni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na swali lake la pili ambapo amesema kama Serikali imeshindwa kusimamia kushuka kwa bei; naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania na Taifa letu kwa ujumla tupo katika soko huru kwa bidhaa zote, kwa hiyo sio kwamba Serikali imeshindwa kusimamia kushuka kwa bei, hapana, haijashindwa na ndiyo maana sasa hivi baada ya kuondoa kodi ile kwenye bidhaa hii Serikali imeendelea kupokea maoni mbalimbali ya wananchi wetu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuweka bidhaa hii kuwa *ringfenced* Serikali inaendelea kufanya tafiti mbalimbali, lakini kuna changamoto ya kusema kwamba kodi inayotozwa *specific* kwenye bidhaa hii iwekwe kwa ajili ya wanafunzi hawa kwa sababu yapo makundi mengine ambayo kodi zinatozwa kwenye bidhaa zinazotumika *specifically* na makundi kadhaa, kwa hiyo tutatengeneza ombwe la kila kundi kuja kuomba kodi inayotozwa kwenye makundi hayo waweze kupewa wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama nilivyosema inaendelea kufanya utafiti, tumekwenda nchini Afrika Kusini, Botswana na Kenya kujifunza nini wanafanya. Wenzetu waliondoa kodi hizi na wakagundua kwamba haiwezi kuleta matokeo chanya kama ambavyo yamekuwa ni majibu ya Serikali yetu ndani ya Bunge lako Tukufu. Kinachotakiwa kufanyika ni kubuni njia nyingine ya kuhakikisha watoto wetu wa kike wanapatiwa bidhaa hizi lakini bila kui-*attach* na kodi au tozo zozote zinazotozwa kwenye bidhaa hii kwa sababu tumejiridhisha kwamba unapoondoa kodi wanaonufaika ni wazalishaji kwa sababu tuko kwenye soko huria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kwamba ni mkakati gani kama Serikali tunaweka; nimesema sasa hivi tunaendelea kufanya tafiti mbalimbali ambapo tutakapojiridhisha na *options* ambazo zitaleta matokeo chanya kwa pande zote mbili watoto wetu wa kike na Serikali yetu, basi tutakuja na *option* hiyo ndani ya Bunge lako Tukufu ili tuweze kuwasaidia watoto wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware, unaona funzo hapo? Serikali peke yake kuondoa kodi wakati mwingine haisaidii, wafanyabiashara wanafaidika hapo katikati.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kwa niaba yake Mheshimiwa Ally Keissy.

Na. 115

**Huduma ya Mawasiliano – Mpanda Vijijini**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO)** aliuliza:-

Vijijini vya Kapanga, Katuma, Simbwesa, Kasekese, Kungwi na Kabage havina mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano ya simu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kapanga, Katuma Mpembe na Simbwesa vilipatiwa huduma ya mawasiliano mwaka 2016. Mradi huu ulitekelezwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya *Vodacom* kwa ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Vijiji vya Kasekese, Kungwa na Kabage vya Kata ya Sibwesa vilifikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia mradi wa *Halotel* wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji 4,000 nchini mwezi Septemba, 2018. Hata hivyo, baada ya kukamilika vifaa vya mawasiliano

vilivyofungwa vilipata tatizo la kiufundi na kupelekea wananchi wa vijiji hivyo kutopata huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya mawasiliano vilivyopata matatizo vimeshaagizwa na vinategemewa kuwasili hivi karibuni na vitafungwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2019 ili wananchi wapate huduma ya mawasiliano itakayowasaidia kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaridhisha lakini ahakikishe kweli, maana yake vijiji hivi vimekaa porini sana, havina mawasiliano, tena kwenye mbuga za wanyama mtu akijeruhiwa inakuwa taabu hata mawasiliano ya gari kuja kuwachukua.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la nyongeza; katika Kijiji cha Kizi ambapo kuna mkongo wa mawasiliano umejengwa na Serikali lakini kijiji hakina mawasiliano, je, Mheshimiwa Waziri, nimemfuata ofisini kwake zaidi ya mara kumi kuhusu Kijiji cha Kizi, vipi anaoneje hilo swali langu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali. Mbunge anapokuja ofisini kwako mara kumi, ya kumi na moja anaulizia Bungeni. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Keissy kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ametaka nimhakikishie kwamba eneo hilo ambalo limetajwa nitafikisha mawasiliano. Kama nilivyomhakikishia ni kwamba vifaa viko bandarini, sasa hivi tulikuwa tunafanya *clearance* kwa ajili

ya kuvipeleka sehemu husika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeleka hayo mawasiliano kabla ya mwisho wa mwezi wa Sita kama nilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Kijiji cha Kizi; tayari nimekwishatembelea kijiji hicho na tulikuwa na Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimpongeze kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya mawasiliano, katika majimbo mengi sana hapa nchini, jimbo lake lina asilimia 93 ya kupatikana kwa mawasiliano, nimhakikishie tu kwamba hicho kijiji chake kilichobakia tutakwenda tutashughulikia na tutakiingiza kwenye Mpango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli tutashukuru sana Mbunge baada ya kutembea mara kumi kuja ofisini, Mheshimiwa Ally Keissy au itabidi uongee *mother tongue* ndiyo Waziri aelewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa nilikuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake mazuri, yeye mwenyewe anajua kwamba minara ya Waheshimiwa Wabunge wengi haifanyi kazi ikiwemo mnara wa kwangu Kilolo na ameahidi mara nyingi kufika kuhakikisha kwamba minara inafanya kazi. Sasa je, atakuwa tayari kwenda kabla ya Bunge hili, kufika Kilolo na kuhakikisha kwamba mnara ule unafanya kazi?

**SPIKA:** Kabla ya Bunge hili hapana, sitampa kibali, baada ya Bunge hili labda. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niwe mkweli, Mheshimiwa Mwamoto amekuwa akifika mara nyingi sana ofisini kufuatilia

masuala ya minara kwenye jimbo lake. Ni kweli pia kuna minara kama mitatu, minne hivi ambayo haipeleki mawasiliano vizuri sehemu kubwa, nadhani ni kwa sababu ya watumiaji wengi sana, kwa hiyo, inakuwa na uhafifu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeleka timu ya wataalam waende wakaiongezee nguvu minara kwenye maeneo yake ili iweze kuwahudumia wananchi kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuendelee na swali la Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo kwenye Wizara hii hii.

Na. 116

**Ujenzi wa Barabara ya Makofia-Mlandizi-Vikumburu**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Ujenzi wa Barabara ya Makofia-Mlandizi-Vikumburu kwa lami ni ahadi ya Ilani ya CCM tangu mwaka 2010, na kwa sababu upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo umekamilika:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kwa swali hili, Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makofia-Mlandizi-Vikumburu ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia *TANROADS* Mkoa wa Pwani inayounganisha Wilaya za Bagamoyo, Kibaha na Kisarawe. Serikali imeanza mpango wa kuijenga barabara ya Makofia-Mlandizi-

Vikumburu kwa kuanza na hatua ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni na uthamini wa mali zitakazoathiriwa na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu ilikamilika Agosti, 2017 kwa kipande cha Makofia-Mlandizi na kipande cha Malandizi-Maneromango usanifu ulikamilika Novemba, 2018. Baada ya usanifu wa sehemu iliyobaki ya Maneromango-Vikumburu kukamilika na gharama ya barabara nzima kujulikana, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiedelea kutafuta fedha za ujenzi, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili kuendelea kupitika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya Sh.753,381,515 zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kutambua kwamba hii ni ahadi ya chama chetu ya muda mrefu tangu Ilani ya mwaka 2010, huu ni mwaka wa tisa na sasa usanifu umekamilika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni muafaka sasa kwa kipande kile cha Makofia hadi Mlandizi ambacho usanifu wake umekamilika kuanza taratibu za ujenzi mapema iwezekanavyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu hivi sasa usanifu umekamilika na wananchi hawa walikuwa wanasubiri fidia ya maeneo yao tangu kipindi ambapo barabara hii ilitangazwa kujengwa kwa maana ya takribani imefika miaka tisa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwalipa fidia wananchi hawa kutoka Makofia hadi Mlandizi mpaka

Vikumburu ili waweze kupisha ujenzi wa muundombinu huu muhimu kwa furaha?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwa sababu nafahamu amekuwa akifuatilia sana barabara nyingi za Mji wa Bagamoyo, ikiwemo barabara hii ya Makofia-Mlandizi lakini pamoja na barabara nyingine ambazo zinaunganisha Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, ni kweli kwamba barabara hizi alizozitaja, ukiichukua kutoka Bagamoyo - Mlandizi - Kisarawe ziko kilometa 100, lakini kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba kazi kubwa imeshafanyika na sasa tunakamilisha kufanya mapitio ya *compensation* (fidia) kwa wananchi ambao watapisha mradi huu. Kama ilivyo kanuni, tukishawalipa wananchi hawa sasa tutakuwa na haki ya kuanza kuenga kipande hiki cha barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu tu Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwamba kipande cha barabara hiyo kutoka Makofia mpaka Mlandizi kilometa 36.7 sasa tunakamilisha. Tathmini ya awali ilionyesha kama fidia ya shilingi bilioni 11 au 12, hivi sasa Mtathmini anafanya *review* ili tuweze kuwa na uhakika wa kiasi gani wananchi hawa wanastahili ili tuwalipe tuanze kujenga kipande hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba kwa sababu barabara hii inaunganisha vipande viwili, kile cha

kutoka Kisarawe - Mlandizi, kile kipande cha kutoka Kisarawe - Maneromango kama kilometa 10, hivi sasa ujenzi unaendelea. Kwa hiyo, niseme tu kwa ujumla wake kwa wananchi wa Bagamoyo na Pwani kwa ujumla kwamba barabara hii yote kwa ujumla wake ujenzi tumeshaanza na tukilipa fidia pia kipande cha kutoka Mlandizi - Bagamoyo tutaanza kukijenga ili wananchi waweze kunufaika na matokeo makubwa ya kazi nzuri ya Serikali yao.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nangurukuru-Liwale ni muhimu sana kwa wakazi wa Liwale, lakini siyo hivyo tu ni barabara iliyoahidiwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020. Je, Serikali inawaambia nini wana Liwale juu ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, barabara ya Nangurukuru - Kimambi - Liwale.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimpongeze tu Mheshimiwa Kuchauka kwa sababu namfahamu amekuwa akiifuatilia sana barabara hii, ni kilometa 230 kutoka Nagurukuru - Liwale. Niwahakikishie tu wananchi wa Liwale kwa ujumla wake, maana walikuwa wanajiona kama wako Kisiwani. Mheshimiwa Kuchauka anafahamu tunatoka Nachingwea, kilometa 129 kuja Liwale na tuko kwenye hatua ya usanifu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge asiharakishe tu shughuli, tutakuja na pendekezo kwenye bajeti yetu inayokuja kwa ajili ya kusanifu barabara hii ya kutoka Nangurukuru - Liwale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliombe tu Bunge lako tutakapokuja na pendekezo hilo watupitishie ili twende kusanifu barabara hii ya Mheshimiwa Mbunge Kuchauka na hatimaye tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Anna Joram Kidarya, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 117

**Mawasiliano ya Simu - Babati Vijijini**

**MHE. ANNA J. GIDARYA** aliuliza:-

Jimbo la Babati Vijijini linakabiliwa na changamoto ya muda mrefu ya huduma ya mawasiliano ya simu hasa katika Vijiji vya Yorotonik, Endagwe, Hoshan na Endakiso ambako hakuna kabisa mnara wa mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo katika maeneo ya vijiji husika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Eng. Atashasta Nditiye, Vijiji vya Yorotonik, Endagwe na kadhalika.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuratibu utekelezaji wa jitihada muhimu za kuwezesha maeneo yote nchini kufikiwa na huduma za mawasiliano sawasawa na maelekezo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016. Kupitia Mfuko wa Mawasiano kwa Wote Serikali itaviainisha

Vijiji vya Yorotonik, Endagwe, Hoshan na Endakiso kwa kuangalia ukubwa wa eneo, idadi ya wakazi wake pamoja na kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya ruzuku kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini kukamilika, vijiji hivyo vitajumuishwa katika orodha ya miradi itakayoingia katika zabuni zinazotarajiwa kuingizwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Gidarya, tafadhali, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tatizo lililoko Babati Vijijini ni tatizo pia lililoko Kiteto, Vijiji vya Makame, Ishkribo, Asamatwa, Ngaboro, ni lini sasa vijiji hivi vitaunganishwa pamoja na hivi Vijiji vya Endagwe, Hoshan, kwa ajili ya kufanya tathmini ili wananchi wapate huduma ya mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kijiji cha Landanai kilichoko Simanjiro na Kijiji cha Ngage, ni vijiji ambavyo vina idadi kubwa ya watu lakini mpaka sasa vijiji hivi havijafanyiwa uthamini kwa ajili ya kupata mawasiliano hayo. Ni lini sasa Serikali itapeleka huduma hii Landanai? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali, kwenye wilaya hizo jirani zote, Kiteto na kwingineko.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gidarya, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kiteto alivyovitaja, bahati nzuri vimekwishaletwa mezani kwangu na Mbunge wa Kiteto,

kupitia Chama cha Mapinduzi kwamba havina mawasiliano na tumekwishaviingiza kwenye orodha ya vijiji vitakavyopelekewa huduma ya mawasiliano na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshauri tu Mheshimiwa asiwe na wasiwasi vijiji alivyovitaja vitapepelekewa mawasiliano na vijiji vingine hivyo vyote alivyoviulizia Mheshimiwa Mbunge, tayari ninayo orodha yake nililetewa na Mbunge wa jimbo husika. Nimhakikishie tu Mheshimiwa tukitoka hapa tunaweza kuwasiliana ukaangalia orodha ya vijiji hivyo kuona kama vimeshaingizwa au la, kwa sababu nina hakika vyote vimeshaingizwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kabla sijauliza swali naomba nikutakie heri ya Pasaka kwa niaba ya Warombo wenzangu wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amenukuliwa katika vyombo vya habari akisema kwamba kuanzia tarehe 1 Mei, 2019 kutakuwa na usajili mpya wa laini zote kwa kutumia alama za vidole. Ameendelea zaidi kusema kwamba hakutakuwa na ruhusa ya kumiliki zaidi ya laini mbili mpaka ruhusa maalumu ya maandishi. Mheshimiwa Waziri anafahamu kuna maeneo mengine laini hazipatikani, kuna maeneo Vodacom ipo lakini Airtel haipo. Sasa mkifanya hivyo hamtaona kwamba mtawatesa wananchi ambao huduma za baadhi ya laini hazipatikani katika maeneo yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Watu wanajifichaficha, laini hii Bi. Mkubwa, laini hii nyingine nyumba ndogo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Atashasta Nditiye, laini moja tu bwana, majibu tafadhali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la usajili kuanzia tarehe 1 Mei, 2019. Ni kweli tumezielekeza kampuni za huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi kuanza sasa utekelezaji wa kusajili kwa kutumia alama za vidole na zoezi hilo litaanza kuanzia tarehe 1 Mei, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako tutaomba sasa Bunge lituruhusu tulete Madawati Maalumu ya watoa huduma ili Waheshimiwa Wabunge wafanye usajili wao wakiwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote kwamba hakuna sehemu ambako nilizungumza kwamba kila Mtanzania atakuwa na laini moja tu ya simu, hapana. Kilichozungumzwa na nilichokizungumza na walikuja kufafanua wenyewe baadaye ni kwamba tunatamani kila Mtanzania awe na laini moja ya simu kwa mtandao mmoja, akitaka laini nyingine, kwa sababu *possibility* ipo, mtu unaweza ukawa unatumia Tigo lakini ukataka *Ipad* yako itumie Vodacom, tunaruhusu, useme, lakini tunaepuka utitiri wa laini nyingi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenyewe ni mashahidi mnaombwa fedha kila siku, tuma kwa namba hii, tuma kwa namba hii, hizo ni laini ambazo hazina tija na zinatuumiza sana Watanzania. Tulizungumza kwamba mtu awe na laini moja kwa mtandao mmoja, Vodacom moja, Tigo moja, Airtel moja na kadhalika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani, bado kuna swali la nyongeza hapohapo, laini moja kwa mtandao mmoja, aah, kama kuna swali la nyongeza simameni nitawapa nafasi lakini ni kwa hili. Ndiyo Mheshimiwa Kikwete nimekuona, tafadhali.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, naomba nirejee katika swali la msingi, siko katika mambo ya laini ya Mheshimiwa Selasini.

**SPIKA:** Uliza, uliza.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo Babati Vijijini yanafanana moja kwa moja na yaliyopo katika Halmashauri ya Chalize. Nimemwandikia sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake lakini utekelezaji umekuwa ni wa taratibu sana. Sasa kwa kuwa jambo hili nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri, naomba anijibu wamefikia wapi juu ya matatizo ya mawasiliano katika Kata ya Kiwangwa, Msata na Lugoba kama ambavyo tumeelekezana? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Majibu ya wananchi wa Chalinze, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Vijiji vya Kiwangwa katika baadhi ya maeneo yana tatizo la huduma ya mawasiliano lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo lake analolitaja la Kiwangwa linahitaji kuongezewa nguvu kwenye mnara wa mawasiliano ulioko pale. Kwa hiyo, namshauri aje tuonane baadaye tuangalie vijiji vingine ambavyo tumeviingiza kwenye mpango wa kupelekewa huduma na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee sasa na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mheshimiwa Ally Saleh Ally.

Na. 118

**Chuo cha Diplomasia Tanzania**

**MHE. ALLY SALEH ALLY** aliuliza:-

Chuo cha Diplomasia kimekuwa na umuhimu mkubwa katika masuala ya kidiplomasia na uwakilishi wa Tanzania nje ya nchi.

(a) Je, Chuo cha Diplomasia kimetoa wahitimu wangapi na mgawanyiko wake ukoje hadi sasa?

(b) Je, wahitimu wangapi hadi sasa wamepanda na kuwa *Career Diplomats?*

(c) Diplomasia inaenda sambamba na mawasiliano, je, Serikali haijafikiria kuongeza lugha zinazofundishwa chuoni hapo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali namba 118 kutoka kwa Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Chuo cha Diplomasia mwaka 1978 hadi hivi sasa, chuo kimetoa jumla ya wahitimu 3,421, kati ya hao, wahitimu katika ngazi za Shahada ni 72, Stashahada ya Udhamili katika Menejementi ya Uhusiano wa Kimataifa ni 503, Stashahada ya Udhamili katika Diplomasi ya Uchumi ni 341, Shahada ya kawaida ni 2,084, ngazi ya Cheti ni 347 na wahitimu 74 ni wa Mafunzo Maalumu ya Maafisa Waandamizi wa Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, katika idadi hiyo ya wahitimu wa Chuo cha Diplomasia, wanawake ni 1,060 na wanaume ni 2,361. Wanafunzi hao walitoka nchi za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Botswana, Burundi, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Guinea, Kenya, Komoro, Libya, Malawi, Msumbiji, Namibia, Palestina, Rwanda, Sudan, Zambia, Zimbabwe pamoja na hapa kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa chuo hiki mwaka 1978, zaidi ya wahitimu 500 kutoka Tanzania wameweza kuwa *Career Diplomats* na kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, chuo kinatambua umuhimu wa lugha katika nyanja za masuala ya mahusiano ya kimataifa na diplomasia. Chuo kimeongeza idadi ya lugha za kigeni zinazofundishwa, mpaka hivi sasa chuo kinafundisha lugha saba (7) ambazo ni Kiarabu, Kichina, Kifaransa, Kihispania, Kingereza, Kikorea na Kireno. Halikadhalika, chuo kimetayarisha mtaala wa kufundishia lugha ya Kiswahili kwa wananfunzi wa kigeni ili kueneza lugha hiyo kimataifa. Mafunzo hayo yataanza kutolewa kuanzia mwaka wa masomo 2019/2020. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Malindi.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika siku chache ambazo nimeridhika la jibu la Serikali, *this is a very good answer from the Government*. Kuna takwimu za kutosha, kuna maelezo ya kutosha. Hivi ndivyo ambavyo ningetarajia majibu ya Mawaziri wengine yawe kama haya. Nina maswali mawili ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo chetu ni cha miaka mingi hivi sasa na kama uzoefu, basi upo wa kutosha: Je, Mheshimiwa Waziri katika muongo ujao, miaka kumi ijayo, anakionaje chuo chetu? Kitakuwa kimefikia hadhi na kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kada ya wana-diplomasia ni muhimu sana, kuna ambao tunaamini kwamba chuo hiki kinapaswa kuwa ndiyo alama ya Tanzania maana *Career Diplomacy* na hata *Political Diplomacy* wote wanapita hapa ili kwenda ku-*shape* sera na mitizamo na namna ya kuilinda na kuitetea Tanzania.

Je, kwa kiasi gani chuo hiki kinaweza kutumika kuwa ni *think tank* ya kujenga sera na mikakati ya kidiplomasia ili

kwenda kuitetea nje kwenye ushindani na ukinzani wa Kidiplomasia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya nje, Mheshimiwa Dkt. Damas Danieli Ndumbaro, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Ally Saleh kwa pongezi alizozitoa kwa jibu ambalo tumelitoa. Pili, nichukue fursa hii kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza aliuliza: Je, tunakionaje chuo kwa miaka kumi ijayo? Naomba tumweleze Mheshimiwa Ally Saleh, Mbunge wa Malindi pamoja na Watanzania wote kwamba Chuo chetu cha Diplomasia ni chuo ambacho kinaheshimika sana Barani Afrika. Umeona idadi ya nchi ambazo zimeleta wanafunzi hapa na zinaendelea kuleta wanafunzi hapa, hiyo ni ishara tosha kwamba heshima ya chuo hiki ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Wizara ni kukifanya Chuo hiki sasa kivuke mipaka kwenda nje ya mipaka. Tuna makubaliano ya awali na ndugu zetu wa Argentina waweze kukitumia chuo hiki kupata elimu ya Diplomasia. Hiyo ni ishara kwamba tunavyokwenda miaka kumi ijayo, yajayo yanafurahisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili aliuliza; je, Chuo kinaweza kuwa kama *think tank?* Hivi sasa kada ya Diplomasia inakuwa vizuri, tumepata wataalam wengi na sisi kama Serikali tunaendelea kuimarisha hiki chuo kwa kuweza kusomesha waatalam wengi zaidi na kuleta wengine kutoja nje kwa kupitia nyanja za ushirikiano ili kukifanya chuo hiki kiendelee kuheshimika na kitoe waatalam wengi watakaosaidia Tanzania katika Diplomasia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Madini, swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, tafadhali.

Na. 119

**Utafiti wa Madini - Jimbo la Morogoro Kusini**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya utafiti wa uhakika katika Vijiji vyote vya Jimbo la Morogoro Kusini ili kubaini madini yaliyopo?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje Wachimbaji wadogo wa Rubi, Spinel na Dhahabu ili waweze kuzalisha zaidi na kupata masoko ya uhakika?

(c) Je, ni lini Serikali itatuma Wataalam wa kuthibitisha wingi wa madini ya *Graphite* na Chokaa katika maeneo ya Jimbo la Morogoro Kusini ili mipango ya kuchimba iweze kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini *(GST)* ilifanya utafiti wa awali wa kijiolojia katika Jimbo la Morogoro Kusini na kutengeneza ramani ya kijiolojia *(Quarter Degree Sheet – QDS)* zipatazo tisa.

Mheshimiwa Spika, taasisi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwemo kampuni ya *Beak Consultants* ya Ujerumani na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kati ya mwaka 2013 na 2014 walifanya utafiti wa awali na kubainisha uwepo

wa madini ya dhahabu katika Kata za Mkuyuni, Mikese, Mazimbu, Kisemu na Tununguo; vilevile madini ya chokaa katika Kata ya Mkuyuni na Kisaki; madini ya Kinywe *(graphite)* katika Kata za Mvuha, Mkuyuni, Kisemu na Mtombozi.

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti huo ulibainisha pia uwepo wa madini ya *ruby* katika Kata za Tawa, Mkuyuni na Mkambalani. Vilevile kuna madini ya *spinel* na *barite* katika Kata za Mkuyuni.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP)* imenunua mtambo wa kuchoronga miamba mipya na kuikabidhi katika Shirika la *(STAMICO)* kwa lengo la kufanya utafiti katika maeneo ya wachimbaji wadogo kwa gharama nafuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Kusini.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana ya swali hili; na kwa kweli ni majibu sahihi. Napenda tu niulize maswali madogo ya nyongeza. *(Makofi)*

Swali la kwanza, yapo maeneo ambayo hayakutajwa hapa ambayo ni Dutumi Bwakila Chini, wana dhahabu na *ruby*; Konde wana dhahabu na *gemstone,* hiyo *spinels*; pia Singisa wana *ruby* ya kutosha. Sasa swali langu la msingi kwa maana ya yale yaliyojibiwa yajumuishwe na maeneo haya mapya ili sasa tuweze kupata uhalisi wa sehemu ambazo madini haya yanapatikana. Hili ni ombi tu.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, Serikali ina utaratibu gani kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo kifedha pamoja na vifaa kwa ajili ya kuboresha uchimbaji wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo hayajatajwa. Maeneo ambayo tumeyataja ni yale maeneo ambayo tumeona ni *potential* kwa uchimbaji. Vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote ya Morogoro tunayafahamu na tumetengeneza ile *Quarter Degree Sheet* ambayo inaonesha ramani zote za uwepo wa madini.

Mheshimiwa Spika, vile vile uwepo wa madini ni kitu kimoja, lakini madini yanayolipa *automatically* tu utaona kwamba wachimbaji wanaelekea katika maeneo yale. Ni kama vile inzi anavyofuata kidonda; wachimbaji wakishaona kuna *potential* maeneo ya uchimbaji, wenyewe unaona wameshasogea pale.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambaji ule mkubwa inabidi utafiti wa kina ufanyike na pawe na ile hali ya kuonesha kwamba kuna madini ya kutosha na hata uwekezaji mkubwa unaweza ukawekezwa pale. Kwa wachimbaji wadogo wana uwezo wa kusogea na tuko tayari kuwasaidia kuendelea kuwapa taarifa za kijiolojia.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema kuhusiana na kuwawezesha wachimbaji wadogo; Wizara imekuwa bado inasaidia kuwawezesha wachimbaji wadogo. Hapo nyumba tulikuwa katika huo mradi wa *SMMRP,* tulikuwa tunatoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo, lakini ruzuku hiyo ilikuwa inatumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tumesimamisha utoaji wa ruzuku hiyo, sasa tunaangalia namna bora ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ambapo tukiwapa fedha zile, basi waweze kununua vifaa, wafanye tafiti mbalimbali na kuwawezesha kuchimba. hapo awali, walikuwa wanapewa hata wasiyokuwa na sifa, na kweli mpaka sasa tunafuatilia na kuhakikisha kwamba tunakwenda kuwasaidia wachimbaji wadogo tunapokuja na *modality* nzuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar Mbunge wa Nyang'hwale, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kuna tatizo kubwa upande wa watumishi wa Madini na *TMA*. Kumekuwa na ucheleweshwaji sana wa ushushaji wa mashine upande wa *elution* na kusababisha hasara kwa wenye *elution* na pia kwa wachimbaji:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuongeza watumishi upande wa *TMA* na Madini ili ushushaji wa mashine zile za *elution* iwe wa kila siku ili kupunguza zile hasara wanazozipata watu wenye *elution*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Nyongo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna tatizo kidogo kwa wafanyakazi ambao wapo katika Tume ya Madini. Kwa sababu baada ya mabadiliko ya Sheria *TMA* ilikufa, imeanzishwa Tume ya Madini. Kwa hiyo, sasa hivi wafanyakazi wote, walioko Mikoani wako chini ya Tume ya Madini. Tuna tatizo kidogo kwa wafanyakazi, lakini sasa hivi tuna kwenda kuongeza wafanyakazi wengi zaidi ili waweze kutoa huduma kwenye zile *elution*.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kusisitiza, watu wote wenye *elution* tumeona kuna matatizo makubwa sana yanayofanyika, watu wengine wanaenda kule wanafanya mambo ambayo hayaeleweki. Tunaendelea kudhibiti na tunaendelea kutoa tamko kwamba wanapo-*load carbon* kushusha dhahabu wasijaribu kushusha bila uwepo wa wafanyakazi wa Tume ya Madini. Tunakwenda kuongeza, lakini sasa hivi tunajitahidi kuhakikisha kwamba kila siku waendelee kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, tunaendelea kurekebisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve. Mheshimiwa Rose.

Na. 120

**Vituo Maalum vya Ukaguzi wa Magari Barabarani**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza:-

Imekuwa ni kawaida sasa kwa Askari wa Usalama barabarani kusimamisha magari ya usafiri wa Umma kama vile daladala na mabasi na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu wa kuwa na Vituo Maalum vya Ukaguzi huo ili kuokoa muda wa wasafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabani, Sura ya 168 iliyorejewa mwaka 2002 Kifungu cha 81, kinampa uwezo Askari Polisi wa kulisimamisha gari lolote barabarani au sehemu yoyote anapolitilia shaka na kulikagua au pindi linapokuwa limetenda kosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani limeshaandaa utaratibu wa kuwa na vituo maalum vya ukaguzi wa mabasi ya Umma katika vituo vikuu vya mabasi vyote katika kila Mkoa ambapo mabasi ya abiria hufanyiwa ukaguzi kabla ya kuanza safari na pale yanapofika mwishoni wa safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ukaguzi wa pembezoni mwa barabara *(road side inspection*) ambao huhusisha mabasi ya daladala na vyombo vingine vya moto hufanyika katika vituo vya ukaguzi maalum *(check points)* ambavyo

vipo katika barabara kuu na katika barabara nyingine za Miji pamoja na Majiji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nakubaliana kabisa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuwa pale Polisi anapokuta kuna umuhimu wa kusimamisha gari ambalo limevunja sheria ni muhimu wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa tumekuwa na hivi vituo maalum vya ukaguzi, sasa hivi kumekuwa na changamoto kubwa hasa kwenye mabasi ya daladala. Kumekuwa na *unnecessary stop* na kusababisha ucheleweshaji wa wananchi kwenda kufanya shughuli zao. Nitakupa mfano, unakuta daladala imesimamishwa na *Traffic* yuko pembeni ana-*argue* na Konda kwa nini hana *proper uniforms?* Haya ilibidi yafanywe kabla huyu abiria hajaingia kwenye gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, nilitaka kujua sasa kama Serikali na Jeshi la Polisi tumejipanga vipi kuhakikisha sasa tunakuwa na hii *mandatory car inspection* tofauti na utoaji wa stika wa sasa ukizingatia hizi stika zimekuwa zinatolewa kwenye magari yasiyo na viwango na kusababisha ajali kubwa za barabarani. Nakushuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa maswali hayo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni, Tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri sana na ya msingi. Baada ya pongezi hizo sasa nitoe majibu ya maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mbali ya sheria ambayo nimeinukuu inayotoa mamlaka kwa Askari kusimamisha gari

popote anapoitilia hitilafu, ambapo madhumuni ya sheria ile kimsingi inatokana na baadhi ya madereva wetu nchini ambao wamekuwa wakikiuka Sheria za Barabarani mara kwa mara, kwa mfano, utakuta mtu anaendesha gari kwa *speed*. Kwa hiyo, Askari akiona utaratibu wa uendeshaji kama huo, lazima achukue hatua.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe wito kwa wananchi hasa madereva kutii Sheria za Barabarani ili kuepusha usumbufu. Pili, nataka nichukue fursa hii pia kutoa wito kwa Askari wetu wa usalama barabarani nchi nzima ambao kama wapo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge najua atakuwa ame-*experience* hiyo, kama wapo ambao wanafanya utaratibu wa kusimamisha magari kiholela kwa kujifichia chini ya mwamvuli wa sheria hii bila kuwa na makosa yoyote, basi waache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kuwa na utaratibu wa ukaguzi wa lazima, nataka nimwelezee Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali tumeshalitafakari kwa kina suala hilo na tunatambua kuwa na utaratibu wa ukaguzi wa lazima ni jambo ambalo ni muhimu na haliepukiki katika karne hii tuliyokuwa nayo, siyo tu kwamba litasaidia kutoa fursa kwa magari yetu kukaguliwa vizuri zaidi na hivyo kuwa na magari salama barabarani, lakini itasaidia kuiongezea mapato Serikali na hususani Jeshi la Polisi katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo tunazikabili. Kwa hiyo, kwa kutambua hilo tumekuja na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunatamani kwamba katika mabadiliko ya sheria ambayo itakuja, utaratibu huo utakuwa unasimamiwa na baraza jipya la usalama barabarani ambalo tunatarajia lije na muundo mwingine. Kwa hiyo, ni Baraza Tendaji, lakini hata kama matamanio yetu hayo bado hayajafikiwa au yatakuwa yamechelewa kufikiwa, tumeshatoa maelekezo kwa Shirika la Jeshi la Polisi *(Police Cooperation Soul)* kuanza mchakato wa kuanzisha utaratibu huo wa ukaguzi lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue fursa hii vilevile kuwaelekeza Jeshi la Polisi kupitia Shirika hilo la Maendeleo kuharakisha huo mchakato ili uweze kuanza mapema ikiwezekana hata kabla ya Awamu hii ya Kwanza ya utawala wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli haijamaliza muda wake.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa vituo hivi vya ukaguzi wa magari barabarani siyo tu muhimu kwa wananchi vilevile ni muhimu sana kwa Askari wetu. Tunatambua kazi kubwa wanayofanya Askari wa Barabarani, lakini Askari hawa mara nyingi wanapopata ajali kulipwa haki zao inachukua muda mrefu. Kwa mfano tu, katika Mkoa wangu wa Arusha kuna Askari wengi waliopata ajali wakiwa kazini, lakini mpaka sasa hivi hawajalipwa stahiki zao.

Je, ni lini Serikali italipa maaskari ambao wamepata ajali kazini haki yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali. Utawakumbuka lini Maafande wetu hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nikiri kwamba kulikuwa na changamoto za baadhi ya malipo ya stahiki mbalimbali za Askari wetu nchi nzima ikiwemo hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameizungumza, lakini lazima nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano, lazima tujipongeze kwa pale ambapo tutafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya malimbikizo haya yameanza kulipwa na tunaamini kwamba kama kutakuwa kuna maeneo ambayo bado hayajakamilika, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezungumza, hii fidia

ya Askari ambao wanapata ajali barabarani, basi tutakamilisha pale michakato mingine ikiwemo uhakiki pamoja na bajeti itakapokaa sawa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama ana maombi mahususi ya Askari ambayo anafahamu, basi aweze kutupatia ili tufuatilie tujue ni tatizo gani lililosababisha mpaka leo wawe hawajapatiwa stahiki zao?

**SPIKA:** Tumalizie basi Mheshimiwa Masoud na Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na mabadiliko ya Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani ambayo inatarajiwa kuletwa hapa Bungeni, kuna malalamiko kwa madereva mbalimbali kwamba kosa lolote linapotokea, basi hakuna onyo, hakuna karipio. Karipio kubwa ni shilingi 30,000/= kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonekana kwamba Polisi kwa wakati huu wanakusanya zaidi fedha kwa njia ya mapato zaidi kuliko kutoa karipio au kutoa onyo. *PGO* inaelekeza nini pale ambapo dereva amefanya kosa dogo la kwanza juu ya tatizo hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi Naibu Waziri tafadhali, Mheshimiwa Eng. Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni imani yetu na imani ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote waliomo humu ndani kwamba mtu yeyote ambaye amechukua chombo cha usafiri na kuingia barabarani, maana yake kwanza amepata mafunzo ya kutosha na ana leseni.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni moja, lakini la pili nina hakika Mheshimiwa Masoud anatambua kwamba tumekuwa

tukifanya kazi kubwa sana ya kutoa elimu kuhusiana na usalama barabarani kwa kutumia njia mbalimbali ili kuwakumbusha wale madereva ambao wamekuwa wakighafirika katika kufuata Sheria za Usalama Barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kuzingatia hayo mawili ni imani yetu kwamba mtu yoyote ambaye yuko barabarani anaendesha gari, anatambua wajibu wake na hivyo basi, sidhani kama ni jukumu la Jeshi la Polisi kuanza sasa kutoa elimu barabarani wakati mtu anahatarisha uhai wa raia wengine. Kwa hiyo, niendelee kusisitiza kwamba, ni vizuri kila mmoja ambaye anaendesha gari barabarani ajue kwamba kuna sheria na afuate sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba wale ambao hawafuati sheria basi wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ikiwemo kutozwa faini. Hata hivyo, kuna baadhi ya changamoto ambazo tumekuwa tukizizungumza kila siku zinahitaji busara katika kuzikabili na niendelee kutoa wito kwa Askari Polisi kuzingatia busara wakati mwingine pale ambapo kuna matatizo ambayo yanaweza kuepukwa. Kwa mfano, kama ambavyo hata Mheshimiwa Waziri amekuwa akizungumza mara zote, unakamatwa mtu kwa kosa moja linazalisha makosa mengi, mtu anashtakiwa kwa makosa zaidi ya matano au sita. Kwa hiyo, mambo kama haya na mambo mengine ambayo yamekuwa kero kwa wananchi, hayo tumekuwa tukitoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi litumie busara katika kuyakabili. Hata hivyo, tunataka kusisitiza umuhimu wa kutii sheria bila shuruti ili kuepusha ajali na kuokoa maisha ya Watanzania ambao wamekuwa wakipoteza maisha yao na kupoteza vyombo vyao kila siku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, swali la mwisho.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwenye barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro tumeona sasa hivi wamefunga *cameras*. Sasa kwa nini camera zile zisifungwe nchi nzima ili sasa baada ya kufungwa zile *camera* Askari wanaokaa barabarani warudi vituoni,

waende wakashughulike na masuala mengine ya wahalifu, kwa sababu msingi wao wa kukaa barabarani mkubwa ni *speed.* Sasa kwa kuwa zinafungwa *camera* ambazo zitakuwa zinachukua picha, zinatuma *report* kwenye *database, wherever* halafu zile *report* zinafuatiliwa hata baada ya wiki mbili, mwezi mmoja mtu anapelekea tiketi kwa mujibu wa *details* za gari lake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi, umejibu maswali mengi Mambo ya Ndani na inagusa watu wengi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMB0 YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo mwelekeo wa Serikali yetu. Ni imani yetu kwamba, mambo yatakapokuwa yamekaa vizuri kibajeti tutafunga *camera* katika Miji mikuu yote na maeneo mengine nchi nzima. Kwa hiyo ni suala tu la kuvuta subira na kazi hiyo itafanyika hatua kwa hatua kadri ya hali ya fedha itakapokuwa inaruhusu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo la Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba.

Na. 121

**Uzalishaji wa MW 5000 za Umeme Ifikapo 2020**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kufikia uzalishaji wa zaidi ya *megawatts* 5,000 za umeme ifikapo 2020.

Je, ni mkakati gani umewekwa ili kufikia lengo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Tanzania inajenga uchumi wa viwanda, Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 imeweka mipango ya kuzalisha umeme wa kutosha na unaotabirika. Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeweka mpango wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 5000 ifikapo mwaka 2020. Kufutia mpango huo, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo maji, gesi asilia na jua. Miongoni mwa miradi ya kuzalisha umeme inayotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia Kinyerezi *I* kutoka *megawatts* 150 za sasa na kufikia *megawatts* 335. Utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2019.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kufua umeme kwa gesi asilia ni Kinyerezi II, *megawatts* 240 ambao utekelezaji wake umekamilika mwezi Aprili, 2018, badala ya 2019 inayosomeka hapo na mradi wa kuzalisha umeme wa Mtwara wa *megawatts* 300 unaotekelezwa chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan *(JICA).* Mradi huu unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, mwezi Disemba, 2018, Serikali ilianza kutekeleza mradi za kuzalisha umeme wa kutumia nguvu ya maji *(Stiegler's Gorge) megawatts* 2,115 pamoja na mradi wa Rusumo, *megawatts* 80. Miradi mingine itakayoanza kutekelezwa hivi karibuni ni mradi wa Ruhudji, *megawatts* 358, mradi wa Rumakali, *megawatts* 222 na mradi wa Kakono, *megawatts* 87. Miradi hii inatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itatekeleza miradi ya kuzalisha umeme wa nguvu za jua *megawatts* 150 (Kishapu),

upepo *megawatts* 100 (Singida) na miradi ya Makaa ya Mawe *megawatts* 600.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hii itaongeza umeme katika gridi ya Taifa kutoka *megawatts* 1602 kutoka kwenye vyanzo vilivyotumika kuzalisha umeme kwa sasa na kufikia *megawatts* 10,000 ifikapo 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na natambua jitihada kubwa sana zinazofanywa na Serikali katika kuongeza uzalishaji wa umeme lakini nina swali moja tu la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha na kuwezesha kisera uwekezaji wa miradi midogo midogo ya uzalishaji wa umeme hususan katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya Taifa kama vile Mkoa wa Kigoma?

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Hapana, Mheshimiwa Waziri wa Nishati mwenyewe, Mheshimiwa Kalemani.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika swali la msingi la Mheshimiwa Katimba. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia wazalishaji wadogo wadogo katika nishati kwa upande wa maeneo ambayo hayana gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama ambavyo tumeeleza katika jibu la msingi, pamoja na kuzalisha umeme mkubwa katika maeneo mbalimbali yenye gridi ya Taifa, bado Serikali inahamaisha sana uzalishaji wa umeme mdogo mdogo katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya Taifa. Katika maeneo ya Kigoma mathalani; wazalishaji wadogo wameshajitokeza, Kampuni ya *Nexgen Solar White* imeanza kuzalisha *megawatts* tano ambazo sasa wanafanya

majadiliano na Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* kuingiza kwenye gridi ya Taifa. Kwa hiyo ni matumaini yetu maeneo mbalimbali ya Ujiji ambayo yameshafanyiwa utafiti kwenda mpaka Kaliua kuja mpaka Mkoa wa Tabora wazalishaji wataongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza maelezo ya upana zaidi kwenye suala la nyongeza la Mheshimiwa Katimba ni kwamba katika maeneo ya Mkoa wa Kigoma na Uvinza ambayo hayajapitiwa na umeme wa gridi ya Taifa, hivi sasa Serikali imeanza kujenga njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa gridi ya Taifa ili Mikoa ya Kigoma na Katavi nayo ifikiwe na gridi ya Taifa. Sasa hivi ujenzi unaanzia Tabora kupitia Jionee Mwenyewe-Juhudi-Nguruka mpaka Kidawe Mchini-Kigoma, kwa hiyo, hata wazalishaji wadogo wa umeme mdogo mdogo nao wataingizwa kwenye gridi ya Taifa.

**SPIKA:** Muda Waheshimiwa Wabunge hauko upande wetu. Sasa niendelee na matangazo. Nianze kuwatambulisha wageni wetu:-

Kwanza ni wageni wangu walio katika jukwaa la Spika akiwa ni Ndugu Methusela Gwajima ambaye ni Mwanasheria na Kada wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Gwajima karibu sana. Huyu ni Gwajima *junior* huyu. Ameambatana na watoto wake ambao ni wanangu pia, Evelyne Gwajima, Mery Gwajima na Victoria Gwajima. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni:-

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wa Kilimo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake, Ndugu Medson Sanga. Karibu sana Medson yuko kule, karibu sana sana sana. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Magreth Sitta ambao ni Walimu wakiongozwa na Afisa Elimu Msingi Wilaya ya Urambo, Mwalimu Gladys Lumato. Walimu-Urambo karibuni

sana sana sana. Karibuni Wanyamwezi ninyi, karibuni Dodoma, ahsante sana. Mmeleta Matobholwa? *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanakwaya wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Ndumanisa Pallangyo. Wanakwaya karibuni sana sana, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 45 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Kwaya Kuu ya Ushirika wa Arusha *road* wakiongozwa na Mchungaji Aggrey Ngwale. Kwaya kuu Arusha *road* karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Kanali Mastaafu, Masoud Ali Khamis ambao ni familia yake kutoka Mjini Unguja wakiongozwa na mke wake Ndugu Zuhura Saleh Amour. Karibuni sana wageni wetu kutoka Zanzibar, wale pale. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Rashid Sangazi ambao ni familia yake kutoka Mlalo, Mkoani Tanga wakiongozwa na mke wake Zaina Rashid. Bi Zaina yuko wapi hapo? Ahsante sana. Jamani shemeji yetu huyo kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi, lakini wako pia watoto wake; Baraka, Saida na Rashid Shangazi. Ahsante sana, karibuni sana familia ya Mheshimiwa Shangazi. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi 20 na Walimu 15 kutoka Liwale Mkoani Lindi wakiongozwa na Mwalimu Sadamu Malombe. Karibuni sana sana sana. Hili ndiyo kundi ambalo limetoka mbali kweli kweli. Karibuni sana kutoka Liwale kule sijui ni Kijiji gani hiki au ni pale pale Liwale Mjini na Ngano sijui au Makwenjiganga au Mtawatawa au Mpigamiti. Hayo ni majina ya vijiji vya Liwale hayo. *(Kicheko/Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ally Hassan King ambae ni Mtunzi wa filamu ya *Festula*, Ndugu Salim Saleh. Yule kule, karibu sana Salim Saleh. *(Makofi)*

Wageni 130 wa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ambao ni wasanii kutoka Shirikisho la Filamu Tanzania wakiongzwa na Mwenyekiti wa Shirikisho hili, Ndugu Simon Mwakifwamba. Karibuni sana sana sana. Leo Shirikisho la Filamu mmefunga kazi. Mheshimiwa Mwakyembe unaona timu ya filamu huko? Ahsante sana na karibuni sana, karibuni wapendwa. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni watoto wake, watoto wa Esther Matiko saba wakiongozwa na mdogo wake Ndugu Florence Matiko. Hapana ni familia yake jamani Waheshimiwa, karibuni sana, karibuni sana sana. Esther huyu inaelekea amejaaliwa huyu. *(Makofi/Kicheko)*

Mwenyekiti wa ibada, *Chapel* ya Bunge, Anna Lupembe anawaomba waumini saa 7.00 Mchana, Msekwa na mtoaji neno wetu atakuwa Mpaka Mafuta wa Bwana, Mchungaji Pallangyo wa *Arusha road,* natumaini na kwaya itakuwepo kutumbuiza kwenye ibada ya saa 7.00 na hii kwaya mnaijua mambo yake. Ni vizuri kwenda kuona na kusikia neno la Bwana kule kwa wale ambao ni waumini wa upande huo.

Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 26, siku ya Muungano, Ijumaa wiki hii kutakuwa na mechi kati ya Bunge na Baraza la Wawakilishi na Baraza la Wawakilishi wamesema wanakuja kisawasawa na wanakuja wengi. Kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa Dodoma saa 9.00 alasiri uwanja wa Jamhuri tujae pale, tuwe pamoja na wenzetu wa Baraaza la Wawakilishi, tuwafundishe mpira. Kutakuwa na mpira wa miguu na mpira wa pete na wamepania kweli kweli wamesema wanataka kuja kuwaonyesheni kwamba Baraza la Wawakilishi siyo masihara. Pia mfike kwa wingi kwa sababu nami nitakuwepo na Spika wa Baraza la Wawakilishi atakuwepo, sasa mikiniacha niwe peke yangu Waheshimiwa sitaweza kushangilia peke yangu. Kwa hiyo tuwashangilie, wachezaji wetu Ijumaa tarehe 26, saa 9.00 alasiri.

Tarehe 28, Jumapili kutakuwa na mechi kati ya Bunge *Sports Club* kwa maana ya timu ya *Netball* na *Football* na *UDOM* na mechi hizi zitachezwa katika viwanja vya UDOM. Pia ni vizuri jioni tunakwenda katika mambo kama haya kuburudika kidogo kuangalia nini kinaendelea, kubadilisha mawazo. Wakati mwingine Dodoma inakuwa kidogo *docile,* kwa hiyo ni vizuri kujichanganya kidogo.

Matangazo yameishia hapo, tunataka tuendelee sasa *unless* kuna neno. Kwa sababu hakuna, Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, tunaanza na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaji Juma Nkamia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Nataka kuchangia sana kwenye uhuru wa vyombo vya habari; najua kabisa kwamba katika Taifa hili sasa hivi kutoa habari imekuwa ni jambo hatari sana kuliko hata ugaidi.

Mheshimiwa Spika, nizungumze tu ukweli kwamba wako vijana wetu wengi sana ambao wamepata shida kubwa wamepigwa, wamewekwa mahabusu, wameteswa, wamekaa rumande zaidi ya miezi mine na bila kupelekwa Mahakamani na baada ya kupelekwa Mahakamani wameshinda kesi zao zote, lakini bado wana maumivu na vilema wamebaki navyo. Natoa mfano, kwa mfano, kijana mmoja anaitwa Mdude Nyagali ambaye yeye alikuwa anakosa kwenye mitandao, anakosoa utendaji wa

Mheshimiwa Rais na kutoa maoni yake, huyu mtu alikamatwa usiku, alipigwa, alisafirishwa kutoka Mbozi mpaka kwenda Dar es Salaam na alikaa Dar es Salaam zaidi ya miezi miwili huku akiwa amepigwa, amevunjwa miguu yake na akiwa hoi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia wako vijana wengi sana ambao wamekamatwa na vijana hawa mpaka sasa hivi wengine hawajapelekwa Mahakamani, lakini mpaka sasa hivi bado wanaendelea kukamatwa. Tunaomba sana wakati Waziri anakuja kuzungumza hapa, aje atuambie ni vijana wangapi ambao wamekamatwa katika Taifa hili kwa sababu ya makosa ya kimtandao wakati wanatoa maoni yao kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaijenga nchi hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile atueleze kwamba ni vijana wangapi ambao wamefunguliwa mashtaka na wamefungwa gerezani kwa sababu wamepatikana na hatia. Yote hii tunataka kujua ni namna gani nchi yetu ilivyoweza kuzuia uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ninataka kuzungumzia, yuko Mwandishi wa habari ambaye anaitwa Ansbert Ngurumo ambaye alikuwa anajaribu kuandika habari, kuwapasha habari Watanzania huyu mtu alianza kutishiwa kwamba anatoa habari ambazo zinaweza zikasababisha utulivu na amani ukatoweka katika nchi hii, huyu mtu aka...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka vitu vingine una uhakikanavyo lakini?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nina uhakika. Hii ya Ansbert Ngurumo nina uhakika nayo, hayupo yupo Finland na alitoa...

**SPIKA:** Huko Finland na sisi, si kaenda mwenyewe!!

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** *No,* analalamika...

**SPIKA:** Haya andelea kuchangia

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, anazungumza kwenye vyombo vya habari. Haya tunayotoa ni mawazo, tunatoa ushauri humu ndani ya Bunge, nia na madhumuni ni kuona Serikali inafanya mabadiliko, nia na madhumuni ni kuona Serikali inaacha uhuru wa vyombo vya habari, inaacha Watanzania wanatoa habari na wanatoa maoni yao kwenye Taifa letu. Nchi haijaanza leo, nchi imeanza muda mrefu, hii ni Awamu ya Tano ya Serikali katika Nchi hii ya Tanzania. Serikali zote zilizopita sheria zilikuwepo lakini Serikali ya Awamu ya Tano imetunga Sheria nyingi za makatazo, sheria nyingi ambazo zimesababisha…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka subiri kidogo. Naamini Waheshimiwa Wabunge mnapotaka kuchangia mnajiandaa. Ukitaka tu kuchangia unasimama tu, Serikali haitungi sheria anayetunga sheria ni ninyi wenyewe. Tunaotunga sheria ni Bunge, ukisema Serikali hii imetunga sheria nyingi, imefanya hivi unakuwa unawasingizia lakini cha muhimu hapa cha kuelewa; uhuru wa kutoa maoni siyo uhuru wa kwamba sisi tukishakuwa Wanasiasa ni kutukanwa na kila mtu, kusingiziwa na kila mtu, yaani ukishakuwa Mwanasiasa basi kosa. Mtu akutukane, akudhalilishe, afanye anachofanya, ukimuuliza nini anasema uhuru wa habari, hapana, hakuna uhuru huo.

Hivi wewe ukitoa maoni yako, ukayatoa tu maoni yako ukapinga jambo, ukafafanua jambo utagombana na nani? Tatizo *when they go to the person* na ili tuwafundishe vijana wetu wote tuna wafuasi hapa, tuwafundishe namna ya kutoa maoni yao badala ya kutumia kichochoro hicho cha uhuru kutukana watu, kudhalilisha, watu wana familia zao, tuna utamaduni wetu katika nchi, tunaheshimiana. Kitoto kidogo kinatukana mtu kama babu yake au baba yake itakuwa Taifa la aina gani hilo? *(Makofi)*

Kwa hiyo tunapoilaumu Serikali, mimi sikatai, lakini vilevile tuna jukumu sisi la kuwalea vijana wetu wajue hata kukosoa kwenyewe kuna utaratibu wake, kuna nidhamu

yake. Unapotaka kuiambia Serikali iambie katika utaratibu fulani lakini unapomtukana mtu anafunga masikio, hasikilizi. Yaani kuwa kiongozi ndiyo basi utukanwe tu kukicha? Haiendi hivyo.

Ndiyo maana naishia kwa kuwashukuru sana wale wanaoliombea Taifa hili, tumemaliza Pasaka vizuri, nawashukuru sana Watanzania walioliombea Bunge na waendelee kuwaombea viongozi. Ndiyo viongozi tunakosea lakini pia huombewa si lazima uwe unatukana tu kila siku, upige na magoti kidogo tuweze kuiona njia vizuri zaidi kama nchi tusonge mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawaonea huruma sana kwani mnatukanwa sana, mnadhalilishwa sana bila hatia. Mtu hata hajui chochote, hana *information* yeye mwenyewe lakini uhuru wa habari, huu ni utamaduni wa wapi wa kutukana watu hovyo?

Mheshimiwa Mwakajoka, mimi sipingi hoja yako na dakika nazitunza, nachosema ni kwamba tuna wajibu na sisi wa kuwafundisha hawa vijana waache habari ya kutukana watu. Endelea Mheshimiwa Mwakajoka. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru tu kwa kutoa ufafanuzi, lakini niseme ukweli tu kwamba nachoshangaa ni kwamba mnajitahidi sana kusimamia hali halisi hasa tukizungumza sisi, hebu tuchukulie mfano Gazeti la Jamvi kila siku linatukana Watanzania, Mheshimiwa Waziri yuko hapa, kila siku linatukana viongozi wa Vyama vya Upinzani, kila siku wanazungumzia akina Mheshimiwa Membe na kadhalika yaani kila siku linatukana, hata siku moja hatujaona hatua yoyote inachukuliwa. Sasa yote haya tunavyosema kwamba tunataka tuone nchi yetu inakuwa na utulivu na inafuata misingi hasa ni misingi gani watu wengine wanatukanwa tuko kimya na kila siku tunazungumza humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Yaani hilo tunakemea kwa pamoja, mimi na wewe tuko pamoja.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, tunazungumza ndani ya Bunge, Mheshimiwa Waziri yuko pale lakini hakuna hata siku moja kwamba hili Gazeti limefungiwa au limechukuliwa hatua yoyote kwa sababu tu hili gazeti inasemekana kwamba watu wanaolihudumia ni Serikali yenyewe, sasa hatuwezi kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Profesa Shivji amezungumza kwenye mtandao, akasema wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza tulipewa uhuru wa kutoa mawazo na uhuru wa kusema na wakati tunasema Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza alivyosikia aliwatuma watu wake waje watusikilize, walitusikiliza, tukawaeleza na wakatuelewa vizuri. Leo Tanzania mtu akitoa mawazo na maoni yake amekuwa ni adui, hilo jambo halitawezekana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka Profesa Shivji amezuiliwa na nani kuongea?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, *no*, amesema hivyo lakini hata ukisikiliza jana na hotuba...

**SPIKA:** Kama anasema hivyo anazeeka vibaya Profesa. Endelea Mheshimiwa Mwakajoka. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ukisikiliza Maaskofu wote waliohubiri siku ya Pasaka wamezungumzia jambo hili kwamba Tanzania uhuru wa habari kwa kweli imekuwa ni tatizo, ni lazima Serikali ikubali kupokea mawazo na maoni, iache uhuru wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tuko ndani ya Bunge pamoja na kwamba mlipiga kura nyingi humu mkasema Bunge lisiwe *live* lakini ukweli tu ni kwamba Watanzania wanahitaji sana kuona Wabunge wao wanasema nini lakini jambo hili limefungwa. Mambo mengi ambayo tunayazungumza ndani ya Bunge ambayo ni maslahi ya wananchi yamefungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tumepata taarifa kwenye mitandao na vyombo vya habari, *IMF* wamesema kwamba wanatakiwa waruhusiwe tu na Tanzania watoe habari ya jinsi gani uchumi wa nchi yetu unakwenda lakini mpaka sasa hivi kimya. Tunaomba pia Mheshimiwa Waziri aseme hii ni kwa sababu ya kutokuwa na uhuru wa vyombo vya habari. Vyombo vya habari vinaogopa kuandika kwa sababu wanasoma kwenye mitandao lakini wanasema wakiandika na kama hawajaruhusiwa inakuwaje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, una uhakika *IMF* imeomba itoe habari?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** *IMF* ndio imeomba?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, wameomba Serikali ya Tanzania iwaruhusu ili wachapishe ile hali ya uchumi wa nchi yetu kwa jinsi ambavyo wameiangalia. Wamezuiliwa, wameambiwa wasitoe. Sasa kama mmezuia na taarifa hiyo na walipa kodi wanataka kujua kuhusu kinachoendelea.

**SPIKA:** Yaani Tanzania ina uwezo wa kuwazuia *IMF* wasichapishe chapisho lao?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ni sheria lazima nchi husika iruhusu, sasa Tanzania haijaruhusu …

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, anatuchelewesha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, natumia Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inasema kwamba Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali tunachojua sisi bado tunaendelea kufanya mazungumzo na *IMF* kuhusu ripoti hiyo na si kweli Tanzania imezuia ripoti hiyo isitolewe. Sasa naomba kwa kuwa mimi nafahamu na Waziri wa Fedha yuko hapa anafahamu na ana maelezo ya kutosha tu kuhusu jambo hilo ambalo linapotoshwa na Mheshimiwa Mwakajoka, naomba ama Mheshimiwa Mwakajoka afute hizo *statement* zake za kuituhumu Serikali kwamba imeficha hiyo ripoti na haitaki ripoti hiyo itolewe au alithibitishie Bunge kwamba taarifa anazozisema ni sahihi na ripoti aliyonayo ni sahihi na hakuna jambo lolote ambalo linaendelea kwa sasa ndani ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Alichokisema Mheshimiwa Mwakajoka kidogo tu, *unless* unisahihishe Mheshimiwa Mwakajoka, alichokisema Mheshimiwa Mwakajoka ni kwamba Tanzania imewazuia *IMF* wasitoe hiyo taarifa yaani *IMF* inaomba kibali halafu *IMF* imezuiliwa Tanzania isichapishe hiyo ripoti, ndio jambo alilolisema. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika majadiliano ambayo yanaitwa *Article Four Consultations,* Timu ya *IMF* ilikuwa hapa nchini kuanzia tarehe 26 Novemba mpaka tarehe 7 Desemba, 2018. Baada ya pale walitoa taarifa na kwa utaratibu ni kwamba wakitoa ile rasimu ya taarifa inarudi Serikalini ili tuweze kuitolea maoni na wao waweze kuyazingatia kabla ya kuichapisha ripoti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo nilikuja kuiona tarehe 18 Machi. Hata hivyo, baada ya kuwa sisi tumepeleka maoni

yetu lakini tuliona hayajazingatiwa kwenye taarifa hiyo. Nilipokuwa Washington juzi zilizungumza na Bwana Abebe Selassie, Mkurugenzi wa *African Department* na mpaka leo saa tisa bado tutaendeleza majadiliano kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ni kwamba baada ya *Executive Board* ya *IMF* kuijadili taarifa hiyo, Serikali inakuwa na siku 14 za kuipitia na kusema itolewe au isitolewe. Kwa hiyo, wasiwahishe mjadala Serikali bado inazungumza na *IMF* na hakuna sehemu ambayo tumezuia ni utaratibu wa *IMF* yenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tuendelee Mheshimiwa Mwakajoka, nafikiri imekusaidia.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru tu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekubali kwamba ni kweli maoni yao hayakuzingatiwa na ndiyo maana hawajaruhusu. Kwa hiyo, sikuwa muongo kama alivyokuwa anazungumza *Chief Whip* pale Mheshimiwa Mhagama, niko sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine ambalo nataka kulizungumza hapa, tumezungumzia uadilifu katika nchi. Kuna gazeti lingine linaitwa Tanzanite. Gazeti hili limekuwa linaandika matusi kila siku ya Mungu, kuwatukana viongozi, kuwagombanisha watu, kuwaita watu magaidi na mambo mengine, mabaladhuri sijui namna gani, wanataka kupindua nchi, hawa watu wanatakiwa kuuwawa lakini Serikali iko kimya inatazama tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, Tanzania Daima nayo mbona hulitaji?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, aah, aah, unaona sasa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unataka kuniambia kwamba tusizungumze kwa sababu Tanzania Daima hatujalizungumza?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, lakini haya tunayokuambia unapaswa kuyachukulia hatua.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kama kuna vijana wanapigwa na wananyanyaswa kwa sababu tu ya kuandika kwenye mitandao lakini leo gazeti ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unamsumbua Mheshimiwa Mwakajoka dakika zake zinapotea.

**MHE. MCH. PETER SIMON MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kanuni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Wewe ulikuwa unataja magazeti nikakuongezea na lingine, endelea Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, gazeti linaandika, wewe unatuambia leo hapa kama Kiongozi wa Mhimili ambapo tulitegemea ungekuwa unatoa maamuzi mazuri kwa sababu umepewa uongozi...

**SPIKA:** Mimi nimekuongezea kwenye idadi yako tena unanilaumu kwa sababu nimetaja? *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, umetoa mwongozo mzuri hapa ukasema Mheshimiwa Mwakajoka ulipaswa kuzungumzia kuhusiana na hali halisi kwamba watu wasitukanwe lakini tunaona magazeti haya yanatukana watu, wanasema watu wanyongwe. Wameongeza watu, wanamtaja Mheshimiwa Heche, sijui nani kwamba hawa watu ni hatari wanyongwe, wanataja watu wanyongwe. Hivi kweli nchi hii mnakubali kwamba ni kweli kwa sababu ya mtu kutoa maoni yake, kuzungumza ndani ya Bunge au kwa kuonyesha msimamo wake huyu mtu anastahili kunyongwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado dakika moja.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane kwamba haya lazima tuyachukulie hatua na tusifananishe na kitu kingine. Ndiyo maana umesema kwamba tusiendelee kufananisha vitu ni lazima tuchukue hatua. Naomba pia hatua zichukuliwe, kama Mheshimiwa Waziri atashindwa kuzungumza kuhusiana na jambo hili tutaona kabisa kwamba hili gazeti ni la Serikali na wanatumwa kufanya hivi. Serikali inayoweza kuwatuma waandishi wa habari wakaandika vitu vya hovyo namna hii, hii Serikali itakuwa dhaifu sana na tunakoelekea kutakuwa siyo kuzuri hata kidogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unakoelekea sasa, Mheshimiwa Mwakajoka. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahaa, nimeisema Serikali siyo wewe, siyo mhimili wetu Mheshimiwa, huu nauheshimu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea, malizia. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusiana na

mambo ya michezo. Kwenye nchi hii tunapenda sana michezo na Serikali imekuwa inashangilia sana tunaposhinda.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza hivi juzi *Taifa Stars* imeingia *AFCON* tumemsikia Mheshimiwa Polepole anasema kwamba hii ni Ilani ya CCM. Sasa juzi tumepigwa mechi tatu zote mfululizo sijui Ilani ya CCM imeshindwa, maana sasa tunaingiza siasa kwenye michezo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka nijue Ilani ya CCM imeshashindwa tayari maana tumepigwa mechi zote tatu. Tukishinda Ilani ya CCM, tukipigwa hamsemi, yuko kimya Polepole. Naomba pia mumwambie ajitokeze aseme Ilani ya CCM imeshindwa ili Watanzania wajue kwamba Ilani ya CCM imeshindwa kwenye mechi hizi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, mimi Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, ila unajua siasa zikiingia kwenye michezo haiwezi kuwa bora hata siku moja. Tunachohitaji ni kukaa pamoja, ushindi wa Timu ya Taifa ni wa pamoja, ni wa Watanzania wote wanashangilia, wanafurahi kwa pamoja lakini inavyotokea ...

**SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa Mwakajoka. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Katibu, Katibu, Katibu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakajoka Frank. Mheshimiwa Frank bwana kila akisimama anatupiga kweli kweli bwana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Alhaj Nkamia, tafadhali. Jamani Bunge ndivyo lilivyo namna kidogo kidogo siku zinaenda au sio jamani? *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha sote salama. Mimi nitachangia mambo matatu. Kwanza, nitazungumzia kwa ufupi sana maandalizi ya Timu ya Taifa, *TBC* na *FIFA*, *ZDFA* na *TFF* na muda ukiruhusu nitazungumzia kwa ufupi sana suala la uhuru wa habari.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu wake na watendaji wote wa Wizara. Kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Filamu, dada yangu Fisoo na niwapongeze pia wasanii wote wa Tanzania, wanafanya kazi nzuri na wanafanya kazi kubwa kwa sababu kazi ya usanii ni ngumu sana na inahitaji ubunifu wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC)* ni Shirika la Umma lakini bila kuwezeshwa kuwa ni mitambo ya kisasa usikivu wake hauko vizuri sana. Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, nashukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa siku za karibuni imeonesha kujali Shirika hili lakini yapo maeneo haisikiki vizuri. Hata kwako kule Kongwa yapo baadhi ya maeneo haisikiki vizuri, hata kule Chemba lakini pengine nadhani Serikali ikihakikisha kwamba fedha zilizotengwa zinakwenda itasaidia zaidi *TBC* kusikika na kuonekana vizuri. Hata hapa Dodoma ule mtambo hauko vizuri, kwa hiyo, hata maeneo ya kwetu kule Chemba, Kondoa, Singida wakati mwingine ni tabu kusikika. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri jambo hili Serikali ikalitilia mkazo na kuangalia pia maslahi ya wafanyakazi wa *TBC,* nadhani baada ya siku Shirika hili litasimama kwa miguu yake yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nizungumzie maandalizi ya Timu zetu za Taifa. Ni aibu sana na lazima tukubali kama Taifa kwamba huwezi kuandaa mashindano halafu ukashika nafasi ya mwisho. Huwa inatokea mara chache sana, hata Korea walipoandaa Kombe la Dunia waliishia robo fainali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama kuna vitu ambavyo vilinishangaza ni kuona Kamati inasema vijana wale

wakichukua ubingwa wanawapa magari na shilingi milioni 20. Ni sawasawa na mtoto wako wa miaka 8 ana *birthday* unamwambia nitakununulia gari. Kwa hiyo, kuna mahali tulipwaya kidogo na pia hatukuiandaa timu hii vizuri kwa sababu hata mashindano iliyokuwa inakwenda kwa *trials* ilikuwa ni bonanza. Wamekwenda Rwanda kwenye bonanza, wakaenda wapi sijui kule kwenye bonanza hatukuwaandaa vizuri. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri sasa tuangalie *in future* tunawaandaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuwaangalie wachezaji hawa wanapatikana vipi kwa sababu nikiangalia ile timu ilikuwa ina wachezaji nane (8) wanatoka timu moja ya *Alliance* ambayo inashika karibu nafasi ya sita (6) kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Kwa hiyo, kuna tatizo hilo, nafikiri tuangalie namna gani tunaweza kuwapata vizuri.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Timu yetu ya Taifa ya *Taifa Stars* inakwenda kwenye michezo ya *AFCON* Cairo na michezo hii imesogezwa mbele tu kupisha mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao unatarajiwa kuanza tarehe 5. Mwezi ukiisha maana yake ni kwamba tunaenda kwenye mashindano, lazima tujiandae vizuri sasa. Tusipojiandaa vizuri tunaweza kwenda kushika mkia kwenye lile kundi, Mungu pisha mbali lakini kwa kweli lazima tujiandae vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo limekuwa likijitokeza sana ndani ya Bunge mwaka nenda miaka rudi, tangu mimi nimeingia ndani ya Bunge hapa 2010 linazungumzwa nalo ni suala la Zanzibar kuwa mwanachama wa *FIFA*. Kwa mujibu wa *United Nation Resolution No.*25, Zanzibar *is not a sovereign state*. *FIFA* inatambua *sovereign state except* Wales, Scotland, England na Ireland ambazo ni *founder* wa *FIFA*.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Zipo nyingi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nenda karejee kesi iliyoamuliwa katika Mahakama ya Rufaa ya

Khamis Machano. Nadhani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikae na Serikali ya Zanzibar kwa sababu nayo hii isiwe kama kero ya Muungano, Tanzania *Olympic (TOC)* ina mwakilishi kutoka Zanzibar ambaye kwa sasa ndiye Rais wa *TOC*.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ipo haja kwenye nafasi za Makamu wa Rais wa *TFF* mmoja akatoka Zanzibar ili kuondoa hii hali ambayo kila siku inatokea humu lakini Zanzibar kuwa mwanachama wa *FIFA* ni jambo gumu. *(Makofi)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Juni, 2011, Timu Maalum ya Zanzibar iliyokwenda *FIFA* iliandikiwa barua na aliyekuwa Katibu Mkuu wakati ule Bwana Volker kwamba Zanzibar *is not a sovereign state,* kwa hiyo haiwezi kuwa mwanachama wa *FIFA,* ni suala la busara tu.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumwarifu kwamba kwa mujibu wa *FIFA* mbali ya zile nchi wanachama za awali alizozitaja lakini pia kuna nchi ambazo sio *sovereign state* kama Macau, Hong Kong na nyingine pia ni wanachama wa *FIFA* kwa sababu nyinginezo. Uanachama wa *FIFA* hauko-*based or sovereign state* tu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ally, namheshimu sana, tumefanya naye kazi *BBC* na alikuwa anakaa kwangu. *(Kicheko)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, pia ni rafiki yangu, kuna tofauti kubwa sana unapoizungumzia Macau...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh unabisha hilo? *(Kicheko)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, sijawahi kukaa kwake. *(Kicheko)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, Hong Kong, Macau siyo *permanent member* wa *FIFA,* kwa hiyo, asipotoshe Bunge. Taarifa yako nimeipokea lakini siyo sahihi na kwa sababu ni rafiki tunaheshimiana hakuna sababu ya kugombana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hilo jambo ipo haja kwa Serikali kutumia busara.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hata Mheshimiwa Ally Saleh anafahamu hakuna nchi isiyokuwa na sheria. Huwezi kusimama tu unasema mimi kwa sababu ni mwandishi wa habari nitukane kwa sababu kuna uhuru wa habari, hakuna. Hata huko kwa wakubwa Mheshimiwa Ally Saleh wewe shahidi hakuna mtu anaweza kuandika tu akatukana Serikali au akatukana Kiongozi yeyote kwa sababu tu kuna uhuru wa vyombo vya habari, uhuru una mipaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani. Leo ni kweli yapo baadhi ya magazeti yanaandika vitu vya ajabu sana *and the Government is quiet.* Sasa upande wa pili kule wanasema hili Gazeti la *Tanzanite... (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kama ni msumeno ukate kotekote. Hilo gazeti unalosema la *Tanzania Daima* nalo ni moja kati ya magazeti ya ovyo sana katika nchi hii na ninashangaa linaachwa. La ovyo sana na mmiliki wake yuko humu humu ndani, rafiki yangu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Nani?

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, siwezi kumtaja, lakini yupo humu ndani na anasikia. kama hajasikia atapigiwa simu. Lazima tufike wakati kama Taifa, sheria za nchi ziheshimike. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, jamaa alinikata pale.

**SPIKA:** Muda hauko upande wako.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie bajeti ya Wizara ya Habari. Kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Juma Nkamia na kwa sababu sisi wote ni wanataaluma, tumekuwa katika taaluma ya habari, naomba niseme kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Tanzania ni nchi ya pili kwa Afrika Mashariki kwa uhuru wa habari, pamoja na kwamba imeshuka nafasi 10. Kwa mujibu wa *report* ya *Without Borders* na *The Press Freedom Index* ya 2018 Tanzania kwa Afrika na kwa dunia pia ni ya 93. Kenya yenyewe ni ya 96, Uganda ni 117, Rwanda ya 156 na Burundi ni ya 159. Kwa hiyo, utaona kwamba, Tanzania bado sisi ni kinara, tuko vizuri katika uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia imeshika nafasi ya pili kwa kuenzi uhuru wa habari na wa kisiasa. Imetanguliwa na Kenya kwa Afrika Mashariki na hii ni kwa mujibu wa *report* ya *Freedom House* ambayo ni ya mwaka huu wa 2019.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu hiyo, tunakumbuka kwamba mwaka 2018 Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alichaguliwa

pia kama kiongozi bora. Ni maoni na kura kutoka kwa wananchi katika Bara hili la Afrika ambao wametambua utendaji wa Rais wetu mpendwa kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niendelee kwa kuchangia. Ninaomba niende moja kwa moja kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC). TBC* ni Shirika la Umma na mashirika yote duniani hata ukienda *CNN, BBC,* yote hayo yamefikia pale kutokana na jitihada nzuri za Serikali. Na mimi nina imani kubwa sana na Serikali na jitihada kubwa anazofanya Rais wetu katika kuhakikisha kwamba *TBC* inasimama.

Mheshimiwa Spika, zile fedha tulizopitisha mwaka 2018, hata kwa bajeti ya mwaka huu utaona ni kwa jinsi gani tunaliboresha Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* ili liweze kuwa kama zamani lilivyokuwa pamoja na maslahi ya wafanyakazi wa *TBC.*

Mheshimiwa Spika, naomba pia, nizungumzie Waandishi wa Habari wa Tanzania. Hali ilivyo sasa ni mbaya. Waandishi wengi bado hawalipwi maslahi yanayostahili na wanafanya kazi katika mazingira magumu. Namwomba Waziri tuone ni kwa jinsi gani tunavyowasaidia Waandishi wa Habari ili basi na wao waweze kufurahia kazi yao.

Mheshimiwa Spika, sisi hapa bila Waandishi wa Habari, wananchi hawawezi kupata habari zinazoendelea.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina, Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kanuni ya 64(1)(a) inasema, *"Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-*

*(a) Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."*

Mheshimiwa Spika, mchangiaji anayeendelea kuchangia saa hizi amelieleza Bunge hili kwamba, Rais alichaguliwa kuwa Rais bora. Sasa naomba atusaidie tu kwa uelewa mpana kwamba hizi taarifa naona kama haziko sahihi, hizi kura zilipigwa wapi? Atusaidie tu kwa sababu, naona kama taarifa kidogo hazina...

**SPIKA:** Kanuni zetu zinasema wewe kwa kuwa umesema hajasema ukweli, wewe unausema ukweli sasa. Yaani wewe ndio uliambie Bunge ukweli ni upi? *(Makofi)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu, hili jambo sijawahi kulisikia, nataka tu kusema kwamba kwa nini Mbunge anayecha...

**SPIKA:** Sasa mbona umesimama kumbe hata hulijui! Basi huna hoja kaa. Endelea Mheshimiwa Amina, endelea na mchango wako. Endelea na mambo mengine tu. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kumsaidia tu aende katika Jarida la *African Leadership Magazine* ambalo lina Makao yake Makuu London, Uingereza, atapata taarifa hizi, lakini pia taarifa ziliwekwa wazi kwa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kuchangia. Niliishia pale kwa kuzungumzia Waandishi wa Habari. Naiomba Serikali na ninajua Serikali ni makini kuangalia kwamba hata baadhi ya wamiliki ambao hawawalipi Waandishi wa Habari ambao ni waajiriwa wao maslahi wanayostahili. Wapo

ambao bado wanadai mishahara yao. Waandishi wa Habari kwa kweli wana hali ngumu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kulisimamia hili kuhakikisha kwamba hawa waandishi wa habari wanaweza kulipwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, tuzungumzie pia suala zima la wasanii. Wasanii wa kizazi kipya wamekuwa na mchango mkubwa sana katika nchi hii. Nakumbuka wakati nafanya kazi ya Uandishi wa Habari miaka ya 1990 nyimbo zilizokuwa zimetawala ni kutoka Congo, kutoka Mataifa ya nje, lakini muziki wa kizazi kipya umebadilisha hiyo *mentality* na hivi sasa katika vyombo vyetu vya habari, redio, *TV* na hata maeneo mbalimbali ni muziki wa kizazi kipya.

Mheshimiwa Spika, ukienda Kenya, utaona jinsi ndani ya Afrika Mashariki, Tanzania tunavyoongoza kwa muziki huu wa kizazi kipya. Tuone sasa ni kwa jinsi gani tunawapatia haki zao, ambapo nakumbuka tulipitisha sheria kuona ile *percentage* wawe wanalipwa. Je, napenda kufahamu kwamba ile sheria tuliyopitisha, tayari imeshaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, je, tunajiandaa vipi katika kujenga kumbi za kisasa kama walivyo wenzetu, nchi zilizoendelea? Ukienda India kuna *Bolywood,* ukienda Marekani pia hivyo hivyo. Sasa je, tunafanyaje kwa nchi yetu hapa Tanzania? Tunaona sasa hivi filamu zimeporomoka hapa nchini kwa kweli, siyo kama ilivyokuwa. Naomba Waziri atuambie kwamba ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, niende pia kwa Msemaji Mkuu wa Serikali. Mimi binafsi nampongeza kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kuhakikisha kwamba yale yanayofanywa na Serikali yetu jamii na Watanzania wanatambua; lakini tuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba Ofisi hii ya Msemaji Mkuu wa Serikali inakuwa siyo idara, iwe ni ofisi maalum ambayo itakuwa na uhuru mpana zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia, kama ilivyokuwa Dar es Salaam tunaona Serikali imehamia hapa, lakini je, hapa

Dodoma Hakuna Idara ya Habari Maelezo? Wakitaka kuzungumza, wengi tutawasikia wamekwenda *Dodoma Hotel* na maeneo mengine. Tunahitaji kuwa na ukumbi wa kisasa ambapo watu mbalimbali watakwenda hapo kwa ajili ya kwenda kuzungumza na Waandishi wa Habari na sivyo kama ilivyo sasa hivi ambapo hatujui na hatujaona Ofisi Maalum ambayo ni ya Mtendaji Mkuu wa Serikali ambaye ni Msemaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atueleze ni kwa namna gani basi Serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba tunapata Ofisi Maalum ya Msemaji wa Serikali ambaye anafanya kazi nzuri sana katika kuweka mambo mazuri yanayofanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kutokana na utendaji huo ndiyo maana waafrika wengi wanatambua jitihada anazofanya Mheshimiwa Rais wetu. Nasi pia tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anayofanya na tunazidi kumtia moyo kuona kwamba tunakwenda katika nchi ya viwanda ambayo uchumi wake unakua. *P*amoja na changamoto hizo tulizonazo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Tanzania Rais Magufuli na Serikali yake nawaombea Mungu na iendelee kusonga mbele. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Bafadhil na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nianze na hoja ya uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba niweke *record* sawa kwamba *Tanzania Daima* imefungiwa mara kadhaa na kupewa onyo mara kadhaa. Tunachotaka, Serikali isikae upande mmoja. Tunapokuwa tunalalamika ndani ya Bunge, tunategemea Serikali itachukua maoni yetu na kuyafanyia kazi. Watu wanapoitwa ni hatari; na vyombo vya habari vinasomwa na watu wengi. Tunategemea Serikali aidha ichukue hatua inayowezekana kama ilivyochukua hatua kwenye vyombo vingine vya habari ikiwepo *Gazeti la Tanzania Daima. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la uhuru wa vyombo vya habari tunategemea Serikali ije na mkakati wa kuweza kuwalinda hawa wenye vyombo vya habari pamoja na Waandishi wa Habari. Mpaka nasimama hapa kuzungumza, kuna Mwandishi wa Habari ambaye mpaka leo yamekuwa malalamiko ya Waandishi wa Habari wenyewe pamoja na sisi Wabunge na wananchi wengine. Azori mpaka leo hatujasikia Serikali inasema nini juu ya huyu Mwandishi wa Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana haki ya kupata habari kwa mujibu wa Katiba yetu, lakini Waandishi wa Habari wana haki ya kutoa habari. Ni lazima tujue hapa ni kweli kwamba uhuru wa habari una mipaka yake, lakini hiyo mipaka isiwe pale ambapo Serikali inatakiwa kukosolewa. Serikali lazima ikosolewe. Ni kweli lazima kuwe na mipaka kwa sababu kila kitu kikipita kiasi ni sumu. Waandishi wa Habari wanahitaji ulinzi. Sasa hivi wanatishwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, anaweza akaja Mwandishi wa Habari kwamba tunaomba azungumzie utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano. Anapoanza kuzungumza, anakwambia aah, hayo siwezi kutoa kabisa. Sasa umeniruhusu nitoe mawazo yangu; hili suala litaleta shida sana kwa sababu, Waandishi wa Habari wanaweza kutoa

habari kwenye chanzo chochote. Sasa kama watawekewa mipaka na vitisho, sidhani kama tutalisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumetoka kwenye hali ambayo sasa tunaamini kwamba ni Taifa huru na uhuru wenyewe ni pamoja na Waandishi wa Habari kuwa huru kutoa kile ambacho wanaona kinastahili kutolewa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni BASATA. BASATA majukumu yao ni pamoja na kukuza wasanii wetu, lakini tunaona sasa majukumu ya BASATA yamebadilika. Wasanii hawa wanapokuwa wanaanza kule chini, jukumu la BASATA ni kuhakikisha wanakuza vipaji vyao, lakini leo tunaona wanaanza kuwafungia wasanii. Huyu msanii mpaka anaanza kutambulika na Taifa huko chini ana mikakati aliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, napenda nijue Serikali ina mkakati gani wa kuweza kukuza vipaji vya vijana wetu? Siyo wanakuja kuwatambua pale ambapo sasa ana uwezo wa kulisaidia Taifa kwa pesa zake kwenda nje. Kwa sababu sasa hivi kama msaanii anataka kwenda nje ya nchi lazima atoe taarifa kwa BASATA, lakini BASATA mbona hawajaja na mkakati wa kuwasaidia kuwatafutia huko nje; aidha kuwaunganisha na *network* ya wasaanii wengine ambao wako nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunategemea chombo hiki kiwasaidie na siyo kuwakandamiza. Jambo lingine ni viwanja vya michezo. Tunatambua kuna viwanja vingi ambavyo vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi, sitataka kuhoji sana kwa nini wanamiliki viwanja hivi, lakini nilizungumza Bunge lililopita kama wameamua kuvimiliki waviboreshe. Kuvimiliki tu halafu mkashindwa kuviboresha sidhani kama mnawasaidia Watanzania, kwa sababu viwanja hivi vingine kabla, tulipokuwa kwenye mfumo wa chama kimoja vilikuwa vinaendeshwa na Watanzania wote siyo Chama cha Mapinduzi peke yake. Sawa, mmevichukua, tunaomba basi mviboreshe ili viweze kuwasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa kujua, tunapokuwa tunazungumzia mara nyingi hapa, Wizara imekuwa inaleta watu tunawapongeza waliofanya vizuri, ikiwemo *Taifa Stars. Taifa Stars* ilifanya vizuri na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akatoa *promotion* ya pombe ambayo iliuzwa nusu bei.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri, labda inawezekana tunatafuta njia nyingine ya kuweza kuwasaidia vijana wetu, lakini sidhani kama ile njia ilikuwa sahihi sana. Kwa nini Wizara isije na mkakati; na hamuwezi kuja na mkakati kama hamjajua kwa nini tunashindwa. Kama wameshinda, Serikali ije sasa na mkakati, siyo wa nusu bei ya pombe kwa sababu watu walilewa na sidhani kama ilisaidia mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, sasa sidhani kama huo ni mkakati wa Wizara au ni yeye tu alikuja na ile *style* na hamjasema chochote mpaka leo. Kama itakuwa hivyo, basi tujue kama ni *style* ya Awamu ya Tano kwamba watakuwa wanawapa nusu bei ili vijana wetu waweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusisitiza, Serikali makini haiogopi kukosolewa. Naamini kuna mambo mazuri yanafanyika, sasa ili yaonekane ni mazuri lazima waruhusu mawazo ya watu wengine waseme. Hamwezi kufanya wenyewe, mnataka kujipongeza wenyewe, lakini anayetaka kukosoa haruhusiwi. Inajenga tafsiri ambayo siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie amejipangaje kuweza kuwalinda wamiliki wa vyombo vya habari, pamoja na waandishi wa habari. Ni namna gani hawa watu wanalindwa? Kwa sababu, hivi vitisho vimekuwa vingi sana.

Mheshimiwa Spika, mwandishi mwenzao wa habari, Serikali inasema nini? Imefikia wapi mpaka leo? Huyu mtu yuko wapi? Lazima Serikali iseme, kunyamaza kimya mnawafanya watu wanakuwa na sintofahamu. Wao hawawezi kusema, sisi ambao tupo kwa niaba yao lazima tuseme.

Mheshimiwa Spika, umezungumza vizuri kipindi anazungumza Mheshimiwa Mwakajoka. Narudia kusema ni vizuri kama sheria inafuatwa kwenye vyombo vya habari, wasiangalie baadhi ya vyombo vya habari. Hili jambo la kutaja watu hadharani kwamba hawa watu ni hatari, kuna mambo mpaka ya ushoga yameandikwa kwenye magazeti.

Mheshimiwa Spika, kuna viongozi ambao wameaminiwa na watu, ni vizuri Serikali ije iweke sawa jambo hili. Kama kweli kuna watu wanafanya mambo hayo, sheria iko wazi, kwa nini wasipelekwe huko kwenye vyombo vya sheria ili sheria ikatafsiri kwamba huyu mtu anafanya kosa la ushoga? Sheria iko wazi, kwa nini chombo hiki kinaandika na Serikali inakaa kimya. Je, tuamini kwamba ni kweli Serikali imepeleka hayo mawazo ili gazeti liandike? Kama sivyo, Serikali isimame hapa itoe maamuzi juu ya chombo hiki. Ukisema hawa watu ni hatari, uhatari wake uko wapi? Umewataja majina na picha zao ziko pale.

Mheshimiwa Spika, wengine ni viongozi ambao tunawaamini, wanaongoza watu wengi ambao wako huko nje. Vinapotokea vitu kama hivi, hatari siyo mpaka mwone watu wanaandamana. Ukiona watu wanasema wengine wanaandamana mioyoni.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri huo mwongozo uliotoa ukautoa na kwenye Wizara. Haya malalamiko ya kila siku, hili gazeti ni la nani? Linasukumwa na nani? Nani yuko nyuma ya chombo hiki cha habari? Kama kuna ukweli, hatua zichukuliwe siyo kunyamaza kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Yaani Mheshimiwa Aida mwanzo mwisho hausifii hata robo, hata kitu kimoja!

Mheshimiwa Nuru Bafadhil tafadhali, Mheshimiwa Shangazi ajiandae.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi kuzungumza machache kuhusu Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwanza, nitazungumzia kuhusu utamaduni. Watanzania tuna tamaduni zetu za asili, tamaduni ambazo zilikuwa zinatuonesha kama kweli sisi Watanzania, lakini sasa hivi hizi tamaduni zinapotoshwa sana kwa kuiga mambo ya kimagharibi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale Tanga kuna makabila katika Mkoa wa Tanga; kuna Wabondei, Wasambaa, Wazigua, Wadigo, tuseme ndio wenyeji wa Mkoa wa Tanga na wana ngoma zao nzuri tu; wanacheza ngoma zao vizuri, lakini utakuta ngoma hizi sasa hivi zinapotoshwa katika ile michezo yake ya kiasili.

Kwa mfano, katika Jiji la Tanga kuna ngoma inaitwa Baikoko. Yaani ukitaja ngoma ya asili ya Tanga ni Baikoko. Nataka kuwaambia ngoma ya Tanga ya asili siyo Baikoko, ile Baikoko ni ngoma ambayo inapotosha sana watoto na kizazi hiki tulichonacho kwa sababu ile ngoma ni matusi matupu mwanzo mwisho. Matusi na watu kukatika katika, yaani mtu kukatakata mauno ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mtu ukimwambia utamaduni anaona labda kusimama na kukatikakatika inakuwa ndiyo utamaduni. Kumbe akiimba ule wimbo ukiwa una ujumbe fulani utawafikia watu, watu wakauelewa ule ujumbe, ndio utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, pia mfano mwingine kuna ngoma ile ya Hiyari ya Moyo, nilipokuwa mdogo, tulikuwa tunakwenda Tanga kuangalia ile ngoma. Mimi nilikuwa naona ngoma ya Hiyari ya Moyo wanacheza tu wanatingisha mabega, lakini sasa hivi mpaka mtu anakatika kabisa mpaka...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kama mtu anaangalia yaani ile ngoma...

**SPIKA:** Mheshimiwa Nuru pokea taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa mzungumzaji, huu ni utamaduni wa kukatika viuno, sasa nashangaa anasema wanakatika viuno. Hivi tuulizane humu ndani ya Bunge, kuna watu wasiokatika viuno?

**SPIKA:** Mheshimiwa Nuru vipi, mimi sijamwelewa lakini labda umemwelewa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Aaa.

**SPIKA:** Haya endelea Mheshimiwa Nuru labda mwenzangu umemwelewa, pokea taarifa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, taarifa siipokei kwa sababu Mheshimiwa Keissy naye anapenda kujipitisha pitisha, samahani kama panya, panya akitaka kutajwa ajipitisha kwa watu.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Kwa hiyo, mimi ninachosema, hebu tujaribu turudi kwenye tamaduni zetu...

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Turudi kwenye tamaduni zetu za kizamani, tufanye...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Nuru, taarifa nyingine unapata. Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla tafadhali.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayesema

hapa Bungeni kwamba utamaduni sio kitu *static,* utamaduni ni *dynamic* unabadilika kutokana na nyakati. Kwa hivyo, utamaduni wa watu wa Tanga hata mimi bibi yangu anatokea Tanga, Machui, umeendelea kubadilika zama na zama ndio maana leo hii hata muziki upo unaoitwa muziki wa kizazi kipya ambao wanaimba akina Sugu na Profesa Jay.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, utamaduni unabadilika, hata lugha ya Kiswahili ukitaka kutafuta lugha ya Kiswahili ni nini imetoka wapi, ni lugha imeibuka zama hizi za miaka hii ya 1900, lakini haikuwepo, sio lugha ya asili. Kulikuwa na makabila zaidi ya 128, lakini yanaunganishwa na utamaduni mmoja wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, napenda afahamu kwamba utamaduni sio *static* ni kitu *dynamic.*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa, anakwambia tu mambo yanabadilika, hayo unayoyaona leo ndio yenyewe.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, asante na ndio kanipeleka mbele ngoja niende mbele halafu nitarudi nyuma, ndio hayo nilikuwa mengine nataka kuchangia. Sasa hivi Watanzania tunachanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili, tunatakiwa tukinyooka kwenye Kiswahili twende kwenye Kiswahili tu tusichanganye lugha Kiswahili na Kiingereza hapana, tunapoteza uzalendo wetu na Utanzania wetu. Tuzungumze lugha moja tu, sisi tunasema tunazungumza Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa, tusichanganye maneno.

**SPIKA:** Anasema tusichanganye changanye maneno Waheshimiwa, unazungumza, mara *mother tongue* sasa inakuwa tabu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Nuru endelea.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Vile vile nikizungumzia kuhusu muziki wa kizazi kipya, kweli tunaupenda muziki wa kizazi kipya, lakini na huo muziki wa kizazi kipya tuuangalie je, ukoje? Je, Wizara kama Wizara au

BASATA je, inazihakiki zile nyimbo? Mfano tukiimba sijui nyege nyege Nyegezi kwetu Mwanza Nyegenzi, wimbo kama huu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Nuru unavunja Kanuni. *(Kicheko)*

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, samahani.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Kwa hiyo, tunatakiwa tulete nyimbo ambazo zina mantiki, zinapendeza mpaka anayezisikia pia pale alipo hata kama alikuwa anaandika atachezesha hata mkono kuona kuwa ule wimbo umemwingia. Kwa hiyo, nyimbo tunazoziimba tunataka nyimbo za kizazi kipya lakini nyimbo ziwe nyimbo zenye mafundisho mazuri sio nyimbo ambazo zinaleta maana mbaya mpaka watoto wanaozisikiliza haziwasaidii chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na nyimbo zenye mafunzo, tulikuwa na akina Mwinamila walikuwa wakiimba mpango wa pili wa maendeleo, unasema, kuleni kuku, mayai, mboga, samaki, maziwa; kuleni chakula bora cha kujenga mwili na kulala kwenye nyumba bora, si ndio? Tulikuwa tunafundishwa kuwa tunatakiwa tule chakula na wakati huo huo tulale kwenye nyumba ambazo ni bora, lakini leo nani kamwaga pombe yangu, nauliza. Sasa hiyo jamani kweli tutakuwa, kwa hiyo tutakuwa hapo hatufanyi... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sugu uende ukawaeleze wenzako, huu ndio ujumbe, ukaeleze kundi lako huko. *(Kicheko)*

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, Ninachoomba twendeni turudi kwenye tamaduni zetu za asili japokuwa kuna nyimbo za kizazi kipya, lakini zile nyimbo za kizazi kipya ziwe na nyimbo ambazo maudhui yake yanalenga kuwajenga wale wanaozisikiliza.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia kuhusu Serikali kuona umuhimu tuwe na shule zetu maalum za wanafunzi wenye vipaji maalum yaani tuwe na shule ambazo tutawapeleka kweli wanasoma masomo mengine lakini wakati huo huo anaendelezwa kimichezo kama ni bondia, mchezaji mpira, labda ni muigizaji, vyovyote inavyokuwa vile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawajengea ile shule na wanakwenda pale, kwa hiyo wakimaliza pale, tunapata wanafunzi ambao ni *cream* kwa kuwapeleka mahali na kuwa wanashiriki katika kuliinua Taifa letu kwa sababu michezo ni afya na vilevile michezo ni ajira.

Kwa hiyo, tukipata watu namna ile tunaweza tukaendelea, kama wenzetu Nigeria walivyowekeza, akina Kanu wale walikuwa wapo kwenye shule za vipaji maalum mpaka leo tumeweza kupata wachezaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu wake, Mheshimiwa Naibu Waziri alikwenda Tanga kuweka jiwe la msingi katika eneo ambalo litajengwa kiwanja kikubwa sana cha michezo. Ninachoomba sasa hivi Serikali angalau ijaribu kujenga uzio kwa sababu wananchi wanajaribu kusogea na mwisho ule uwanja utamezwa, utakuja kukuta wengine watakwambia wanadai fidia walipwe ili waweze kupisha ujenzi wa kiwanja. Kiwanja kile kama kitajengwa kitakuwa kizuri na kitapendeza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nuru.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyopo mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuanza na nukuu ya Katiba kwenye Ibara ya 18 ambayo ndio inayoleta mjadala mpana humu ndani kuhusu haki na uhuru wa mawazo. Hata hivyo, Wabunge wengi wakisoma kipengele hicho hawaendi kwenye Ibara ya 30(1) ambayo naomba niisome; haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii havitatambuliwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, sasa ndugu zangu ni sahihi kabisa kwamba tunao uhuru lakini uhuru wetu una mipaka na mipaka yenyewe ni pale uhuru wa kwako unapoanzia kuna mahali unaishia na uhuru wa mtu mwingine unaendelea. Kwa hiyo, ni lazima tunapolizungumza hili tujielekeze katika ibara zote mbili za Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo huo, naomba nianze na suala hili la vyombo vya habari kuishauri Serikali kwamba ni kweli tulipitisha sheria ndani ya Bunge letu Tukufu lakini jukumu la kutengeneza kanuni tumeliacha kwa Waziri mwenye dhamana tukiamini kwamba atawashirikisha wadau wote katika kutengeneza kanuni. Sasa kwa kuwa sheria kidogo ni ngumu kurudisha mara kwa mara lakini tunaamini kwamba kanuni zikionekana kwamba kwa nyakati tofauti haziendani na sheria tuliyopitisha, basi nimwombe Waziri kwamba sio vibaya kuitisha tena vikao na wadau kuweza kujadili ili kuondoa hizi sintofahamu ambazo tunaziona na zinazungumzwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya hili lote ni kwamba sasa hivi karibu kila Mtanzania ni mwanahabari kwa sababu ya mitandao hii ya kijamii *Instagram, WhatsApp* na *Facebook,* chochote mtu anachofanya ana-*post* matokeo yake baadaye kinaenda kwenye jamii na tunaona kwamba ni jambo la kawaida. Ni vizuri sana hasa kwa kuwa

tumeanzisha maudhui ya hizi *online broadcast,* tuwe makini sana katika eneo hili la kila Mtanzania kuwa Mwanahabari.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni lazima pia hawa Waandishi wa Habari wanaandaliwa kwa namna gani, hili nalo ni jambo la msingi sana. Tumeona vyuo vyetu vingi vya habari vinavyoandaa Waandishi wa Habari ni vya kawaida sana mtaani, ni vya kawaida mno kiasi kwamba hatutarajii kwamba vyuo hivi vije kutengeneza Wanahabari mahiri. Kwa hiyo na lazima hili nalo Serikali ilione kwa sababu yenyewe ndio yenye jukumu la kuhakikisha kwamba tunapata habari ambazo zinalinda mila na desturi zetu kama Watanzania lakini pia zinazingatia uhuru wa Taifa letu na pia kuzingatia usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa leo inawezekana ukakutana na mwandishi wa habari hata hizo sheria zinazoongoza mambo ya usalama wa Taifa hazijui, lakini ni kwa namna ambavyo vyuo vinavyowaandaa ndio ambavyo nadhani tatizo linaanzia hapo. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikatengeneza mitaala kwa kushirikiana na wadau, lakini pia kuboresha vyuo vile ambavyo vinatoa maudhui ya habari ili tuweze kupata Waandishi ambao ni mahiri katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, juzi tulipata wageni kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Duniani *(IPI)* na nilipata bahati ya kuzungumza nao. Wakati tunazungumza walikuwa wamejaribu kulishwa hii dhana kwamba Tanzania hakuna uhuru wa vyombo vya habari, wakaeleza baadhi ya maeneo. Nami katika kujadili tukawa tunazungumza mmojawapo alikuwa anatoka India, nikamuuliza kwamba kwa mfano sasa hivi India ina mgogoro mkubwa sana na Pakistan, nikamwambia inawezekana kweli Mwandishi wa Habari wa India aka-*side* na Pakistan akiwa ndani ya India kuhusu labda ule mgogoro unaoendelea pale katika eneo la Kashmir. Alivyonijibu tu akasema hiyo wala inawezekana kama yupo kwenye chombo cha habari wala hatatoka hata ndani ya chombo cha habari.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba sisi tunadhani kwamba uhuru wa habari ni kila kitu unaweza ukaandika, lakini hawa wenzetu ambao tunatoa mifano kwao na wao wana miiko. Mwingine alikuwa anatoka Ujerumani, wakati tunazungumza naye akasema hivyo hivyo kwamba hata kule Ujerumani kuna mwandishi mmoja aliwahi kuandika habari akatoa picha ambayo inaonesha kifaru cha Ujerumani jinsi ambavyo kilikuwa kimechakaa kwamba je, ikitokea sasa hivi wanagombana na nchi fulani, kwa kifaru hiki tunaweza tukashinda vita? Basi mwandishi yule wala hakuweza kuonekana tena, alikuja kuonekana baada ya mwezi mmoja. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba sio kwamba hakuna uhuru ambao hauna mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwa uchache sana nielezee habari ya michezo kwamba kwenye michezo nako kuna tatizo. Ni kweli kwamba tumefuzu kwenda *AFCON* 2019, lakini lazima tujione kwamba kwanza nchi zimeongezwa ambazo zinashindana, zamani zilikuwa 16 sasa hivi zimefika 24. Kwa hiyo, inawezekana labda ni baada ya kutanua goli ndio tukapata nafasi. Jambo la msingi hapa ni kwamba lazima tuwe na mikakati ya dhati kabisa ya kukuza michezo. Chuo cha Michezo kule Malya ni kwa kiasi gani kinasaidia kutengeneza kama sio Walimu wa michezo kwenye shule lakini hata Makocha ambao wanakuja kufundisha vilabu vyetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwa mfano nchi jirani ya Burundi hapa ina Makocha kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara karibu sita kutoka Burundi na wote ni wa kizazi ambacho kinalingana. Kina Ndailagije, Masoud Juma kuna yule Ramadhan wa Mbeya *City* lakini hapa kwetu Tanzania kuna programu gani ya kupeleka Makocha wetu hawa au vijana wakapate *exposure* ya kujifunza mbinu/medani mbalimbali nje ya nchi. Kwa hiyo, nadhani hili ni eneo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia michezo shuleni, bado michezo shuleni haifanyiki kwa kiwango kile ambacho tulikitarajia na vile ambavyo huko nyuma kilikuwa

kinafanyika. Mheshimiwa Mwakyembe amesoma Shule ya Wavulana Tabora na ameona ni shule ambayo ilikuwa imejiimarisha kwenye kila aina ya mchezo, alikuwepo pale, nadhani mchezo pekee ambao haukuwepo pale ni *netball.* Hivi leo katika tasnia hii ya michezo, hapa mpira wa pete huuoni ukifanya vizuri, kurusha tufe na mkuki hatuoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaona michezo ile ile ambayo jamii imeikubali ndiyo ambayo tunaiona lakini bado kuna michezo mingi ya kukimbia na kadhalika hatuoni ikipewa kipaumbele sana na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana, nimeuliza swali wakati mmoja kuhusu Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Taifa, hebu tupitie hii sera kwa uharaka ili tuweze kutengeneza sera nzuri ambayo pamoja na kushirikisha sekta binafsi, lakini pia Serikali itachukua jukumu lake la msingi la kuhakikisha kwamba sio tu kwamba michezo inakuwa ni sehemu ya burudani, lakini pia michezo inakuwa ni sehemu ya ajira kama ambavyo sasa hivi tumeona duniani kote michezo inaajiri watu wengi sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini sio kwa umuhimu, ni vifaa duni vya *TBC.* Ni kweli shirika letu la Utangazaji *TBC* linafanya kazi nzuri sana sasa hivi na limezidi kujenga imani kwa Watanzania, lakini vifaa hawana. Mfano mzuri upo hapa hapa ndani ya Bunge, ukienda kwenye *Studio* ya Bunge ile ambayo *TBC* wanarekodi ile *mic* lazima wanapokezana, kuna wakati mwingine imefungwa na *rubber band.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana kwamba ili tuweze kuwa na shirika ambalo linalofanana na Taifa letu kwamba Taifa linapiga hatua, lakini pia Shirika la Utangazaji la Taifa tulione kwamba ni shirika ambalo linaweza kushindana na vyombo vingine vya Kimataifa lakini pia na vyombo binafsi ambavyo tunaona vinafanya vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, baada ya hapo Mheshimiwa Naibu Waziri halafu mtoa hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanazofanya, kwa kweli Waziri na Naibu wapo karibu sana na Wizara hii na wadau wote wa michezo na sanaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Rais juzi alimzawadia Peter Tino shilingi milioni tano na hali ya wachezaji wetu wa zamani ambao wamecheza mpira miaka ya 1980 ni mbaya sana. Mheshimiwa Rais ameonesha njia, najua *TFF* inajitawala haiko chini ya Wizara, lakini Wizara ndio *custodian* wa michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara, wawashauri *TFF* katika bajeti zao angalau wachezaji walioshiriki timu ya Taifa miaka ya 1980 ambao sidhani kama wamebaki hata 10 au 15, najua yupo Manara, Kitwana na Mbwana nafiriki bado yupo, wawapatie bima kuwasaidia wachezaji hawa kwa mateso wanayoyapata sasa hivi mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Jellah Mtagwa namna alivyotumikia Taifa katika michezo hasa mchezo wa mpira. Katika miaka ya 1990 na 1980 Jellah Mtagwa alitumika picha yake kwenye stempu za Tanzania; Shirika hili la Posta sasa hivi lina wajibu wa kumkumbuka Jellah na kumsaidia kwa mateso ya magonjwa ambayo anayo sasa hivi. Ushauri wangu *TFF* iwakatie bima wachezaji wote wa zamani ambao wako hai ili waepukane na mateso ya maradhi ambayo wanayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile wachezaji wote waliocheza timu ya Taifa upo wajibu wa *TFF* kuweka majina yao kwenye uwanja mpya wa Taifa ili kuwa-*inspire* wachezaji wapya na wakumbukwe kwa picha na majina kwa namna walivyochangia ushindi. Wapo wachezaji waliocheza *goal*

*stage* bado wapo ili na wao waonekane na vijana wetu wawe *inspired* na wachezaji wetu wa zamani.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Bodi ya Ligi ya *TFF;* tumeona namna wanavyo-*approve* viwanja vibovu vichezewe ligi. Wachezaji wakicheza kwenye viwanja vibovu na ambavyo vingi vipo wanaumia sana. vilabu hivi vinapata gharama kubwa sana kutibu wachezaji ambao wanacheza na wanaumia kwenye viwanja vibovu vya *premium league.* Naomba bodi hii sasa ivifungie viwanja vyote kwa msimu ujao ili kila kiwanja kiboreshwe na kitengenezwe vizuri na wale ambao viwanja vyao havitafungiwa watafute viwanja mbadala kuepuka wachezaji kuumia na viwango vyao kunini.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii tena kumshukuru Rais kwa namna alivyochangia *AFCON U-17* alitoa bilioni moja, tumefungwa, lakini tusikate tamaa bado tunayo nafasi. Vijana hawa wapewe moyo; hamasa zilikuwa nyingi, lakini maandalizi yetu hayakuwa mazuri. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa mchango wako mfupi lakini ulio moja kwa moja, unaojielekeza kwenye masuala mahususi.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi za dhati kwa Rais kutokana na utekelezaji wake kwa maendeleo ya nchi kwa wananchi wake. Jinsi anavyowasimamia na kuwaelekeza wasaidizi wake katika kutimiza majukumu yao kwa mafanikio ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri bila kuwasahau Katibu Mkuu na wataalam wote ndani ya Wizara kwa kusimama na kutekeleza majukumu yao na kutuwezesha wananchi na wadau wapenda michezo utamaduni na sanaa kufarijika na kuwa na matumaini

makubwa kwa kusonga mbele na michezo, sanaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwamba inasikitisha kila vijana wanapojitahidi kufanya vizuri wanaishia kwenye robo fainali. Naomba nasi tuwachukue vijana wetu kipindi chote na haya mazoezi ya kila siku kama ajira kwao, hadi mashindano yawakute humo humo, kuliko tunavyofanya mazoezi ya matukio, ni kazi ngumu ndiyo maana tunaishia mahali duni. Hivyo tubuni kitu cha kuzalisha ili tupate mapato ya kuwalipa kila mwezi hawa wachezaji ili wafanye mazoezi ya kuleta ushindi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba chuo cha kuandaa wataalam wa michezo, sanaa na utamaduni kuboreshwa na kuongezewa wigo ili tupate uelewa zaidi ya kiwango cha juu, tunahitaji nasi Tanzania tuwe mfano ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wacheza sanaa wa upande wa watoto wa kike, mavazi yao hayana maadili mema. Ni vema uwepo utaratibu wa kufunika miili yao kuanzia kifua hadi chini ya magoti yao na wakacheza vizuri tu. Kwa mfano wanaume wanacheza vizuri na wakati mwingine zaidi ya wa kike huku wakiwa wamevaa kamilifu. Tunaomba sasa wakati umefika turekebishe sheria, kanuni na taratibu zitakiwavyo kuhusu mavazi ya watoto wa kike yatumikayo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba uwepo utaratibu kwa wachezaji wasanii na utamaduni kuwekewa bima ya afya. Pia uwepo utaratibu wa kuwaelimisha kila mara, waepukane na utumiaji wa madawa ya kulevya. Tunapendekeza tunapohitaji kutoa zawadi kwa vijana wetu ni vema tukaendeleza zawadi ya Rais aliyotoa hivi karibuni ya viwanja na hatimaye tuweze hata kuwajengea nyumba za bei nafuu kuliko pesa hatimaye wanakimbilia kununua vitu vya anasa, visivyo na faida baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sanaa, michezo na utamaduni kama kichocheo cha fursa za kiuchumi na umoja na upendo kwa Taifa letu. Takwimu za ukuaji wa kiuchumi katika nchi yetu zinaonesha kwamba sekta hii inachangia zaidi ya asilimia kumi na moja ya pato la Taifa. Hii inaashiria kuwa tukiwekeza zaidi tunaweza kukuza na kuongeza zaidi pato la Taifa letu. Hivyo nashauri Wizara ya Fedha iongeze ukomo wa bajeti kwa Wizara hii ili iwekeze zaidi kwa sekta za sanaa, utamaduni na michezo, kwani bajeti katika Wizara hii ni ndogo sana. Tuwekeze kwenye vyuo vya michezo pia TASUBA na masuala ya utamaduni.

Mheshimiwa Spika, uhuru na haki ya kupata habari nchini; Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoridhia na kusaini azimio la kimataifa la uwazi katika uendeshaji wa Serikali. Kupata habari wananchi ndio utawala bora. Imekuwa ni kawaida sasa wananchi hawaoni Bunge *live* kwa kuwa wanataka kuona wawakilishi wao wanapeleka hoja zao kwa Serikali. Hivi ni kinyume kabisa na haki ya kupata habari na masharti yaliyoridhiwa.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa bajeti ya maendeleo; bajeti ya maendeleo haitoki kama inavyoombwa na kumekuwa na changamoto nyingi katika W izara hii na miradi ya sekta hii katika uwanja wa Taifa, wadhamini mbalimbali wamekuwa wakihudumia uwanjahuo wakiwemo Wachina ambao mkataba wao unaishia mwezi Agosti, 2018 na *sportpesa* mkataba wao mwisho mwezi Mei, 2018. Hata hivyo, hakuna mkakati wowote unaoonesha viwanja hivi vitashughulikiwa kwa kuwa hata bajeti haijajionesha wazi. Waziri anapohitimisha atueleze mkakati ukoje wa kuhakikisha uwanja huu umetunzwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nazidi kusisitiza kuwa na maandalizi mazuri ya michezo kuanzia *under* 17 kwa jinsia zote, kuwe na mkakati wa mafunzo maalum na maandalizi kwa timu zetu. Ahsante sana.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa Taifa – BASATA; lengo la Baraza hili ni kuboresha ubunifu pamoja na kuibua vipaji mbalimbali pamoja na utafutaji wa masoko yenye ubora kwa wasanii.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* na BASATA; hivi vyombo viwili vinavyofanya kazi pamoja, lakini kuna changamoto kubwa kupitia mlolongo mrefu wa usajili kwa wasanii kupata *(stamp)* za *TRA* ili kazi ya msanii iingie sokoni na ukizingatia mikoani ofisi hizi zinalega na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna kanda hazina ofisi za Baraza hili *COSOTA* na BASATA na hii inapelekea kwa wasanii wachanga kushindwa kufuata hatua hizi na uchumi wao mpaka afike Dar es Salaam ndipo apate usajili. Je, hawaoni kwa kushindwa kupeleka huduma kila mkoa ni kuwaumiza wasanii ambazo wako tayari kusajili kazi zao na huku milolongo hii ikiwagharimu? Ni lini watajenga ofisi zao kila mkoa ili kuondoa usumbufu huu?

Mheshimiwa Spika, dhana ya kufungia vyombo vya habari; Sekta ya Habari tulitegemea lengo lake ni kuhabarisha kuelimisha kukosoa na kuburudisha, lakini dhana hii inabadilika kila siku kwa kufungia vyombo vya habari ambavyo vimekuwa vikifungiwa na kufunguliwa gazeti la Mawio Mwanahalisi, Raia Mwema, na baadhi ya redio. Ni kwa nini wanatoka katika dhana ya ukosoaji na wanataka kusifiwa tu?

Je, lengo la Wizara hii ni kwa nini linajikita zaidi katika masuala ya siasa na kuacha kufungia kazi za wasanii, filamu ambazo kimsingi ziko mtaani na zinaharibu jamii. Wana mpango gani katika suala hili kuchunguza kazi zinazosambaa katika jamii video, audio na picha chafu kwenye mitandao hawaoni kwamba wameshindwa?

Mheshimiwa Spika, *Cyber Crimes Act* na Sheria ya Takwimu. Makosa ya kimtandao ambayo kwa ujumla yanaminya uhuru wa kupata habari na kusambaza hili ni tatizo na limepelekea jambo hili kutumika zaidi kisiasa. Sheria hizi zinaminya uhuru wa kujieleza na kukiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, ajira; malalamiko ya wasanii ni mengi katika tasnia hii hususan katika maslahi yao. Sanaa ni ajira, hivyo, tunaishauri Serikali kusimamia maslahi yao na mafao yao ili kuhakikisha wachezaji wasanii wanapata haki zao.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa wasilisho zuri pia jitihada za dhati kabisa za kusimamia tasnia hizi za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nianze kwa kuchangia upande wa vipaji ambavyo vinahitaji kuendelezwa. Watoto wengi hasa mikoani (vijijini) wana vipaji lakini wanakosa mtu wa kuwashika mkono, mfano, ni Kituo cha Michezo cha Manga, Wilayani Handeni, Tanga ambao wamefikia kutoa mtoto mmoja anayeshiriki timu ya *under 17*, lakini hawana uangalizi ambao laiti ungekuwepo tungepata wachezaji bora kabisa wa mpira wa miguu. Pia vipaji mashuleni viufuatiliwe na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, pia tunaona kumekua na wimbi la vijana wengi wakijiunga na ajira ya *online TV*. Hili limesaidia katika kupunguza tatizo la ajira. Ila vijana hawa wanakwamba kwenye ada za kujisajili, Serikali ingeangalia uwezekano wa kuwasaidia angalau waruhusiwe kufanya kazi zao ili mradi wanafuata taratibu na sheria za nchi na hizo ada za usajili zikatwe katika mapato yao ya kila mwezi au wapewe muda walipe taratibu hadi wakamilishe huku wakiendelea na shughuli zao na kujiingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mitandao kusaidia sana katika shughuli mbalimbali za kila siku za jamii kujiingizia kipato, burudani na hata kupashana habari mbalimbali bado kuna wimbi la wanaotumia mitandao vibaya kama vile kutuma ujumbe mfupi unaolenga kutapeli, kufanya biashara za ngono, kutukana katika mitandao, vitu ambavyo nashauri Serikali iweke adhabu kali na zitangazwe hadharani ili wengine waogope wasione kama ni maneno tu bila vitendo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iboreshe viwanja vya mpira hasa mikoani. Viwanja vingi vipo katika hali mbaya na vinahitaji maboresho hasa uwanja wa Mkwawani, Tanga ambao ni uwanja wa siku nyingi na moja ya viwanja vikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, bado mikataba ya wasanii wetu haiko vizuri na wanachopata hakilingani na kazi wanazofanya. Serikali ingeangalia uwezekano wa kuwa na mkataba maalum unaotoa maelekezo ya ujumla kwa wasanii wote, mfano, kama msanii atatumika katika tangazo au kazi ya aina fulani malipo yake yaweje ili kuondoa ukandamizaji unaotokea kwa wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha leo kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwenye hoja iliyo mbele yetu. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwenye Wizara hii Dkt. Harison Mwakyembe, Mheshimiwa Naibu Waziri Juliana Shonza pamoja na watumishi wote wanaohudumu katika Wizara hii, wote kwa pamoja nawapongeza sana kwa kufanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Redio Tanzania, *TBC FM* hii ni redio ya Taifa lakini usikivu wake katika baadhi ya mikoa ni mbaya sana na mikoa au wilaya zingine hakuna kabisa. Jambo hili linafanya jamii kubwa kukosa habari muhimu zinazohusu Taifa letu. Mfano katika Wilaya ya Liwale Mkoa wa Lindi redio hii haipatikani kabisa. Nimeliuliza jambo mara nyingi bila majibu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mchakato wa kutafuta vazi la Taifa. Je, mchakato huu umefikia wapi? Hata hivyo yako mavazi yanayovaliwa hapa nchini hasa na wanawake wakati wakiwa kwenye sherehe mbalimbali. Je, hakuna sheria inayokataza mavazi hayo? Hapa nazungumzia yale mavazi ya nusu uchi yanayoacha maungo wazi.

Mheshimiwa Spika, ziko nyimbo zinazoimbwa na wasanii nyimbo hizo, hufungiwa baada ya wimbo husika kutoka je, hakuna sheria inayokataza wimbo kabla ya kutoka kupitiwa kwanza maudhui yake, kwani kufungia wimbo ambao umeshatoka haisaidii sana kwani tayari huwa umeshaingia kwenye mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ni moja ya tunu ya Taifa letu; kwa nini basi Wizara haina mpango mkakati wa kukikuza Kiswahili ambacho sasa kimeanza kuharibiwa na vyombo vyetu vya habari, viongozi wa kisiasa na wasanii mbalimbali kwa kuchanganya na lugha nyingine kama vile kiingereza (KISWKINGE) jambo hili linaharibu lugha yetu ya Kiswahili, lakini pia yako magazeti yanashindwa kuandika Kiswahili fasaha. Imefika sasa kuwa na Chuo cha kufundisha Kiswahili na kutungwa kwa sheria ya watumishi wote wa vyombo vya habari na wasanii kupitia kwenye Chuo hicho cha Kiswahili ili tunu ya Taifa iweze kuhifadhiwa. Pia Chuo cha Sanaa Bagamoyo kipewe fedha za kutosha na kujengewa uwezo na miundombinu wezeshi. Vilevile chuo hiki kipewe pia jukumu la kusomesha lugha ya kisiasa, sambamba na somo la kukuza uzalendo.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, kwa nini timu ya hamasa ya kui-*support* timu ya Taifa iliundwa na Wanasiasa, Mwenyekiti wake akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam? Suala hili linagawa watu kwa kuwa siyo watu wote ni wana CCM. Binafsi sikuunga mkono kwani ilikuwa *movement* za kisiasa, tuache kuingiza timu zetu katika siasa, uzalendo siyo kampeni ni hiari ya watu kupenda nchi yao. Hii ni aina nyingine ya siasa kwenye Wizara hii, wote tunajua mchakato na sababu za uzalendo.

Mheshimiwa Spika, upungufu katika Sheria ya Huduma za Habari kama ilivyothibitisha Mahakama ya Afrika Mashariki *(EAC),* sheria hii irudishwe mara moja na kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, *TBC* kuendelea kutumika kama chombo cha *propaganda* cha CCM. Ni aibu sana kwa Nchi

yetu. Rejea vipindi mbalimbali kwenye *TBC,* swali, je, hii ni *TV* ya Chama? Mbona kazi za vyama vingine hazionyeshwi? Kuweni wazalendo tuondoe aibu hii kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni lini Bunge litaanza kuoneshwa live. Niishauri Wizara kuja na mapendekezo ya kurudisha *live broadcasting* kwa kuwa ni pesa ya wapigakura. Je, ni sahihi kuwanyima haki ya kujua kinachojadiliwa na kuamuliwa na wawakilishi wao?

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya *Olympic*; nashauri tuwaandae vijana katika michezo mingine kama kurusha tufe, mishale na hata kuruka kwa kuwa tumeshindwa kufanya vizuri katika mpira na kukimbia, hivyo hatuna budi kuangalia nyanja nyingine.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa na mchango wake mkubwa katika kuinua Sekta za Michezo, Sanaa na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara na Viongozi wa Wizara kwa kazi kubwa na ya uzalendo mkubwa katika kuzisimamia sekta zote za Wizara na kufikia hatua nzuri ya mategemeo kwa Taifa na wananchi. Napenda kuwatia moyo waendelee na juhudi hizo wanazozifanya, michezo na sanaa imekua na imeleta sifa kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iendelee kuendeleza vipaji vya wanamichezo pamoja na wasanii wetu sambamba na kuvumbua vipaji vipya. Serikali iendelee kuwatambua na kuwaenzi wasanii na wanamichezo kwa mchango wao mkubwa walioutoa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia vyombo na Taasisi zake zinazohusika na kutoa elimu ya maadili, viendelee kutoa elimu juu maadili mema kwa wasanii, waigizaji na wanamichezo ili waendelee kuwa kioo kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili, Serikali na Wizara kwa ujumla naipongeza kwa kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili; lugha yetu hii imezidi kuzungumzwa duniani. Hivyo, nashauri juhudi hizo za kukiendeleza Kiswahili ziendelee kwa lengo la kukiongeza nguvu duniani kote, kuitangaza nchi yetu kupitia lugha yetu hiyo ya Kiswahili, kudumisha utamaduni pamoja na kuongeza soko la ajira kwa wataalam na watumiaji wa Kiswahili hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, michezo ya zamani ambayo yana faida na mchango kwa Taifa na wanamichezo wenyewe ambayo imepotea au haina nguvu ifufuliwe na kupewa msukumo. Nashauri Serikali iongeze fedha kwa Wizara hii ili kukamilisha majukumu yao. Mwisho Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara nawapongeza kwa kazi nzuri ya kuendeleza kazi zote zilizomo ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, nimeona ni vema nami nikachangia mchango wangu mdogo katika Wizara hii ambayo inasimamia utamaduni wetu, sanaa na michezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa na Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Naibu wake, Mheshimiwa Juliana Shoza, Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizi nzuri kwa Wizara hii bado kuna changamoto ya usikivu wa *TBC* Taifa, hususani katika Jimbo langu la Itigi na hasa katika Mji wa Itigi. Itigi kuna redio ya Kanisa Katoliki (Redio Mwangaza) ambao wamefunga mtambo wao ambapo umezuia kabisa matangazo ya *TBC* Taifa. Je, ni lini sasa *TBC* itasikika Itigi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na majibu ya Serikali mara kwa mara kuwa katika bajeti ya nyuma yaani miaka iliyopita kuwa Serikali itafunga mtambo Itigi ili kuifanya *TBC*

Taifa isikike. Naomba sasa katika bajeti hii Serikali kwa maana ya Wizara hii sasa ifunge mtambo Itigi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza hapa Bungeni kwamba *local channels* za *TV* zitaoneshwa kwenye ving'amuzi bure bila kulipia lakini hadi sasa zoezi hilo limeshindikana. Serikali haioni kwamba huku ni kuwanyima wananchi wa Tanzania kupata habari? Hivyo, ni vyema Serikali ikaweka msisitizo kuhusu jambo hili ambalo ni haki ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ijenge vizuri uwanja wa mpira uliopo Mji mdogo wa Mlowo ambao ulizinduliwa na Mwenge tarehe 2 Aprili, 2019. Uwanja huu ujengwe vizuri ili kuruhusu michezo mingine iwe na miundombinu mizuri. Mfano michezo ya mpira wa pete, *volleyball* na michezo mingine.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mpira wa miguu nchini, Serikali iangalie namna ya kuanzisha *academy* katika kanda mbalimbali nchini. Leo nchi nyingi zilizoendelea duniani kisoka zilianza na *academy* na sasa zimefikia hatua kubwa ya kisoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuongelea kuhusu viwanja vya michezo. Kulingana na changamoto za viwanja vingi nchini kuwa chakavu, jambo hili linatakiwa kupewa kipaumbele na Wizara ili kuweza kukuza michezo katika ngazi mbalimbali nchini na pia italeta chachu kwa vijana wenye vipaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu kuboresha usikivu. Kwa sasa kuna shida kubwa ya usikivu wa chaneli zetu, hasa kwenye maeneo ya mipakani. Naomba maboresho yafanyike ili kuwasaidia wananchi wanaoishi maeneo ya

mipakani kupata habari za taifa lao badala ya kupata habari za nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, tatu ni usalama wa waandishi wa habari na wamiliki wa vyombo vya habari. Kwa sasa kumekuwa na vitisho na watu kupotea, je, Wizara ina mkakati gani wa kuwalinda kwani kuwepo kwa waandishi wa habari ni muhimu sana katika taifa lolote lile.

Mheshimiwa Spika, nne, vazi la taifa. Mpaka sasa vazi la taifa halijajulikana na imekuwa ni malalamiko ya muda mrefu kwa wananchi katika ngazi mbalimbali nchini kuhusu vazi hili. Je, Wizara mpaka sasa imefikia hatua gani kuhusu vazi la taifa?

Mheshimiwa Spika, tano, chuo kikuu kwa ajili ya walimu wa michezo. Nashauri kijengwe chuo kikuu cha walimu wa michezo ili kuweza kukuza michezo nchini kwani kwa sasa kuna uhaba wa walimu bora wa michezo. Hii pia itasaidia kuinua michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, sita, wanamichezo wanaofanya vizuri ndani na nje ya nchi. Kumekuwa na malalamiko kwa kiasi wanachopewa baada ya ushindi kwamba wanapewa kiasi kidogo sana ambacho hakiendani na kiasi walichopata, jambo ambalo linapunguza morali kwa wanamichezo wetu.

Mheshimiwa Spika, saba, nashauri Wizara iweke utaratibu mzuri wa kuibua vipaji mbalimbali kuanzia huko wilayani na mikoani ndani ya nchi yetu. Ni imani yangu kuwa wilayani na mikoani kuna vipaji vingi.

Mheshimiwa Spika, nane, kufungia magazeti. Suala hili limekuwa likileta sura mbaya kwa mataifa mengine yanayotuzunguka. Suala la kufungia magazeti linaathiri wamiliki, waajiriwa pamoja na wananchi wanaopata habari ambayo ni haki yao.

**MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu,

Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuleta hotuba nzuri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kampeni ya Uzalendo yenye kaulimbiu "Kiswahili Utashi Wetu, Uhai Wetu" imenigusa sana. Umuhimju wa lugha unaonekana siku zote katika kufikisha taarifa sahihi kwa walengwa. Lugha isipoeleweka, hata ujumbe unaotumwa haufiki vizuri na wakati mwingine inawezekana kusababisha madhara.

Mheshimiwa Spika, watoto wadogo ni wepesi kujifunza lugha, wakifundishwa lugha vizuri wanadaka mafundisho haraka na kutumia mafundisho hayo katika maisha yao ya kawaida. Ili kuwajengea uwezo watoto wetu ni lazima lugha fasaha ya Kiswahili itumike katika mafundisho, mihadhara, makongamano na kadhalika. Kuna neno kama "NANILII" ambapo vijana wengi hata wa shule za sekondari na vyuo vikuu wanalitumia sana, mimi silipendi. Katika kuhamasisha uzalendo wetu, ni muhimu sana kutumia lugha fasaha ya Kiswahili kutoa mafunzo kwa vijana wetu katika shule, vyuo na wahariri wa magazeti na kadhalika ili kupeleka ujumbe sahihi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu. Bunge hili kupita mjadala wake katika bajeti ya Makamu wa Rais limedhihirisha kwamba kuna haja ya kutoa elimu ya Muungano kwa watu wote (elimu kwa wanafunzi wadogo na watu wazima) ili dhana ya Muungano ieleweke vizuri kwa watu wote. Nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara inayoshughulikia Muungano ili kuratibu mafunzo ya uzalendo, ukiwemo Muungano wetu kwa watu wote. Katika hili, lugha fasaha ya Kiswahili ni lazima itumike vizuri, vyombo vyote vya habari vitakavyoshiriki vielekezwe kutumia Kiswahili fasaha katika kufikisha ujumbe kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii na nampongeza sana mtoa hoja, Mheshimiwa

Waziri kwa hotuba nzuri na wasilisho lililojaa weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Timu yetu ya Taifa kwa kuweka historia ya kufuzu Mashindano ya Mataifa ya Afrika maarufu kama *AFCON* yatakayofanyika nchini Misri Juni, 2019. Ni matumaini yangu na Watanzania baada ya kusubiri kwa miaka 39, *TTF* watajipanga vilivyo katika kuandaa timu yetu ili iweze kufanya vizuri katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa viwanja vyetu hususan vya kuchezea soka uangaliwe kwa karibu na mamlaka husika. Kwa mfano, kwenye mashindano ya ligi kuu viwanja vingi hususan vya mikoani vipo katika hali mbaya kiasi kiasi cha kuhatarisha usalama wa wachezaji wenyewe. Naomba wasimamizi wa mpira nchini *(TFF)* waweke utaratibu madhubuti timu zinazocheza katika ligi kuu viwanja vyao vikaguliwe na wasiokidhi viwango walazimishwe kucheza kwenye viwanja vya jirani vyenye ubora.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa inasifika duniani kwenye mchezo wa riadha. Siyo siri wanariadha hawa wengi chimbuko lao lilikuwa Wilayani Mbulu, Mkoani Manyara. Umefika wakati sasa Wizara ikaona haja na hoja ya kujenga Chuo cha Michezo Wilayani Mbulu ili kulea vipaji vya vijana ili wengi wapate fursa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu kwa usimamizi mzuri wa kazi za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuchangia kwa maandishi na nianze kwenye michezo. Pamoja na juhudi za kusimamia michezo, kuna haja ya kuongeza bidii kwenye michezo mingine ikiwa ni pamoja na riadha, mpira wa pete, gofu na mengineyo badala ya kuweka jicho letu kwenye

mpira wa miguu ambako bado tunahitaji kuweka juhudi na mikakati madhubuti ili vijana wetu waweze kucheza vizuri na pia miongoni mwao watokee makocha badala ya kutegemea makocha kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuwe na utaratibu wa kuimarisha viwanja vya michezo badala ya kuwa na viwanja vingi vya mpira wa miguu wakati kuna vipaji vya aina mbalimbali vya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie au chombo maalum kiwepo kwa ajili ya kufuatilia watangazaji, kwanza katika maslahi yao, vifaa vya uhakika vya utangazaji na mwisho kuangalia au kuchuja waandishi/watangazaji ambao hawana maudhui ya utangazaji na matamshi sahihi na fasaha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, taasisi zote zilizoko katika Wizara na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, sekta ya michezo na burudani, iwapo itasimamiwa vizuri kwa kutenga bajeti ya kutosha itasaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiwango kikubwa lakini pia michezo inaitangaza nchi kiutalii duniani.

Mheshiimiwa Spika, kwa mfano, michezo kama mpira wa miguu, riadha, wasanii wa muziki, wasanii wa vichekesho *(stand up comedy),* ngoma za asili na wasanii wa maigizo (sinema); hawa wote ni chanzo kikubwa cha mapato yao wenyewe na hata Serikali inaweza kupata kodi yake kwa kiwango kikubwa iwapo kutakuwa na uwekezaji wa kisasa kwa sekta hii. Naiomba Serikali iwekeze kwa kiwango cha kutosha katika Sekta ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kidogo kwenye Wizara hii muhimu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba wasanii wa Tanzania wanapata shida sana kutokana na usimamizi mbaya kwa maana ya ulinzi wa kazi za wasanii. Je Serikali haioni umuhimu wa kuileta kwenye Bunge lako Tukufu Sheria ya Hati Miliki na Hati Shiriti, Na.7 ili tuipitie upya na kuifanyia marekebisho? Kwani sheria hii imeshapitwa sana na wakati na inaonekana kuwa ndiyo chanzo cha wasanii wa Tanzania kuwa maskini na wengine kupata *stress* (msongo wa mawazo) na kujikuta wanajingiza kwenye matumizi ya madawa ya kulevya na unywaji wa pombe kupitiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimishaji wa sanaa. Serikali haioni ikirasimisha rasmi wasanii itaweka mambo mengi kuwa rasmi na kusaidia Serikali kujua kipato cha kila msanii anachoingiza kupitia sanaa na kuweza kukusanya kodi yake vizuri tofauti na sasa ambapo vipato vya wasanii havijulikani na kusababisha Serikali kupoteza pesa nyingi kupitia kodi.

Mheshimiwa Spika, tumeona Serikali ikihangaika na mikataba mibovu waliyoingia wasanii na kunyonywa kwa kiwango cha ajabu na cha kusikitisha sana lakini mikataba kati ya wasanii na mashirika mbalimbali ingekuwa wazi ingesaidia sana mbali ya Serikali kupata kodi pia wasanii wangepata nafasi ya kuweza kukua zaidi na pia ingepelekea kupata ushauri mbalimbali juu ya kuwekeza (kuji-*brand)* zaidi ili kuwafanya wawe *professional* zaidi na kuepuka hali za wasanii wengi wa Tanzania ambao wengi wao wanakufa maskini kutokana na kutokuwa na msaada wowote wa kifedha na ushauri na mwisho wao kuwa mbaya na wa kusikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iache kuwatumia wasanii kisiasa na ijikite kuwasaidia wasanii wawe *neutral* na kufanya shughuli zao za kitaifa na siyo kichama zaidi. Kwa kuwatumia wasanii kisiasa inawaumiza sana kwenye jamii

kwani siyo kila shabiki wa muziki anaipenda CCM, hivyo kupelekea wale wasioikubali CCM kutowa-*support* kwa sababu wanatumiwa na CCM na mwisho wao kuwa mbaya, mfano, msanii Marlaw.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze bajeti ya BASATA maaana hawa ndiyo walezi wa sanaa ya Tanzania na pia ndio kama baba na mama wa sanaa ya Tanzania. Bajeti ya shilingi milioni 22 kwa mwaka ni ndogo sana na haitoshi kuwawezesha kuwafikia wasanii wote nchi nzima na kuwaelimisha na kuwasimamia kama majukumu yao yanavyojieleza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia BASATA waache kufungia hovyo kazi za wasanii bila kufuata sheria kwani hakuna sheria inayoruhusu BASATA kufungia kazi za wasanii wa Tanzania. Kwa kufingia hovyo kazi za wasanii BASATA wanavunja sheria na wasipoangalia ipo siku watajikuta Mahakamani wakishtakiwa na wasanii wanaojielewa na itaharibu sana mahusiano kati ya wasanii na BASATA kitu ambacho kitadidimiza zaidi ukuaji wa sanaa yetu ambayo inategemea sana mahusiano mazuri kati ya wasanii na BASATA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke BASATA ni mlezi wa sanaa ya Tanzania na siyo Mahakama ya kuwasulubu wasanii wa Tanzania. Naomba sana waitumie vema nafasi na heshima ya kuwa mlezi wa sanaa ya Tanzania na washirikiane vizuri na wasanii wa Tanzania kwa maslahi mapana zaidi ya sanaa ya Tanzania, Taifa letu na kizazi hiki na kizazi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, michezo ya ngumi. Michezo hii ni muhimu sana kwa uchumi wa vijana wa Tanzania lakini kuna shida ya mapromota wengi wanatumia nafasi zao vibaya kwa kupeleka wachezaji nje ya nchi na kuingia mikataba mibovu. Hata hivyo, naishukuru Serikali kwa kuunda Kamati ya Ngumi ambayo kwa muda mfupi imeleta mafanikio kuonyesha mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Spika, ulingo. Tunaomba Serikali inunue ulingo mwingine ili kuongeza upana wa matumizi ya ulingo kwani kwa sasa upo mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, mabondia wa kike. Tunaomba Serikali isaidie mabondia wa kike katika kuwasimamia kupata haki zao za kikatiba.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ina wasanii wengi mno, lakini wasanii wale hawajulikani kwenye tasnia ya vyombo vya habari na ukiangalia Serikali pamoja na kupoteza mapato mengi ya kuchangia Taifa letu unakuta tunazikosa, lakini pia wasanii hawa kupoteza taaluma yao na mwishowe hujiingiza kwenye mambo ambayo hawana fani nayo na kupoteza mwelekeo wa maisha yao. Kwa hiyo niishauri Serikali yangu tuwawekee miundombinu rafiki ili tusipoteze vipaji vya wasanii hawa kwani mwisho wa siku Taifa letu litaongeza mapato kupitia wasanii wetu hasa wasanii wa Lushoto.

Mheshimiwa Spika, pia Wilaya ya Lushoto ina vijana wengi wana vipaji vya mchezo hasa mpira wa mguu, lakini pia kuna changamoto kubwa ya kiwanja cha mchezo. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu itujengee uwanja wa michezo katika Jimbo la Lushoto ili tuweze kuwapata kina Mesi kutoka Lushoto. Pamoja na hayo niishauri Serikali yangu hasa Waziri mwenye dhamana, michezo ifundishwe mashuleni ili kubaini vipaji toka mashuleni.

Mheshimiwa Spika, najua upo UMISHUMTA na UMISETA, hii haitoshi, kuwe na ratiba ya vipindi katika shule zetu. Pia, niiombe Serikali yangu hasa Waziri mwenye dhamana wakati wanawatafuta wachezaji hasa hawa wa chini ya miaka 17 waende mpaka wilayani kwani kuna wachezaji wazuri mno wanakosa tu kuonekana katika vyombo au hakuna wa kuwasemea.

Mheshimiwa Spika, Redio ya Taifa ni shida katika Wilaya ya Lushoto. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu itujengee mnara wa *TBC 2* ili wananchi wa Lushoto waweze kupata mawasiliano ya matangazo ya habari kuliko ilivyokuwa sasa. *Booster* imefungwa kwenye mnara wa redio, kwa hiyo kusababisha usikivu wa *TBC* kuwa mdogo yaani usikivu hauendi mbali na kama tunavyojua *TBC* ndio redio yenye uhakika wa taarifa zake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nisisitize kuwekewa mnara wa *TBC* ni muhimu mno hasa kwa maslahi ya wananchi wa Lushoto.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pili, nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutayarisha na kuiwasilisha kwa ufasaha na kwa utaalam.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, michezo; napenda kuipongeza Serikali yetu kwa hatua inayochukua katika kuendeleza michezo. Michezo ni miongoni mwa mambo ambayo yanaonesha utambulisho wa nchi. Naipongeza Serikali kwa kuilinda na kuiwezesha timu yetu ya Taifa mpaka kufika katika hatua ya *AFCON.*

Mheshimiwa Spika, michezo ni hasara, Serikali inabidi iongeze juhudi ya kuisaidia timu yetu bila ya kujali hasara, bila ya kuisaidia hatuwezi kufika hatua ambapo tunaikusudia. Pia naishauri Wizara ichukue hadhari na iwe makini katika uchaguzi/uteuzi wa wachezaji na viongozi wa kuendeleza na kuendesha timu hiyo. Uchaguzi wa sasa hauridhishi hata kidogo kwa kuwa timu hii ni ya Taifa la Tanzania (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ni vyema uchaguzi wa wachezaji uzingatie pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nalipongeza sana Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC)* na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri ya kurusha na kutangaza habari kwa Watanzania.

Pamoja na kazi nzuri wanayoifanya watangazaji, wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(1) Uchakavu wa mitambo ya *TBC* mingi ni ya miaka ya zamani. Naishauri Serikali inunue mitambo mipya na ya kisasa ili *TBC 1* iweze kuonekana vizuri nchi nzima na *TBC* Taifa *(Radio)* isikike vizuri nchini kote.

(2) Maslahi duni ya wafanyakazi wa *TBC* husababisha wafanyakazi kuhamia vyombo vingine binafsi.

(3) Magari yamechakaa hasa kwa *TBC* Kanda ya Kati na ni machache na hivyo kuwafanya wasitembelee maeneo mengine ili kuchukua habari. Habari nyingi zinakuwa za mjini tu badala ya vijijini ambapo wapo wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waandishi wa Habari ni wachache, habari zinazoandikwa nyingi ni za mijini tu siyo vijijini. Naishauri Serikali iajiri Waandishi wa Habari kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna migogoro mingi ya vilabu vya mpira wa miguu: Je, nini chanzo cha migogoro hiyo? Pili, Serikali inasaidiaje kutatua migogoro hiyo ili kuboresha hali ya soka hapa Tanzania? Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia *Serengeti Boys* ili wafanye vizuri katika mashindano yanayoendelea hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Michezo, kama tujuavyo ni afya, ni furaha na yanaleta upendo. Duniani pote magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu la kupanda na kushuka, ugonjwa wa kisukari na magonjwa ya moyo huepukika mapema kwa kufanya mazoezi, lakini hapa Tanzania Halmashauri nyingi hazina viwanja vya michezo na pia barabara zetu sio rafiki kwa watu kufanyia mazoezi, hakuna sehemu za watembea kwa miguu.

Je, kwa nini Serikali isikae chini ili Wizara hii na Wizara ya Miundombinu wakaweka mikakati iwe ni lazima wanapojenga barabara wahakikishe kuwepo na sehemu za wapita kwa miguu ili iwawezeshe wananchi kutembea?

Mheshimiwa Spika, vile vile ni vizuri katika sehemu za kazi pawepo na sehemu za kuogea ili wafanyakazi watembee kwenda kazini, wakifika ofisini wanaoga.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyote vilivyotekwa na CCM katika kila Halmashauri virudishwe kwenye Halmashauri kwa kuwa vilikuwa ni vya Umma na wananchi wote wavitumie kwa ajili ya mazoezi.

Je, Serikali ina mpango gani kwa kukifufua kiwanja wa *King Memorial* kilichopo Mkoani Kilimanjaro katika Manispaa ya Moshi ili kianze kutumika? Ukizingatia kiwanja kile kina michezo zaidi ya saba lakini kipo tu pale wananchi wanapanda maharage wakati kiwanja kipo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na mchakato wa ku-*design* vazi la Taifa na fedha zilitumika kwa ajili ya vazi hilo, lakini hadi leo hatujapata mrejesho, zoezi hili lilifikia wapi? Je, ni lini mchakato wa vazi la Taifa utakamilika?

Mheshimiwa Spika, ni haki ya wananchi kupata habari lakini ni jambo la kusikitisha vyombo vya habari havipo

huru na vimebanwa sana. *Local channel* za *television* tulielezwa zilitakiwa ziwe bure, lakini cha kusikitisha ni chombo kimoja tu cha *TBC* ndicho kinachotoa matangazo tena kwa upendeleo, hawatoi habari zote. Mfano, hata hotuba za Upinzani Bungeni hazijawahi kutangazwa na *TBC*.

Mheshimiwa Spika, magazeti hayana uhuru. Yakiandika ukweli huwa yanapewa adhabu ya kufungiwa. Je, huu ndiyo uhuru wa habari mnaoutangaza?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kwetu sote. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuona umuhimu wa Wizara hii na kumteua Waziri na Naibu Waziri walio waelewa na makini sana kwenye kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Juliana Shonza, Katibu Mkuu Ndugu Susan Mlawa, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholaus B. William, Mkurugenzi wa Habari Dkt. Ryoba na Viongozi wote Wakuu kwenye Idara nyingine ikiwemo Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nakubali kabisa kwamba kuna mambo ambayo yanatendeka, yanabadilisha utamaduni wetu bila hiari yetu Watanzania, kutokana na uwepo wa mitandao kama luninga, simu na kadhalika. Baadhi ya mambo hayo ni mavazi yasiyo ya heshima, maigizo ya filamu za nje na mengineyo. Je, Serikali ina mpango gani kukomesha vituko hivyo katika hatua za awali kama kwenye Shule za Msingi?

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Idara ya Habari. Tatizo langu ni mtiririko wa taarifa ya habari asubuhi. Je, ni lini *TBC* itatangaza habari mfululizo bila kuingiliwa na majadiliano yoyote ili tuwahi kazini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Inaumiza sana kuona jinsi ambavyo hatujaweza kuingia kwenye kiwango cha juu cha Kimataifa kwenye soka. Nataka ieleweke kuwa,

maandalizi yetu ya zimamoto hayatatufikisha mbali. Kila Wizara iwe na dawati la michezo mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wachezaji waandaliwe toka utotoni kwa lishe bora, elimu na mazoezi. Makuzi ya wanamichezo yasimamiwe toka awali na wazazi na waalimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja na ninaomba kwenye miaka ijayo waongezewe fedha zaidi bila ukomo.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, *Olympic* ni maarufu sana duniani kwa sasa. Ni michezo inayoendeshwa kwa ukwasi mkubwa wa fedha na hivyo Mataifa yanayoandaa yamekuwa yakijizolea mamilioni na mabilioni ya fedha za kigeni. Kwa nini Serikali haifikirii kujenga kituo cha michezo ya *Olympic (Olympic Centre)* katika moja ya fukwe zetu tulizojaliwa na Mungu kama vile ufukwe wa Kijiweni uliopo Mchinga Lindi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ioneshe nia hiyo kwanza, kisha itafute wachezaji ambao wataingia ubia na Serikali katika kufanikisha jambo hilo muhimu kwa uchumi na maendeleo ya Sekta ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni *TBC* kugeuzwa kuwa chombo cha chama badala ya kuwa chombo cha habari cha Taifa. Imefahamika kuwa duniani kote *Television* ya Taifa inafanya kazi kwa karibu na Serikali iliyopo madarakani, lakini *TBC* inavuka mipaka na hivyo kuondoa kabisa ladha ya kuendelea kuitazama na hamu ya kuipenda. Jambo hili halina afya njema kwa mustakabali wa Taifa linalokusudia kupiga hatua ya maendeleo na kufikia uchumi wa kati. Ujumbe wangu, *TBC* iache kushabikia siasa za mrengo mmoja pekee, inapoteza watazamaji na wasikilizaji wake kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni wazo la Serikali kuandaa mashindano maalum ya Insha yanayohusu Lugha

ya Kiswahili ili kuongeza hamasa na hulka ya vijana wetu kuipenda, kuithamini na kuienzi lugha yetu hii. Mheshimiwa Waziri, mashindano haya yanaweza kuanzia ngazi za Shule za Msingi hadi Chuo Kikuu. Ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi nyingi sana kwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Juliana Shonza na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuinua vipaji na kuendeleza soka la Tanzania pamoja hotuba yao iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri yaliyoorodheshwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba nipatiwe ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ripoti nyingi sana za mchakato wa Vazi la Taifa na tumekuwa na kiu kubwa sana kuona mchakato huo unafika mwisho ili Tanzania itambulike kwa vazi lake kama zilivyo nchi nyingine. Je, ni lini sasa Serikali itahitimisha hili jambo zuri?

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wa kike wamekuwa wakishiriki Mashindano ya Ligi (soka) Timu za Wanawake, wakiwa na changamoto nyingi sana kiasi kwamba hata ushiriki wao umekuwa mgumu. Nilitegemea ligi hii ingetumika hata kupata vipaji kwa mabinti zetu ili waweze kushiriki katika Timu ya Taifa ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua mkakati wa Serikali wa kusaidia hizi Timu ziweze kushirihiki ligi kuu, kwa sababu wanaishi katika mazingira magumu mpaka wanadhalilishwa kwa kutembeza mno bakuli.

Mheshimiwa Spika, nashirikiana na wote walioipongeza *TBC* kwa kazi nzuri sana. Nilikuwa naiomba Serikali itoe kipaumbele kuongeza bajeti ili waboreshe mitambo, pia usikivu uwepo katika maeneo yote kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itenge fungu la fedha katika bajeti hii na ifike kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zetu nchini waweze kuweka utaratibu maalum wa kutoa vibali vya ujenzi za kumbi za starehe kwamba zisiwe karibu na makazi ya watu ili kuepusha usumbufu kutokana na kelele zinazotokana na shughuli mbalimbali zinazofanyika katika kumbi hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda sanaa zetu, nashauri Serikali iweke utaratibu wa kisheria utakaowezesha vituo vyote vya *Radio* na *Television* nchini kupiga muziki wa wasanii wa nyumbani kwa asilimia 70 ili pia kukuza soko la bidhaa za wasanii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali irejeshe viwanja vya wazi ambavyo vilikuwa vikitumika kwa michezo mbalimbali na vimebadilishwa matumizi bila kufuata utaratibu maalum.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutunga Sheria kali ambayo itakataza wasanii wa muziki na maigizo hususan wa kike kuvaa nguo au mavazi ambayo yanakiuka maadili na utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwe na vazi rasmi la Taifa ambalo litamtambulisha Mtanzania yeyote yule awapo nje ya nchi yetu na popote pale atakapokuwa hivyo jitihada za makusudi zifanyile ili kufanikisha suala hili.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na mafanikio yasiyo endelevu kwenye Sekta ya Michezo, hii ni kwa sababu wanamichezo wetu wanakosa misingi imara ya kitaaluma kimichezo. Msingi wa kitaaluma unaweza kupatikana vizuri zaidi kupitia shule zetu kwa ngazi mbalimbali kuanzia Shule za Chekechea na kuendelea. Kikwazo kikubwa kimekuwa ni kutokuwa na Walimu ambao ni Wataalam wa Michezo na Miundombinu ya kutumia kushiriki michezo, hali ambayo imekuwa inaathiri sana vipaji vya wanamichezo.

Mheshimiwa Spika, hivyo nashauri, michezo iwe ni moja ya masomo katika mitaala ya shule zetu hali ambayo itafanya watoto wote wenye vipaji mbalimbali waweze kuviendeleza. Kuwe na mkakati maalum wa kuandaa walimu watakaotumika kuwafunza vijana wetu na kukuza vipaji mbalimbali kwenye shule, vilabu vya michezo na kadhalika. Kwa mfano, timu zetu za mpira wa miguu hivi sasa zinafundishwa na walimu kutoka nje na hakuna idadi kubwa ya walimu wa Kitanzania wanaofundisha soka nje ya nchi.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo: vyombo vya habari siyo huru kabisa, haiwezi kufanya kazi yake ipasavyo. Matokeo yake Serikali haiwezi kujisahihisha na kupata maendeleo, haiwezi kujua ni wapi imekosea. Naiomba Serikali iangalie upya Sheria hiyo ya Vyombo vya Habari, kuvibaini ili visifanye kazi zake inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii iangalie ni namna gani inatoa elimu kwa wananchi juu ya kudumisha maadili mema. Hata walimu mashuleni, pia wazazi wafundishe maadili kwa watoto wao maana kuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili kwa watoto na vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mila na desturi katika makabila mbalimbali ni nzuri. Hivyo, nashauri makabila wahamasishwe kudumisha mila na desturi ambazo ni nzuri. Mfano, heshima kwa wakubwa kwa kuwapokea wakubwa mizigo au kuwaachia viti maeneo ya mikusanyiko.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye tathimini juu kutoangalia Bunge, kwa sababu watu wengi wanalalamika, hawaelewi nini kinaendelea Bungeni na kwamba hawaelewi kama wawakilishi wao wanawawakilisha vyema au la.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumemaliza wachangiaji, sasa nimkaribishe Naibu Waziri, Mheshimiwa Juliana Shonza, una dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema na uzima kuweza kufika siku ya leo. Kipekee kabisa, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, kwa miongozo mikubwa ambayo amekuwa akinipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa michango yake mizuri ambayo imekuwa ikitoa kwa Wizara yangu. Vilevile nishukuru pia michango yote ambayo imeweza kutolewa na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimepewa muda mchache, nitaomba nijielekeze katika masuala machache, hususan nikianza na hoja ambazo zimeibuliwa na Kamati. Kuna hoja ambayo imetolewa na Kamati ya namna gani sisi kama Wizara tutaboresha suala zima la Chaneli yetu ya Utalii ambayo tumeianzisha mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba sisi kama Wizara tunayo mipango mizuri kabisa ya kuhakikisha kwamba tunaboresha Chaneli yetu hii ya Utalii. Kwa sababu ndiyo tunaanza mwaka wa fedha wa 2019/2020 tumejipanga

kushirikiana na wadau wetu kuhakikisha kwamba Chaneli hii ya Utalii inafanyiwa maboresho makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Wajumbe wa Kamati kwamba tunayo mipango mizuri sana ya kuhakikisha kwamba Chaneli hii ya Utalii kwanza inaboreshwa lakini vilevile itakuwa ni chaneli ambayo inaweza kusikika kimataifa. Kwa sababu lengo ni kuhakikisha chaneli hii siyo kwamba inasikika tu ndani ya nchi lakini pia iweze kusikika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mipango ambayo tunayo mpaka sasa hivi tayari Chaneli hii ya Utalii imekwishaanza kuoneshwa kwenye chaneli mbalimbali za kimataifa ikiwepo kwenye chaneli ya *DSTV,* Zuku na kwenye chaneli zote ambazo zinatumia mfumo wa *satellite.* Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa kufanya hivyo itakuwa ni njia mojawapo ya kuweza kusaidia Chaneli yetu ya Utali iweze kutazamwa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, Chaneli yetu hii ya Utalii kwa sababu ni chaneli ambayo iko ndani ya nchi lakini tunajua kwamba kimataifa huko tunazo chaneli nyingi sana ambazo zimebobea katika masuala haya ya utalii, mpango wetu wa kwanza ni kuhakikisha kwamba tunashirikiana na makampuni mbalimbali ya kimataifa ambayo yamebobea kwenye masuala haya ya utalii kuhakikisha na sisi kama nchi Chaneli yetu ya Utalii inaweza kutazamwa kimataifa. Kwa hiyo, huo mpango tunao na tunaamini kabisa kwamba muda mfupi na ndani ya mwaka wa fedha huu ambao tunauanza wa 2019/2020, mazungumzo hayo yatakuwa tayari yameshakamilika na Chaneli yetu ya Utalii itaanza kuonekana katika hizo chaneli za kimataifa ikiwemo Chaneli ya *National Geographic.*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ya Kamati ambayo imezungumza kuhusu kuboreshwa Shirika letu la Magazeti (*TSN).* Nikiri kwamba kumekuwa na changamoto ya muda mrefu hususan katika suala zima la mapato, kwamba mapato mengi hususani suala zima la matangazo katika magazeti haya ya Serikali yamekuwa yakishuka.

Changamoto hii ilitokana na kwamba kumekuepo na ukuaji mkubwa sana wa kasi ya teknolojia ambayo kwa namna moja ama nyingine iliathiri upatikanaji wa matangazo katika magazeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba sisi kama Wizara tumeliona hilo na kunapokuwa na changamoto yoyote ile lazima tuangalie namna gani ambavyo tutaitumia hiyo changamoto kama fursa. Sisi kama Wizara kwa kushirikiana na *TSN* tumekuja na mpango wa kuhakikisha kwamba tunaweza kukabiliana na hiyo changamoto, kwa sababu suala la ukuaji wa teknolojia, pamoja na kwamba inaweza kuwa changamoto kwa namna moja lakini vilevile ni fursa ambayo naamini hata sisi tukiitumia inaweza kusaidia sana katika kuboresha haya Magazeti ya *TSN.*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba na sisi tunaanzisha chaneli yetu wenyewe ya kimtandao. Televisheni hiyo tayari imekwishaanzishwa ambayo inaitwa *Daily News Digitals.* Tunashukuru kwa sababu televisheni yetu hiyo ya mtandao inafanya kazi nzuri sana. Ndani ya muda mfupi mafanikio ni makubwa sana kwani watazamaji wameongezeka lakini vilevile imesaidia sana kuweza kuongeza mapato katika Taasisi yetu hii ya *TSN.*

Mheshimiwa Spika, iko hoja pia ya Kamati ambayo imezungumzwa kuhusu Serikali iangalie namna gani ya kuweza kuongeza fedha katika Chuo chetu cha TaSUBa kwa sababu kumekuwa pia kuna changamoto kwamba chuo kipo kwenye ukingo wa ufukwe wa bahari na mara kwa mara kunatokea mawimbi ambayo yanaathiri miundombinu ya chuo kile. Niseme kwamba ushauri ambao umetolewa na Kamati tumeupokea lakini kwa sababu ni suala la kushauriana na Wizara ya Fedha na uzuri wenzetu wa Wizara ya Fedha wako humu ndani, sisi kama Wizara tunaendelea na mashauriano kuhakikisha kwamba chuo chetu hiki ambacho kimsingi kimetunukiwa kuwa chuo cha ubora uliotukuka katika Afrika Mashariki kwa maana ya *center of excellence,* kuhakikisha kwamba Serikali inatenga pesa lakini kila mwaka

pesa zinatolewa. Hilo likifanyika tutaweza kumaliza changamoto mbalimbali ikiwemo hilo suala la kuweka fensi ili kuweza kuzuia bahari isiweze kuharibu miundombinu ya chuo vilevile kuhakikisha tunajenga na kuboresha madarasa pamoja na kumbi mbalimbali ambazo zipo kwenye hicho chuo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ambayo pia imetolewa kuhusiana na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering,* kwamba inakwenda kumaliza muda wake mwezi Agosti 2019, itasababisha Uwanja wetu wa Taifa utakosa mdhamini wa kuweza kuukarabati. Nikiri kwamba ni kweli, sisi kama Wizara tunatambua kwamba tuliingia mkataba na Jamhuri ya Watu wa China kupitia hiyo Kampuni ya *Beijing Construction Engineering* na unakwenda kumalizika Agosti, 2019.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie fursa hii kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi kama Wizara tupo kwenye mazungumzo na kampuni hii ili kuhakikisha tunauhuisha mkataba huu. Niseme kwamba mazungumzo yetu yamefika pazuri na tunaamini kwamba tutakapofikia mwafaka mkataba ule utaweza kuhusihwa ili kuhakikisha kwamba kampuni hii inaendelea kuhudumia Uwanja wetu wa Taifa katika masuala mbalimbali yakiwemo masuala ya umeme, maji pamoja na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hoja mbalimbali ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Kuna hoja ambayo imeibuliwa na Kamati, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Shangazi pamoja na Mheshimiwa Juma Nkamia kuhusiana na suala zima la kuboresha mitambo ya *TBC.* Ni kweli kwamba siku za nyuma tulikuwa tuna tatizo kubwa sana la uchakavu wa mitambo ya *TBC.* Nikiri kwamba Serikali ya Awamu ya Tano tangia ilipoingia madarakani tumeona bajeti ya uboreshaji wa Shirika letu la *TBC* ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Ukianza bajeti ambayo ilitolewa mwaka 2016/2017 ilikuwa Sh.1,000,000,000; mwaka 2017/2018 ikapanda ikawa Sh.3,000,000,000; na sasa hivi 2019/2020 imefika Sh.5,000,000,000. Sasa tunavyoingia kujadili bajeti

ya mwaka 2019/2020, bajeti kwa ajili ya kuboresha masuala yote yanayohusiana na *TBC* imefika Sh.5,000,000,000. Kwa hiyo, Serikali ina nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunaboresha mitambo. Hata ukienda kwenye ofisi ambazo ziko pale Mikocheni, Dar es Salaam imefungwa mitambo mipya kabisa ambayo inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, lengo la haya yote ni kuhakikisha kwamba Shirika letu la *TBC* kwa sababu kazi yake ni kuhabarisha umma, Watanzania waweze kupata habari ambazo ni za ukweli na za uhakika, tunataka shirika hili lifanye kazi yake kwa umakini ili Watanzania waweze kuhabarishwa. Yapo mambo mengi mazuri ambayo yametekelezwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mambo mazuri sana, ndiyo maana mimi nikisikia humu Bungeni Wabunge wanakuja na hoja kwamba kwa nini *TBC* inaonesha *Live* ziara za Mheshimiwa Rais, hilo suala mimi linanipa shida sana kwa sababu kwanza kile ni chombo cha umma lakini vilevile Mheshimiwa Rais anafanya kazi ya Watanzania, hafanyi kazi ya Chama cha Mapinduzi na anapokuwa kwenye ziara anagusa matatizo ya Watanzania wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tutakuwa ni mashahidi namna gani ambavyo kwenye ziara za Mheshimiwa Rais huko mikoani ukipita sehemu zote unakuta Watanzania wametulia wanafuatilia kazi ambazo Mheshimiwa Rais anazifanya; iwe ni baa, saluni au mabenki kwa sababu Watanzania wanaona namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba hatuwezi kuacha kuonesha ziara za Mheshimiwa Rais kwa sababu ni mambo ambayo yanahusu maendeleo na yanawagusa Watanzania na Watanzania ni vitu ambavyo wanapenda kuviona. Sasa kusema kwamba kwa nini tunamuonesha ni hoja haina nguvu wala mashiko. Kwa sababu Mkurugenzi wa *TBC* yuko humu ndani, mimi nimwambie kwamba aendelee kufanya kazi kuhakikisha kwamba Watanzania wanajua namna gani ambavyo Serikali yao inatekeleza Ilani pamoja na ahadi ambazo ziliahidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ambayo imeibuliwa na Mheshimiwa Amina Mollel, amezungumza kuhusiana na maslahi duni ya wafanyakazi wa *TBC.* Niseme kwamba kwa kipindi kirefu sana sisi kama Wizara tumekuwa tukijitahidi kuhakikisha kwamba maslahi ya watumishi wa *TBC* yanaboreshwa na tumechukua hatua mbalimbali. Mojawapo ni kuhakikisha kwamba tunapeleka ombi kwa Msajili Mkuu wa Hazina ili basi aweze kuboresha mishahara ya watumishi wa *TBC.* Tunaamini kwamba katika mwaka huu wa fedha 2019/2020, maslahi hayo ya watumishi likiwemo suala la kupandishwa mishahara yatazingatiwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia Mheshimiwa Naibu Waziri, tayari muda.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi kumekuwa kuna changamoto kubwa sana ya malimbikizo ya madeni kwa watumishi wa *TBC.* Niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu mpaka sasa hivi imekwisha kutoa Sh.3,200,000,000 kwa ajili ya kumaliza madeni yote ya watumishi wa *TBC.* Kwa hiyo, Serikali ipo makini inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa ufafanuzi mzuri sana ulioutoa. *(Makofi)*

Tunaendelea na mtoa hoja, Waziri, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, tafadhali sasa uhitimishe hoja yako, tujaribu kwa nusu saa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa hotuba nzuri iliyosheheni maoni na ushauri ambao Wizara yangu inaahidi kuuchukua na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie nafasi hii vilevile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2019/20 kwa kauli na kwa maandishi. Michango mingi iliyotolewa kwa kweli inalenga kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na ni sekta ambazo zinasimamiwa na Wizara yangu, hivyo, niseme tu kwamba michango yote tumeipokea na tutaizingatia katika utekelezaji wa majukumu kwani wajibu wetu sote ni kuwahudumia Watanzania waliotupa dhamana na wenye matarajio mbalimbali kwetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, nitajibu machache. Kwa kifupi bajeti yangu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 46 ambapo waliochangia kwa maandishi ni 28 na kwa kauli ni 18. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliotambua jitihada zinazofanywa na Wizara katika kuendeleza sekta inazozisimamia kwa kutoa pongezi mbalimbali. Kwa niaba ya Wizara nazipokea pongezi hizo na ushauri uliotolewa kwa kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru vilevile Naibu Waziri kwa kutolea ufafanuzi hoja kadhaa, tena nyingi, kwa haraka. Nami nitatolea ufafanuzi hoja zingine chache kadri muda utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, nianze na mchango adhimu wa Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa ambaye aliongelea masuala mengi muhimu kuhusu uzalendo na umuhimu wake katika maendeleo na ulinzi wa taifa. Ameongelea masuala ya Tunu za Taifa na umuhimu wake kwa maana ya utambulisho wa taifa ukiwemo Mwenge wa Uhuru, yote aliyoyasema namhakikishia Mheshimiwa Dkt. Tisekwa tumeyazingatia kwa maana ya kuyafanyia kazi ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja tu la Mwenge nilitolee mkazo zaidi kwamba kila taifa duniani lina tunu zake ambazo zinalitambulisha na kulipa msingi wa uwepo wake na mwelekeo wa taifa hilo kisiasa, kijamii na kiuchumi. Waliotangulia kujitawala, chukulia wenzetu kama Wamarekani ambao wana Katiba ya mwaka 1787, wana *stars and stripes* (nyota na mistari) ambayo ni bendera yao na inaakisi historia na dira yao. Nyota zile 50 ni yale Majimbo yaliyoungana kuunda Marekani na ile mistari 13 ni yale makoloni yaliyomgomea Muingereza kuweza kuendelea kutawala. Pia wana tai kwenye nembo zao na tunu zao na yote hii inaashiria malengo pamoja na dhamira ya taifa hilo.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wahindi wana Tiranga**,** bendera yao yenye rangi tatu, ambayo inaashiria ujasiri, amani na imani. Vilevile katikati wana gurudumu ambalo linaelezea ndoto aliyokuwa nayo Mahatma Gandhi ya India kuwa na viwanda vya nguo kuweza kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna bendera yetu yenye rangi nne zinazoakisi amani na umoja na rasilimali tele ambazo Mungu ametubariki na ambazo sisi tuna wajibu wa kuzilinda kwa faida yetu na vizazi vinavyokuja. Pia tuna Mwenge wa Uhuru na Kiswahili. Kwa hiyo, utambulisho wetu umeainishwa kwenye sera, nina uhakika Waheshimiwa Wabunge wote wameiona Sera yetu ya Utamaduni lakini utekelezaji kisheria wa maudhui ya sera yetu haujawa wa kasi kutokana na Wizara zinazosimamia utamaduni kubadilika mara kwa mara, nafikiri tumekuwa na Wizara kumi zikisimamia utamaduni katika historia yetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano mdogo kwamba Sera yetu inasema lazima tuwe na taratibu maalum ambazo zitalinda hadhi ya utambulisho wetu. Nitoe mifano michache tu, kwanza, misingi ya Katiba ya Taifa ifundishwe kwa wanafunzi wote katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari. Pili, Wimbo wa Taifa ufundishwe kwa wanafunzi wote kuanzia shule za awali na inasema Wimbo wa Taifa utaimbwa kila siku kabla wanafunzi hawajaingia darasani katika shule za awali, msingi na sekondari. Watu wote watasimama kuimba

Wimbo wa Taifa kabla ya kuanza maonesho na michezo yote yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa. Tatu, itakuwa marufuku kupandisha Bendera ya Taifa iliyopasuka au iliyopauka. Nne, Mwenge wa Uhuru utaendelea kukimbizwa nchini na Serikali itahakikisha kwamba wananchi wote wanauthamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona ipo sababu pamoja na kwamba Wizara zinabadilikabadilika kwa hiyo utekelezaji wa maudhui wa mambo mengi imekuwa siyo rahisi sana, ipo sababu kwa kweli kwa Wizara kutafsiri maudhui ya sera kisheria ili tusiyumbe tena. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jasmine kwa mchango wake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William Ngeleja ameongelea maendeleo ya soka nchini na wengine wengi wamegusia suala hili. Ni kweli kabisa tumepiga hatua kubwa pamoja na Timu yetu ya Vijana kukwama kusonga mbele katika Fainali za *AFCON* Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tumejifunza mengi, nimepata bahati ya kukutana na akina El Hadji Diouf, Tim Etoo na wengine ambao wapo Dar es Salaam kufuatilia vipaji vya Tanzania, wanasema Tanzania tayari ni kivutio cha mataifa na wataalam mbalimbali kuja kuangalia vipaji vilivyopo hapa. Siyo kwa kubahatisha ni kwa sababu sasa hivi, pengine Watanzania hatuoni tu lakini kwa kweli anayeongoza kwa ufungaji magoli Ulaya ni kijana kutoka Bara la Afrika na kijana kutoka Tanzania, kwa hiyo, tuna vivutio vingi sana. Tatizo letu ni kwamba tuko juu changamoto yetu ni kubakia hapo juu na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante Mheshimiwa Ngeleja kwa wazo la kuwa na *sports academies* kikanda ili kuvuna vipaji vikubwa tulivyo navyo pembe zote za nchi. Wazo ni zuri lakini haliwezi kufanywa na Serikali peke yake, tunahitaji kwa kweli ushirikiano wa karibu na sekta binafsi. Changamoto tuliyonayo ni kwamba tunapovumbua vipaji vizuri sana kupitia UMITASHUMTA na UMISETA na vipaji vingine mitaani, tunakosa mahali pa kuvilea kwa mpangilio.

Mheshimiwa Spika, wakati tunahimiza sekta binafsi kushiriki katika ujenzi kwa kweli wa hizo *academies* kwenye kanda zetu, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Elimu kwa kweli tunataka tuanze mara moja kujadiliana na *sports academies* zilizopo na zipo nyingi, kama tano, sita, tuangalie tunaweza kushirikiana kiasi gani kuweza kuchukua vijana wenye vipaji. Tuna Azam, *Alliance* ya Mwanza, *Trust St. Patrick Schools* Arusha, *Lord Baden-Powell* ambayo ipo Bagamoyo na *Fountain Gate Academy* Dodoma. Nafikiri tukikaa chini tunaweza tukaanza mahali fulani tukasogea. Nakuhakikishia tutafanya hivyo ndani ya muda siyo mrefu kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije upande wa habari lakini naomba nianze na utangulizi mfupi ili tuelewane. Habari yoyote inayoandikwa na kuchapishwa yenye athari ya kuharibu sifa ya mtu katika jamii ni kashfa. Ni haki kwa mtu aliyekashifiwa kwenda Mahakamani kudai fidia kwa maumivu aliyosababishiwa chini ya kifungu cha 41 cha Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016. Mara zote tunawahimiza walalamikiwa kutumia kifungu cha 40 kuomba radhi *(offer of amends)* na ukiomba radhi kwa anayejisikia kuathirika, hakuna haja hata kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mara zote tunawasisitizia pia na ningependa pia hili lieleweke hapa kwamba tuepuke kujichukulia sheria mikononi kwa kumnanga aliyekukashifu kupitia njia mbalimbali za mawasiliano, sasa unaondoa uzito wa kesi yako mwenyewe. Wanasheria tunayo kanuni ya haki *(equitable principle)* ambayo inasema *he who seeks equity should come with clean hands.* Anayehitaka haki, basi njoo na mikono misafi. Ukisema umetupiwa madongo, kweli umejaa madongo kwenye shati na wewe umeshika madongo kumtupia mwingine, hoja yako haiwezi kuwa safi sana wakati na wewe una madongo mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Idara ya Habari ndiye mwenye mamlaka chini ya sheria ya kutoa Leseni ya Magazeti kuchapishwa na kuuzwa kwa kuzingatia masharti kadhaa. Hii siyo Tanzania tu, ipo duniani kote. Ana mamlaka

chini ya sheria hiyo ya kifungu cha 9 *ku-suspend,* yaani kusimamisha leseni hiyo pala anapoona masharti ya leseni yanakiukwa. Tatizo la walio wengi, wakishasimamishiwa leseni, hawaendi Mahakamani, bali wanakimbilia kwenye Balozi. Hiki ni kitu cha ajabu nimekiona hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Devotha Minja alinioji, napata wapi mamlaka ya kufungia gazeti kwa muda; kama nilivyofanya huko nyuma? Nitamjibu, lakini nami namwomba kupita kwako atafakari ni kifungu kipi cha sheria kinasema usipokubaliana na Mkurugenzi wa Maelezo, basi kimbilia kwenye Balozi? Sijakiona hicho kifungu. Sijui, nadhani ni aina fulani ya ulimbukeni.

Mheshimiwa Spika, maana sheria inasema, kata rufaa kwa Waziri. Hakuna anayekata rufaa kwa Waziri na wanasema hata Waziri akishatoa uamuzi wake, bado una haki ya kwenda Mahakamani kumshungulikia huyo Waziri pamoja na Mkurugenzi. Hatutumii hiyo nafasi, tunakimbilia Ubalozi; na Balozi zinakuja kila mara kwetu nasi tunawajibu, mmesoma hiyo sheria?

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumjibu Mheshimiwa Devotha kuwa Waziri ana mamlaka chini ya kifungu 59 kinachosema, Waziri ana mamlaka ya kuzuia uchapishaji wa maudhui yenye athari kwa usalama wa nchi au amani katika jamii. Waziri anafikia hatua hiyo siyo tu haraka haraka, hapana. Ni baada ya mtu kuonywa au gazeti kuonywa mara nyingi sana; mara nane, tisa, kumi. Nyie hamwezi kuona hivyo, kwa sababu hamfanyi kazi kwenye hayo magazeti. Sisi tunafahamu, hatuchukui hatua hizi bila kumwonya mtu mara kadhaa. Hii ni kwa mujibu wa mkataba wa Kimataifa wa haki za kisiasa na kiraia ya mwaka 1966. Wengi hawapendi kuisikia hiyo, lakini ndiyo hiyo *International Covenant on Civil of Political Right* duniani kote tumeridhia na hata wakubwa wanaitumia hiyo hiyo. Wewe mchukulie kama Bwana Hasanja ambaye huu ni mwaka wa saba hayupo huru akikwepa kupelekwa Marekani kujibu mashitaka ya kuhatarisha usalama wa Marekani. Ila kwa sababu ni Marekani, aah, ila Tanzania ikitumia hiyo sheria, haki za

binadamu kwa sababu pengine *NGO's* nyingi zinafadhiliwa kutoka huko, hatuoni hiyo ya huyo anayetoa hela.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli, kinyume na alivyosema Mheshimiwa Devotha kuwa tunafungia magazeti kila siku. Sasa kila siku kweli! Pengine hiyo ni lugha tu, siyo kweli. Tulifungia magazeti manne mwaka juzi, 2017 ili Waandishi na wamiliki na wadau waelewe kuna sheria mpya ambayo walikuwa hawaitaki. Hawaitaki tu, hata kuisoma hawajaisoma.

Mheshimiwa Spika, leo hii nikisema nimwulize mtu gani ameisoma Sheria ya Huduma za Habari, naomba Mungu awe shahidi yangu nina uhakika, hata wanaolalamika hapa hawajaisoma hiyo sheria. Ndiyo tatizo letu kubwa tulionalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 sijafungia gazeti lolote; ni juzi tu *Citizen* waliadhibiwa na Mkurugenzi kwa siku saba kwa kushindwa kufuata masharti ya leseni baada ya kuonywa na kuonywa. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanadai kuwa *Tanzanite* halichukuliwi hatua, siyo kweli kwa sababu nyie hamko ofisini kwetu, uliza uweze kupata taarifa. Kwanza mnataka hatua zipi tuchukue? Kulifungia?

Ndugu zangu, malalamiko mengi zaidi ya *Tanzanite*, kama ilivyo kwa gazeti la Tanzania Daima na mengine, ni kashifa. Unakashiwa wewe, heshima yako imeshushwa; unaitaka dola ifanye nini kwa heshima yako kudhalilishwa? Nenda Mahakamani. Ukija kwetu, sisi kazi yetu kubwa ni kumwita chini ya kifungu cha 40 kumwambia omba radhi, huyu akikupeleka Mahakamani utalipa fidia kubwa. Wengi wanaomba radhi, wengine wanakwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda wenyewe ndiyo unakimbia hivi, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani amedai usalama wa wanahabari nchini ni mdogo sana, kuna vitisho, yaani ni hatarishi. Bahati mbaya ametoka, napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge kupitia kwako atembelee tovuti *www.forb.com. Forb* ni chombo maarufu cha takwimu

duniani aangalie taarifa yao ya mwisho wa Desemba mwaka 2019 inayohusu *deadliest countries for journalist in 2018,* nchi hatari kweli kweli kwa Waandishi wa Habari duniani. Inataja India, Mexico, Marekani yenyewe, Brazil na Israel. Tanzania hatumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tupunguze Kauli kali sana hizi bila kufanya hata utafiti, pengine kwa sababu hatujui yanayotendeka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi na Anatropia Theonest wameongelea uamuzi wa Mahakama ya Afrika Mashariki kukosoa baadhi ya vipengele kwenye Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na kutaka viondolewe baadhi ya vifungu. Hii ni mara ya tatu sheria hii inapelekwa Mahakamani. Mara ya kwanza tulikwenda Mwanza haikufanikiwa, mara ya pili Mahakama Kuu Dar es Salaam haikufanikiwa. Sasa imepelekwa Mahakama ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nataka kusisitiza hii ni haki ya Watanzania wanapoona hawajaridhishwa na maamuzi, pengine wana wasiwasi na maamuzi ya vyombo vya ndani, nenda, ndiyo fursa. Ndiyo maana nchi yetu inajivuna kwamba tumewapa wananchi wetu uhuru mpana. Nenda; Mahakama ya Afrika Mashariki wamekwenda. Wengine wanachukulia kama Serikali hapa imeshtuliwa kweli kwa kupelekwa Mahakamani. Hapana, sisi ni Waasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Afrika Mashariki sehemu kubwa kwa Tanzania tumechangia na kuanzishwa hii Mahakama, nenda kwenye *records,* sisi ndiyo tumepiga kelele lazima tuwe na Mahakama ya Afrika Mashariki kwa sababu tunataka wananchi wetu wakiona hawawezi kupata haki, waende sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tu nisisitize kwamba uamuzi huo tumeona una upungufu na tarehe 11 mwezi huu Ofisi ya

Wakili Mkuu wa Serikali ilipeleka *notes* ya kusudio la kukata rufaa ngazi ya juu ya *East Africa Court Justice.* Sisi tunataka tu tuelewane kwenye vipengele mbalimbali, lakini kwa sababu liko Mahakamani sitalijadili sana. Tuna hoja nzito, nina uhakika tutashinda.

Mheshimiwa Spika, siwakatishi tamaa Watanzania wetu ambao mmepewa na nchi yenu uhuru mpana zaidi. Bado wana nafasi ya kwenda Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika, ipo Arusha. Hiyo Mahakama iliazishwa mwaka 1998, nchi 30 zilikubali tukaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba ni sisitize, kuielewa nchi yetu ilivyo, ni nchi tano tu kwa muda mrefu zimekubali wananchi wake waweze kuishitaki Serikali kwenye hiyo Mahakama. Tanzania tumo, sasa hivi tuko tisa. Jamani, mnyonge, mnyongeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khatibu Haji na Mheshimiwa Devotha Minja walioji kwa nini Mkurugenzi wa Maelezo alivitaka Vyombo vya Habari vilivyoandika habari za *ACT* vijieleze?

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kuwa hali haikuwa hivyo. Tarehe 4 Aprili, Kiongozi wa *ACT* Wazalendo, Mheshimiwa Zitto aliitisha Mkutano na vyombo vya habari kutoa maoni yake kuhusu Ripoti ya *CAG*. Hili siyo kosa. Naomba nisisitize Watanzania; Mtanzania ana haki. Ripoti ya *CAG* iko pale, zungumza unavyotaka u-*base* kwenye hiyo ripoti, hatuna shida. Mheshimiwa Zitto alitumia haki yake ya kikatiba kuweza kujadili Ripoti ya *CAG*.

Aidha, kisheria hakuna kosa lolote kwa chombo cha habari kunukuu kile kilichomo kwenye taarifa hiyo. Sasa nashangaa ilionekana kwamba tumezuia, haiwezekani kunukuu chochote, hapana, siyo hivyo. Tena naomba nisisitize kwamba tatizo lililojitokeza pale ambapo magazeti yalipoiacha Taarifa ya *CAG* na kujielekeza kwenye maoni binafsi ya Mheshimiwa Zitto.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zitto alianzisha ya kwake, sasa tukawa na *CAG* wawili. Sasa kwa maadili ya Uandishi wa Habari, kwa sababu hiki ni kitu kipya, siyo *based* kwenye ripoti ya *CAG,* inabaidi umhoji na yule mwingine ambaye anatuhumiwa humo kwamba amepoteza shilingi bilioni 800, ni pesa hii kwamba haionekani, hiyo ni yake wala hata *CAG* hakusema. Ndiyo maana Mkurugenzi wa Habari akasema, jamani eeh, hebu elezeeni, mbona mnakiuka maadili? Hiki kitu kipya wala hakipo kwenye taarifa ya *CAG.* Kule kuuliza tu imekuwa nongwa; na hakuna hata mmoja aliyesimamishwa kwamba unasimamishwa kwa sababu ulimnukuu Zitto wa *ACT*.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kusema kwamba Mkurugenzi wa Idara ya Habari alifanya hivyo kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Huduma ya Habari, hakukosea popote. Mheshimiwa Joseph Kasheku ameongelea hali ya wana tasnia wa filamu; wapo wengi sana hapa; kuwa wana hali ngumu mno na hivyo wanasababisha kujihusisha na kula michango ya misiba; pili, kuendesha madanguro.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwelezea Mheshimiwa Musukuma kupitia kwako kuwa vitendo hivyo havikubaliki kisheria. Ni kosa la jinai kuendesha madanguro. Ukisoma *penal code cap* 16, ni kosa. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani asilichukulie hili kwa nguvu. Nadhani Mheshimiwa alikuwa anatia tu chumvi kidogo ili asikike zaidi hapa.

Mheshimiwa Spika, naelewa vijana wetu wa filamu wanafanya vizuri kuliko kipindi chochote katika historia ya nchi hii. *(Makofi)*

Ndugu zangu, kwa mara ya kwanza naweza pia kusema katika historia ya tasnia ya filamu, Wizara imeingilia kati mikataba ya wanatasnia wa filamu. Kwa mfano, Kampuni ya Jerusalem ya *JB* na Kampuni ya kijana wetu Kigosi RJ zililipwa jumla ya shilingi milioni 32 kwa *intervention* ya Wizara.

Bodi ilikuwa pale kwa niaba ya Wizara, ikafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, tuna mifano mingi ambapo Kampuni, huyu Hussein Kim, amelipwa shilingi milioni 18 na Kampuni ya *Proin Promotions* na *Puppy Zee*. Ninachotaka kusema tu ni kwamba hebu rudi kwenye kitabu changu cha hotuba, tumefanya mengi sana kuweza kuisaidia tasnia ya filamu na sanaa nzima. Najivuna kwamba katika kipindi changu nimeweza hata katika kutetea vijana wetu, wasanii wawili, wanamuziki wameweza sasa hivi kuwa mamilionea kwa sababu wamelipwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa haki ambayo ilikuwa inapotea. Bila Wizara kusimama kidete wasingepata hiyo pesa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwakajoka, amezungumzia uhuru wa habari. Ahsante kwa ufafanuzi ulioutoa Mheshimiwa Spika. Unajua uhuru anaoulilia Mheshimiwa Mwakajoka mdogo wangu pale. Sijui ndiyo ule uhuru wa mtu anaamka tu asubuhi anaamua kumfungisha ndoa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Mheshimiwa Halima Mdee! Maana ndiyo uhuru mnaoutaka huo, bila kujali kwamba unafanya hivyo wakati sisi watu wengine tuna familia, tuna watoto. Ina-*impact* kubwa sana, lakini ndiyo uhuru tunaoutaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu amekaa tu; na uzuri wake nimewaomba wataalamu wa *TCRA* waangalie ni nani. Sitaki kumtaja jina hapa, ni mtu mzima ana familia yake, kakaa nyumbani anaanzisha *rumors* za kipuuzi kama hizo. Sasa hizo turuhusu, itakuwa nchi gani hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwakajoka amemwongelea Ansbert Ngurumo. Nafikiri hao wengine aache tu wajitetee wenyewe kwa sababu nikisema niletee hapa ushahidi kwamba Ngurumo amewahi kutuhumiwa na Serikali hata siku moja; ndiyo utagundua kwamba watu wengine wanaenda Ulaya ni mshiko tu. Kwa kweli hajatuhumiwa na mtu yeyote yule.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa sababu nimepigiwa kengele, niongelee kidogo tu kuhusu hoja aliyoelezea Mheshimiwa Juma Nkamia kwamba vijana wetu wa Serengeti kwa kweli hawakuandaliwa vizuri, pengine ndiyo maana hawakufanya vizuri sana, hapana. Mpira ni mpira. Tuliwaandaa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, niulize swali, hawa vijana wamechukua makombe *competitive* kama *CECAFA* na *COSAFA* kwa kubahatisha? Hapana, ni kwa sababu ya mazoezi mazuri waliyokuwa nayo, lakini mpira ni mpira, lazima mtu mmoja ashindwe na mwingine ashinde.

Mheshimiwa Spika, vilevile vijana wetu walikuwa na *pressure* kubwa mno ya kubeba matumaini ya Watanzania. Umri wa miaka 16 ni mdogo sana. Vilevile nawalaumu watu wanaoitwa ma-*agents.* Wamekuja ma-*agents* kutoka nchi mbalimbali, wote akina Diouf hao, kundi la Etoh**,** kuja kwa watoto wadogo wale unawaambia tunakuhitaji kwenye timu yetu, tutakulipa shilingi milioni 100 kwa mwezi, kanachanganyikiwa. Kanacheza pale kanaangalia ile hela; wazazi wengine wanapata taarifa kwamba mtoto wako bwana ameahidiwa shilingi milioni 100 mpaka 200 kwa mwezi. Wanawaambia, mwanangu usicheze, utavunjika mguu. Hii hela ndiyo itatutoa.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri imetufundisha. Nimeiagiza *BMT* itengeneze Kanuni kwa ajili ya kuendesha shughuli za u-*agency* hapa nchini kuhusu vijana wetu. Nimalizie na Mheshimiwa Aida Khenani, kwamba Serikali inasema nini kuhusu Azory? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tunaongelea kesi ambayo ni dhaifu sana, tena sana. Mwandishi huyu amepotea. Eneo ambalo mamia ya Watanzania wengine wamepotea hawaulizwi wao, huyo mmoja ndiyo dhahabu. Halafu inaulizwa Serikali ambayo yenyewe imeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, Maafisa wetu wa Serikali wamekufa wengi kule. Leo tunaulizwa mmoja, *it is extremely unfair.* Najua mnawalisha Wazungu na wafadhili wengi, matango pori hayo, acha wayapate, lakini ninachosema hatujakosa chochote, acha tushushwe hayo madaraja, sisi bwana uhuru wetu kwanza tunauthamini, hayo madaraja baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa neno moja tu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Rashid Shangazi. Kwanza namshukuru kwa kunukuu Ibara ya 18 na 30 kwa pamoja, kueleza kwamba uhuru duniani kote lazima uwe mipaka. Walikuwa kuniona wale Waandishi wa *(International Press Institute - IPI)*. Huyo Mhindi ndio alikuja akaniambia kwamba tumekuja Tanzania kwa sababu tuna taarifa ya kwamba kuna Waandishi wa Habari 30 wako kizuizini. Nikamwambia naomba usitoke ofisini kwangu unithibitishie hao 30 ni akina nani? Baadaye akaishia kusema nimeona kwenye mtandao wa jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa na mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa hitimisho lako zuri kabisa na maelezo ambayo umeyatoa kuhusiana na hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Nina hakika muda hata kama ungekuwaje usingeweza kumaliza hoja zote maana wengi wameandika na kadhalika. Mtaona kama Wizara wakati mwingine baadhi mnaweza mkayaweka kwenye majibu ya maandishi na kadhalika. *(Makofi)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi, Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Waheshimiwa kabla hatujaanza, niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mara tu tukimaliza shughuli hizi asubuhi hii, tutakutana kwenye ukumbi wa Spika hapo nyuma, Kamati ya Uongozi tukimaliza hapa tukutane kwa muda mfupi hapo nyuma kuna mambo ya kuzingatia. Katibu.

**Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..…….Sh. 4,203,111,000

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri si ndiyo? Tunaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Wakati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anahitimisha hoja yake hapa, alizungumzia kesi namba mbili ya mwaka 2017, iliyokuwa chini ya *East Africa Court of Justice* ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishtakiwa na Kituo cha Haki za Binadamu, Baraza la Habari na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu na kwa maana hiyo ameshindwa. Hata hivyo, wakati Mheshimiwa Waziri anaeleza hapo ameeleza kwamba wako katika mchakato na wao wa kukata rufaa au na wao wameshakata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua kwamba wakati tunaendelea kusubiri rufaa na mambo ambayo yamezungumzwa katika hukumu hiyo ni pamoja na suala zima la utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi. Ni jinsi gani Serikali imejipanga sasa kuhakikisha kwamba mambo haya yaliyozungumzwa na

ambayo kwa kiasi fulani yanaweza yakaathiri hata uwepo wetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanaondolewa katika sheria hii na kama majibu yatakuwa hayaridhishi basi nitaomba kuondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri katika mshahara wake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Shangazi urudie tena kwa dakika moja tu. Swali lako ni nini, kwa kifupi moja kwa moja tu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni kwamba, hukumu imeshakwisha kutolewa, hukumu ya kesi namba mbili katika Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2017 ambayo imetoa haki kwa walalamikaji watatu ambao ni Kituo cha Haki za Binadamu, Baraza la Habari la Taifa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu kwa misingi kwamba sheria ile inakiuka misingi ya utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji.

Sasa wakati Serikali inajipanga kwenda kukata rufaa kwa sasa hivi kabla ya rufaa inachukulia vipi jambo hili hasa kwa mustakabali mzima wa sisi Watanzania kuwemo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo sisi ni….

**MWENYEKITI:** Sasa nimekuelewa, kwenye kipindi cha mpito, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Shangazi kwa swali lake zuri. Kama nilivyoeleza nilipokuwa nahitimisha hoja hii kwamba kwa kweli tumepeleka kusudio la kukata rufaa kwa mujibu wa sheria kwa sababu uamuzi uliotolewa, ulitolewa na Mahakama ya ngazi ya kwanza, wao wanaita *court of first instance,* lakini sasa hivi sisi tunakwenda kwenye ngazi ya pili ambayo ni *upper division* na uamuzi wa *upper division* ndiyo ambao utaweza kuwa na athari kwenye sheria tuliyonayo, lakini kwa sababu tulishasema hapana, hatukubaliani sisi tunaendelea kama kawaida na utekelezaji wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbilinyi Joseph.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kabisa katika hili nisipojibiwa vizuri nitaondoa shilingi na kuondoa huku shilingi *it's not personal* haitaathiri familia kwa sababu najua Mheshimiwa George Mwakyembe ameshamaliza *Masters* na mtoto wa dada yangu Shonza *I can take care* kwa mwaka mmoja ambao atakuwa hana mshahara, naweza nikamtunza. Kwa hiyo hii ni kwaajili ya nchi. Mimi katika suala hili la kesi ya Afrika Mashariki nataka kujua vinginevyo nitaondoka mshahara, kwa kuwa bado hawajakata rufaa tunatakiwa kufanyia kazi uamuzi ambao ni *valid* sasa hivi wa mahakama kwamba tumeshindwa. Ni lini sasa Waziri au Serikali italeta sheria hii ili vifungu hivi vinavyolalamikiwa kifungu 3(a) kifungu 13, kifungu 19, kifungu 20, kifungu 21, kifungu 34, mahakama hii ya Afrika Mashariki imesema wazi kabisa vinakiuka Utawala Bora, demokrasia na utawala unaozingatia sheria. Sasa *regardless* humu ndani tuliongea nini na mkaamua nini kwa sababu mko wengi lakini sasa tukubaliane kabisa kwamba hili suala linatutia aibu nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbilinyi nakushukuru nilikupa nafasi ili usikike, lakini kwa kweli utaratibu wetu tayari alishakutangulia Mbunge mwingine na limepata majibu, Mheshimiwa Shangazi na limejibiwa hapa, kwa hiyo hoja inakufa. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftah.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nchi hii imeweka Katiba na katika Katiba, Ibara ya 18(d) inasema:

*"Kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita ndani ya Bunge hili tulíletewa hoja ya kusitisha Bunge kuonesha *live*

kwa wananchi wetu wa Tanzania, waweze kupata habari mbalimbali na hasa ukizingatia kwamba Bunge hili linapitisha bajeti ya wananchi ambao wametajwa kwenye Ibara hii ya 18, lakini jambo lingine ni kwamba hili suala la kupata taarifa hili ni muhimu sana kwa sababu bajeti tunajadili maisha ya wananchi mmoja mmoja, tunajadili maisha ya wafanyakazi, tunajadili Wizara zote. Kwa hiyo maisha ya Watanzania yame-*base* katika bajeti ambazo tunapitisha hapa Bungeni. Kwahiyo ni wajibu wa Serikali kumwezesha Mtanzania huyu kuweza kupata taarifa za maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi na nakusudia kutoa shilingi kama sitaridhika, kwa nini kwenye kitabu hiki cha bajeti hii mwaka huu Mheshimiwa Waziri kwa sababu alisema tatizo la kuonesha Bunge *Live* ni kwamba Serikali haina fedha lakini tulitegemea kwamba ataomba kwa wahisani na kuweka bajeti, lakini hata shilingi sijaiona humu ya kulipia vyombo vya habari, Bunge liweze kuonesha maisha ya wananchi kupitia bajeti ambazo zinapitishwa hapa. Nakusudia kutoa shilingi kama sitapata ufafanuzi wa kina

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijielekeze kwenye suala la Mheshimiwa Maftah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa ananilisha maneno, eti nilisema hatuna pesa, lakini nasema kwamba tumelizungumza hili suala mara kadhaa. Suala la kuonyeshwa program zetu humu *live* liko kwenye mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafikiri tumeshalieleza sana na Mheshimiwa sijui kama naweza kuongeza zaidi ya hapo, lakini ni kwamba pamoja na hilo amenukuu ibara ya 18 ikisema, kila mtu ana haki ya kupewa taarifa, lakini naomba tuoneshe na kifungu kinachosema hizo taarifa ziwe *live. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama ndio Waziri wa Bunge, hapo hapo ulipo kuna swali la Mheshimiwa Nachuma, anasema kwa nini Bunge halionyeshwi *live*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 53(7)(4), jambo ambalo lilikwishaamuliwa na Bunge hili kwa kuzingatia misingi ya kikanuni haliwezi kufufuliwa tena kwa namna yoyote ile mpaka iletwe hoja mahususi ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo kwa kuzingatia kanuni hiyo Mheshimiwa Nachuma anaweza kama anaona maamuzi ya Bunge hayakuwa sawasawa, atumie kanuni ninazozitaja ili kulileta jambo hili kwa hoja maalum. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nachuma kwa kuwa umejibiwa kikanuni, ile kusema lijadiliwe tena haiwezekani, kwa hiyo kajipange tena. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba pia nimshukuru Waziri kwa majibu aliyonijibu kuhusiana na uchangiaji wangu, lakini naomba niseme tu, yale niliyoyasema juzi kwenye mchango wangu sijabahatisha nimefanya *research* ya kutosha. Wasanii wako hoi, hoi bin taaban na hata kauli ya Waziri kusema Wizara ya Mambo ya Ndani ishughulike nayo si jibu sahihi, siyo tiba kwa sababu asifikiri watu kufanya hizo shughuli wanafanya kwa kupenda, wanafanya kwa shida. Narudia tena kuthibitisha kwamba kauli yangu niliyoisema ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri amejikita tu kuzungumza suala la nilivyosema wasanii wanaendesha biashara za madangulo, lakini hoja yangu ya msingi ya kuwasaidia wasanii wa bongo muvi hajaigusa hata kidogo ili tuwaboreshe, nilimwambia ameruhusu tamthilia za Kihindi, za Kizungu, watu wanatafasiri filamu za kizungu hovyo hovyo, wengine hawajui hata Kiingereza wanadanganya watu, wamepelekea kuua hii tasnia. Mheshimiwa Waziri

hajaja na majibu ya huo mkakati anazungumzia suala la madangulo na kumwambia Waziri wa Mambo ya Ndani ashughulike nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natarajia nitoe shilingi kama Waziri hatanipa jibu kwamba nini mkakati wa Wizara yake kuwasaidia hawa wasanii kutoka huko waliko ili waweze kuinuka watoke kwenye biashara za madanguro na ukuwadi? Akinijibu hayo nitaridhika, asipojibu hayo majibu mazuri, natarajia kutoa shilingi ili Wabunge wenzangu pia kwa sababu wote humu tunawategemea wasanii hasa kwenye chaguzi, naamini wataniunga mkono angalau tuweze kujadili tuone kama Bunge linaweza kuwasaidia wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Sijaelewa kidogo maana wasanii leo wako hapa, kwani hawa wasanii wanashughulika na biashara hiyo, eti jamani mnashughulika na hiyo biashara? Sijui Mheshimiwa Waziri anaelewa vizuri zaidi, tafadhali ufafanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia vizuri Mheshimiwa Musukuma kwenye hili suala. Kwanza naomba tu nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, ingekuwa ni suala pengine linahusu makinikia, magwangala, kwa kweli Mheshimiwa Musukuma mimi hapo ningekaa kimya. Mimi ni msanii, tena nafikiri mungu alinibariki tu kipaji hicho nimeanza kuandika mimi vitabu nikiwa *form four*, nimeanza kuigiza mapema sana mimi *scrip*, mimi ni mwafrika wa kwanza kuandika *script* ya sinema Ujerumani ikashinda, kwa hiyo, naelewa usanii ni nini. Ukinipa gita hapa Mheshimiwa Mbilinyi atachora tu mistari siyo matatizo sana. Kwa hiyo naongea, nina *passion* na hiki kitu, nakielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema Sera ya Utamaduni imesisitiza kabisa tuunde chombo kusimamia maslahi ya wasanii wetu. Tumeunda chombo kinaitwa

*COSOTA, COSOTA* iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, tunahangaika sasa hivi kuitoa *COSOTA* ije katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo hizo ndiyo shughuli ninazozifanya Mheshimiwa Musukuma hajaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Serikali hii ni sikivu, ndiyo maana tuliposikia kwamba kuna manung'uniko Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewaambia vijana njooni niwasikilize. Sasa kama Mheshimiwa Musukuma anaona aendelee na shilingi sijui wasisikilizwe hiyo kesho, mimi nitamshangaa sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mchungaji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Katika majibu yake kuhusiana na michango ambayo tumechangia kuhusiana na Gazeti la *Tanzanite,* kuna maelezo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza ni ya msingi hasa kuhusiana na kwamba watu wanafamilia zao wanavunjiwa heshima, ni kweli kabisa nakubaliana na hoja hiyo. Hata hivyo, bado nataka niende mbele na asiponipa maelezo ya kutosha nitatoa shilingi yake Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti hili kama alivyosema wanataka wa-*regulate* na tuwe na Taifa zuri la kuheshimiana, lakini mambo mengi katika gazeti hili pamoja na kwamba katika maelezo yake amesema kwamba ni masuala ya jinai, *I mean* ya madai, watu wanatakiwa waende wenyewe, gazeti hili ukilifuatilia kwa mfano kumekuwa na kichwa cha habari kinasema: Shoga awachanganya Zitto na Maalim Seif.

Mheshimiwa Mwenyekiti. suala la ushoga katika nchi yetu ni jinai, hajatuambia Serikali imechukua hatua gani katika kumjua huyo shoga na kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti pia gazeti hili linasema: Wananchi wataka JPM atawale miaka 40. Ni kinyume kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marais wanatawala vipindi kumi hajasema hatua gani zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Gazeti hili linasema: Vigogo 14 hatari kwa nchi watajwa. Kama tuna vigogo 14 ambao ni hatari kwa usalama wa nchi watajwa, Serikali imechukua hatua gani? Hajasema. Nataka Mheshimiwa Waziri atoe *commitment,* kuna mambo mengi, bilioni 150 za kumng'oa JPM zatangazwa, hawa watu wamepata wapi hizi hela? Ni watakatishaji. Sasa hatuwezi kuwa na Taifa la watu ambao kwanza wana-*lower standard* ya uelewa wa wananchi tunakubaliana na *mediacracy* kwamba ndio itawale na hili gazeti linakuwa *publicize everywhere* na watoto wananyonya hizi habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate *commitment* ya Wizara. Ni hatua gani zinachukuliwa kwa mtu kama huyu. Kwa mfano, Selasini aliwahi kutajwa ni gaidi, huyu ni Mbunge katajwa gaidi na hili gazeti. Mara linasema Profesa Asad kakutana na Mbowe faragha kulivuruga Bunge, kama Bunge letu linataka kuvurugwa, tunatakaje Bunge livurugwe. Hizi hatua zimechukuliwa ziko wapi? Kwa hiyo naomba *commitment* ya Wizara, ni hatua gani zinachukuliwa kwenye gazeti hili? Kwanza linawafundisha watoto wetu vibaya tunaonekana kwamba vitu ambavyo ni *sub-standard* katika nchi vinakubaliwa. Kwa hiyo naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, vinginevyo nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Bado natafakari kama hii ni hoja au, maana ilitakiwa hoja iwe ni wapotoshaji wote na wale wengine, sasa mnakuwa mnalenga upande mmoja tu. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa ananukuu vichwa mbalimbali vya hili gazeti naomba asiende huko kwa sababu hata leo hii Tanzania Daima inasema hawa ndiyo watakaomkabili Magufuli 2020, wamefanya utafiti wapi? Tuna tatizo hilo, ingekuwa ni kufungia tungefungia magazeti yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja aliyoileta mahsusi ni kuhusu Gazeti la Tanzanite juzi kutoka na kichwa habari kama hicho. Naomba nisiwadanganye hapa Wabunge wenzangu, mimi mwenyewe sikufurahishwa na kitu hicho. Kwa sababu hili ni la maadili, mimi ni mwandishi wa habari tena naweza kujivuna kwamba mimi ni *pioneer student* wa *Tanzania School of Journalism* kabla haijaingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa hiyo, naongea naelewa maadili hapa yalikiukwa. Hatua niliyochukua ambayo sihitaji mpaka nije nyumbani kwako Mheshimiwa Msigwa nikakugongea au niende kwa Mheshimiwa Devotha, nimeandika wito tena huu ni wa kimahakama kum-*summon* anieleze, ukitaka naweza kuiweka hata juu ya meza hapa.

**WABUNGE FULANI:** Iweke.

**MWENYEKITI:** Spika hayaruhusu. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anieleze alikuwa ana maana gani, tumechukua hatua hiyo. Hilo gazeti limetoka tuko kwenye sikukuu za Pasaka, sasa umfuate mtu anakula sikukuu za Pasaka na hiyo barua utaonekana wewe mwenyewe kichaa. Kwa hiyo, sikufanya hivyo, ndiyo maana imeandikwa tarehe ya nyuma lakini tumempelekea, ameipata. Mimi naomba muiamini Serikali siyo kwamba tumefurahia hilo, hatuwezi kufurahia uandishi wa habari ambao haufuati kanuni.

**MWENYEKITI:** Ushauri wa ujumla ni kwamba mambo ya ushoga tuyape nafasi Serikali inapoyafanyia kazi iende kwa utaratibu na umakini mkubwa. Nazungumza hili kwa nia njema siyo kwamba mimi ni mpambe wa mambo hayo. Kwa sababu huko duniani, dunia inabadilika inakuwa ya ajabu kabisa, yaani ukiwagusa hawa watu hovyo hovyo tatizo kubwa kweli kweli lakini tunavyo-*advice* ni vizuri Serikali nayo inajua, sisi wenyewe kama nchi tunajua, eeeh karibu Mchungaji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimekusikia lakini gazeti hili *circulation*

yake ni ndogo sana katika hii nchi lakini ni gazeti ambalo limesheheni matangazo ya Serikali. Hoja ndiyo inapojengwa hapo, kuna nini katika gazeti hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nasisitiza kwa sababu maaelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema anigongee mimi aniletee barua ataleta Wabunge wangapi, tunataka *action* ya Waziri kwa ujumla kwenye vyombo vya habari kama mdhamini mwenye *instument* za kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wabunge wenzangu mnisaidie tuchangie, umesema tuunde taifa lenye maadili mema gazeti hili halituelekezi kwenye maadili mema ya taifa. Natoa hoja Wabunge waniunge mkono ili tuweze kuchangia, bado nang'ang'ania shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa Mchungaji wachangie kuhusu nini yaani, hoja yako mahsusi ni nini? Rudia tena hoja mahsusi ni matangazo, sasa kama ni matangazo sijui kama ni kazi ya Waziri kuangalia matangazo ya kwenye gazeti.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sio suala la matangazo ni kuhusu jinsi ambavyo gazeti hili linaandika mambo kinyume na maadili na mengine ni ya kijinai na Serikali haijachukua hatua na linaachwa tu liendelee.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Si ndiyo hiyo hatua amesema ameshachukua, katoa na ushahidi wa barua na nini au tunataka kuongea tu ndugu zangu? Baada ya hatua hii aliyochukua tumpe nafasi tuone, je, mambo haya yataendelea au hayataendelea? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nyie kaeni mimi nipo na Mheshimiwa Msingwa kwanza aweke vizuri hoja yake. Nakuwekea tu vizuri ili tuelewane, je, huridhiki na hatua hii kwamba ungehitaji hatua zaidi au nini hasa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua anazosema Mheshimiwa Waziri ni ndogo sana ukilinganisha na madhara ambayo gazeti hili linayaleta. Ukingalia wenzetu Rwanda hapo waliingia kwenye machafuko kwa mambo kama haya haya. Kuna wengine nchi hii wameongoza vizuri wamekuwa Mawaziri hata kwenye Serikali yenu lakini hili gazeti linawachonganisha watu ndani ya chama chenu, ndani ya Serikali, linakuja upande wa pili, hapa hatuzungumzii upinzani, tunazungumzia maadili ya taifa. Hata ndani ya Serikali yenu linaongea mambo ambayo ni ya hovyo. Kwa hiyo, tukiliacha gazeti hili hivi hivi bila *commitment* litatuchonganisha na Watanzania hatutaki kugomba. Kwa hiyo, ndiyo maana naomba Wabunge tulichangie kwa pamoja ili Waziri aje na *commitment* kuhakikisha hili gazeti linashughulikiwa.

**MWENYEKITI:** Na Tanzania Daima.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tanzania Daima lina matatizo nalo lishughulikiwe, haina tatizo.

**MWENYEKITI:** Hapo sawa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama lina matatizo hamna shida lichukuliwe hatua lakini inanishangaza tunalinganisha uzito wa Tanzanite na Tanzania Daima, yaani ni vitu viwili havifanani kabisa, mnajaribu ku-*squire*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, wanaotaka kuchangania pande zote mbili na Tanzania Daima nayo. Haya Mashimba Ndaki, Waziri wa Mambo ya Ndani atachukua nafasi huku, tutaanza na Mheshimiwa Magereli halafu Mheshimiwa Ally Saleh upande wa *CUF* na CCM wawili.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa ili name niseme kidogo.

**MWENYEKITI:** Dakika mbili mbili.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Cha kwanza naomba nieleze masikitiko yangu kwamba linapozungumzwa suala la Tanzanite kama gazeti ambalo linachafua sura ya taifa, viongozi na hata mwonekano wa shughuli zetu ndani ya Bunge mnataka ku-*balance equation* eti kwa kusema na Tanzania Daima je? Tanzania Daima siyo gazeti la vikaragosi kama Tanzanite nikuambie ule ukweli. Tanzania Daima ni gazeti la pili linalosomwa baada ya Mwananchi. Kwa hiyo, kufikiri kwamba mnataka ku-*balance story* kwa kuitaja Tanzania Daima inapotajwa Tanzanite, Tanzania Daima kama mlivyosikia kwa wachangiaji wengine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy unavyotengeneza *principle* iwe *principle,* sisi ni viongozi wa nchi, tutengeneze *principle* akiingia Tanzania Daima *principle* imkute, akiingia Tanzanite *principle* imkute lakini ukianza kusema huyu hivi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, subiri kidogo ni lini Tanzania Daima imewahi kukuandika vibaya Mheshimiwa Lucy Magereli? Ndiyo maana huwezi kuona, tunaoandikwa vibaya tunayaona, unapoweka *principle* weka *principle* tu. Sisi tujenge msingi hapa, wanaoingia waukute msingi upo, awe Tanzania Daima, Uhuru, awe nani endelea, Mheshimiwa Lucy. *(Makofi)*

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Daima imefungiwa mara kadhaa na imepewa *penalties* mara kadhaa. Tunaposema tunataka Tanzanite ichukuliwa hatua hatumaanishi kuzuia Tanzania Daima kufanyiwa kitu chochote. Sheria ibaki kuwa sheria kwa nini mna-*defend?* Bahati mbaya kwenye Kiti wewe kama Mwenyekiti na kama Spika unaendelea kutoa aina hii ya ku-*defense what do want out this? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wewe Lucy wewe ngoja sasa, unajua shida yako unajisahau sana. Unapoweka *principle* kama

Bunge, weka *principle*, hawa ni watoto wako, asiyekuwa na adabu yeyote yule achukuliwe hatua. Nimekuuliza swali ni lini wewe Lucy Magereli niletee gazeti la Tanzania Daima umewahi kuandikwa vibaya? Sisi tunaandikwa ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho na Tanzania Daima potofu tupu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapojadili jambo tujadili kwa haki. Ukibeba mtoto wako mgongoni mwingine yupo kifuani hatufikia, kila watu watabeba mtoto wao hapa, itatusaidia nini? Kwa hiyo, wewe jadili hiyo sijui Tanzanite sijui kitu gani lakini tujaribu kuweka misingi kama Waziri alivyotuambia, misingi ya nchi kwenda mbele unaona lakini ukibeba hili zuri, hili hivi na wale wanaoumia upande huu tunafanyaje? *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuanza hapo hapo ulipomalizia habari ya misingi, misingi ipo tatizo mbona haitekelezwi? Sheria ipo mbona haitekelezwi? Inafikaje gazeti linafika linamwandika mtu shoga au linasema huyu ni shoga wa huyu na huyu Serikali inanyamaza kimya? Halafu tunasema kwamba hili ni suala la madai. Hivi kweli mnatarajia Maalim Seif aende Mahakamani kwa suala kama hilo? Mnamtarajia Zitto aende Mahakamani akadai kwamba yeye hamlali shoga huyu au hamlali shoga huyu? Tunafika mpaka hapo? Halafu Mwenyekiti unatetea, halafu unalinganisha, halafu unajaribu kujenga hoja.

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Ally Saleh, hakuna anayetetea, wewe mwenyewe umeeleza vizuri sana ulivyoanzia kwamba sheria zipo kwa nini hazitekelezwa na mimi nipo na wewe hapo, unanielewa? Ndiyo misingi ninayosema na umeanza vizuri sana, hayo mengine uliyoyasema wewe siwezi kuyarudia maana naona unarudia yale yale tena, kama alivyotaja yule na wewe unataja tena yale yale na unataja majina ya watu, kidogo ungekuwa makini.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante yametajwa majina ya watu kwa sababu hili limeletwa Bungeni linajadiliwa.

**MWENYEKITI:** Sasa wewe usirudie maana unakuza.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo la kuwa na magazeti ambayo hayafuati maadili na sheria yatakuja kutukwanza kama ambavyo wengine wamekwazwa. Inafika wakati mtu ataamua la kuamua halafu tutakuja kumlaumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na *principle,* mimi ni *Journalist* tena *professional* na nakubaliana na maadili lakini mbona naona nchi hii imeweka kando maadili na Serikali ipo? Mbona naona nchi hii imeweka sheria pembeni na Serikali ipo? Tusingefika hapa leo kujadili Gazeti na Tanzanite au hata hilo unalosema wewe la Tanzania Daima na mengine, tutofautishe baina ya *critic* na kuchafua watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Tanzania Daima, ni *critic,* wanai-c*riticize* Serikali lakini hawa wanachafua majina ya watu, hiyo ni mbingu na ardhi. Ndiyo maana Mheshimiwa Magereli akasema kwa maana hiyo usifanishe Tanzanite na Tanzania Daima katika picha moja.

**MWENYEKITI:** Unaiua hoja yako, muda umepita. Hoja ilikuwa nzuri unaanza tena kutetea ugonjwa ule ule, yakifanywa na Tanzania Daima sawa, akifanya mwingine siyo sawa, hapo ndiyo kwenye tatizo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Msigwa ni *commitment* ya Serikali na Serikali imeshatoa *commitment* ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema kwamba hata yeye hakufurahishwa na baadhi ya vichwa habari vilivyoonyesha kwenye gazeti hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Msigwa aposema hiyo ni hatua ndogo lazima Serikali iwe na mahali pa kuanzia, haiwezi kuanza mahali pa juu moja kwa moja. Mimi sioni sababu ya Mheshimiwa Msigwa kuendelea kushikilia shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu tayari iko kwenye mchakato wa kufanya hicho anachokitaka. Akitaka apate jibu sasa hivi nadhani sio kitu ambacho kinawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimsihi tu Mheshimiwa Msigwa arudishe shilingi ya Waziri ili Mheshimiwa Waziri aendelee na mchakato ambao tayari amekwishakuunza. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndaki. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, dakika mbili.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba wizi wa fedha za *ESCROW* uliibuliwa na gazeti moja linaitwa *The Citizen*. Sisi upande wa kudhibiti na ufuatiliaji wa makosa ya jinai, ushoga ni kosa la jinai, ugaidi ni kosa la jinai, wizi, mauji ni makosa ya jinai na sisi makosa ya jinai huwa hatufichi wahalifu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye makosa ya jinai fulani akimuua fulani lazima fulani na fulani huyo tufuatilie. Kwa hiyo, hata kwenye masuala ya ushoga tukipata taarifa kupitia chanzo cha chochote cha habari kwamba fulani na fulani wanafanya ushoga na ni kosa la jinai sisi tunapeleleza na mpaka sasa sisi tunapeleleza ili kuona hawa akina Seif na Zitto wanaotajwa kuona kosa hilo la jinai lipo kweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana masuala ya gazeti kuandika watu fulani ni hatari kila siku tuna kitengo cha kukata magazeti ambayo yanahusisha jinai halafu tunafungua majalada tunapeleleza. Kwa hiyo, hawa walivyosema Mheshimiwa Selasini ni gaidi, ugaidi hauna cha kusema huyu akiwa Mkristo hawezi kuwa gaidi, huyu akiwa

Mbunge hawezi kuwa gaidi, huyu akiwa nani hawezi kuwa gaidi na tulikuwa tunachunguza kuona kama Selasini anayedaiwa kuwa ni gaidi kweli lakini tumekuta siyo gaidi, Selasini siyo gaidi. Kwa hiyo na sisi tukichunguza tukabaini kwamba Zitto na Maalim Seif siyo mashoga hatutaendelea na upelelezi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nirudie alichokisema Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kama kwenye upande wa kashfa ambao siyo jinai wale ambao wameumizwa waende Mahakamini, sisi Polisi tuendelee na uchuguzi. Niwahakikishie katika nchi hii yeyote ambaye anatenda kosa la jinai hatutaangalia cheo cha mtu, hatutaangalia dini ya mtu wala nafasi yake katika jamii. Kwa hiyo, hao wanaotajwa hao sisi tunandelea na uchuguzi na tukibaini tutawafikisha Mahakamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, kichwa cha habari kesho hicho. Mheshimiwa Msigwa ndiyo mtoa hoja jamani.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi lakini kama *conclusion* ya rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola, *I think we are not serious* kwenye mambo ya msingi katika nchi. *If is that is the case,* kwa nini gazeti linapewa matangazo na Serikali? Gazeti ambalo linaandika mambo ya hovyo kuliko gazeti lolote katika nchi na mambo ya uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ni-*conclude* kwamba inaonekana hili gazeti ni la Serikali, tuendelee na mambo mengine, mna maslahi nalo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hilo la mwisho la kwako wewe, maoni yako hayo. Mheshimiwa Amina Molel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka tu kupata *commitment* ya Serikali juu

ya michezo kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Kwa sababu mwezi Juni, 2019 Tanzania na hasa tukihusisha Afika Mashariki kutakuwa na michezo kwa ajili ya watu wenye ulemavu lakini sijaona mpaka sasa *commitment* yoyote ya Serikali siyo *TFF* wala sio Serikali. Nataka kujua juu ya suala hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Maelezo mafupi kuhusu michezo ya watu wenye ulemavu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imejitahidi sana kuhakikisha kila mchezo tunauweka juu ya meza na kutoa mchango wetu shahili. Tumeliagiza Baraza la Michezo kuanza maandalizi haraka, ni kama tu ambavyo hivi karibuni tumeweza kusimamia michezo kwa wenye ulemavu wa akili ambapo wametuwakilisha vizuri sana Abu Dhabi na tuliwaita hapa wakati wa bajeti. Nimwombe tu Mheshimiwa Mollel naye tutakapomchangua kwenye Kamati ya kusimamia ya kusaidia kuongoza hii *movement* kuelekea mwezi Juni, asitoe visingizio kwamba hana muda sana. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa tumemaliza upande huo, tuendelee kwenye vifungu sasa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*............Sh.342,760,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning Unit*.............Sh.397,657,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*.........................Sh.118,548,000/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*....Sh.193,851,000/=
Kif. 1006 - *Internal Unit*................................ Sh.117,153,000/=
Kif. 1007 - *Information and Communication Technology*........................................Sh.286,903,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit*...............................Sh.96,941,000/=

Kif. 6001 - *Culture and Development Division*.................Sh.1,424,118,000/=
Kif. 6002 - *Youth Development Division*..............................Sh. 0
Kif. 6004 - *Sport Development* ...................Sh.1,846,574,000/=
Kif. 6005 - *Arts Development Division*.........Sh.2,301,758,000/=
Kif. 7003 - *Information Service*........ ........Sh.13,550,112,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 96 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Kif. 6001 - *Culture Development Division* ...................... Sh. 0
Kif. 6004 - *Sports Development*.......................................... Sh. 0
Kif. 7003 - *Culture Development Division*........ Sh. 6,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linajerea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, taarifa

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako baada ya kukaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji kwamba sasa Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, viongozi wote Wakurugenzi wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya kwa mwaka wa fedha uliopita. Tunajua hata mwaka huu hatujawapa hela ya kutosha sana lakini inatosha, mtajibanabana hivyo hivyo kwa malengo mliojiwekea tunaamini kabisa mtatusongeza mbele. Hii ni Wizara ambayo inatubeba sana haswa kimichezo, kama mnavyojua Watanzania wengi wanapenda sana michezo na macho ya Watanzania yanaelekea *AFCON* - Misri, ni matarajio yetu kwamba timu yetu itafanya vizuri na ikiwezekana itarudi na kombe. Tuwatakie kila kheri katika maandalizi hayo.

Wizara hii pia inalea makundi mengi ambayo yanagusa jamii wakiwemo wasanii wa aina mbalimbali, leo tulikuwa na wasanii wa filamu, Watanzania wengi sana wanafuatilia filamu za hapa Tanzania hasa akina mama. Makazi mengi ukitembelea huko unakuta wanaangalia filamu za hapa nyumbani. Kama walivyosema baadhi ya wachangiaji muziki kizazi kipya nao unazidi kushika kasi, japo wengine bado Sugu akiimba bado sielewi anaimba nini?

Kizazi kipya wengine bado tuko dakika mbili nyuma kidogo lakini mnatusogeza kidogo kidogo tutajiunga tu taratibu kama alivyosema Mheshimiwa Bafadhili kuhusu kinachoimbwa na maudhui yake. Tunatafuta ujumbe sasa kuupata kwa lugha ya siku hizi ni kazi. Kamwaga pombe, sasa unajiuliza pombe kamwaga, kwa hiyo, unajiuliza kuna nini na kadhalika, kumbe wao wana maana zao.

Kwa hiyo, tunawashukuru sana na tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya na mnayoendelea kufanya. Tunawatakia kila kheri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, usivunjike moyo kwamba timu kama *Serengeti Boys* inapopoteza utapata lawama nyingi na kadhalika lakini ni kwa sababu watu wana *expectation* kubwa, hawataki *failure,* wanataka kuona tunashinda, sasa ikitokea, aah, kwenye michezo ipo hivyo. Ndiyo maana hakuna kazi ngumu kama kuwa kocha wa timu ya mpira wa miguu. Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye ni kocha anajua yaani kocha dakika 90 zinakuhumu pale pale, ni ajira fulani ya ajabu sana. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri Wizara, tuko nanyi na sisi kama Bunge tuko tayari kushirikiana nanyi katika magumu yote mtakayokutana nayo kuona namna gani ya kusonga mbele. Wabunge wametoa ushauri mwingi, muende mkauzingatie na muufanyie kazi.

Waheshimiwa Wabunge, pia nichukue nafasi hii kuliambia Bunge kwamba zile taarifa za fedha zilizowekwa hapa kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi zielekee kwenye Kamati zile mbili, Kamati ya *PAC* na *LAAC* zikafanyiwe kazi na maelekezo yetu ni yaleyale asiyetakiwa kukanyaga huko hakanyagi. Maamuzi ya Bunge hayo, Bunge likiamua limeamua.

Mwisho, Kamati ya Uongozi tukutane baada ya kuahirisha shughuli hizi hapa, kuna jambo moja ndogo la kufanya.

Kwa hatua hii tumemaliza shughuli za leo. Kwa kuwa watu ndiyo mmerudi kutoka kwenye Pasaka wengine mmechoka na kadhalika basi jioni ya leo tuweke mambo

yetu sawasawa tayari kukutana kesho saa tatu kamili asubuhi. Kwa jinsi hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.48 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 24 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*